ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais.
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu.
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa.
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa.
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa.
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi.
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole.
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais.
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi.
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae.
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni

51.Mhe. Kazija Khamis Kona Nafasi za Wanawake

52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa Jimbo la Kikwajuni

53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk Jimbo la Kitope

54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid Jimbo la Kiembesamaki

55.Mhe. Marina Joel Thomas Kateuliwa na Rais

56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Jimbo la Mkwajuni

57.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Saba – Tarehe 11 Aprili, 2013

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha hati mezani ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2011/2012.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2011/2012 kwa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa ya mwaka 2011/2012 ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe . Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa).

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, naomba kuwasilisha ripoti mezani ya Kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 52

Ujenzi wa Vituo pamoja na Makaazi ya Askari Polisi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub **-** Aliuliza:

Vituo vingi vya Polisi Zanzibar vimejengwa wakati wa kikoloni katika maeneo ambayo yalikuwa yakizalisha karafuu na nazi katika Kisiwa cha Unguja na Pemba ili kukabiliana na vitendo vya wizi wakati huo.

(a) Kwa kuwa miradi mingi ya Utalii na shughuli za Biashara zipo katika ukanda wa Mashariki ya pwani ya Zanzibar, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za kuishi askari pamoja na vituo ili huduma za polisi zipatikane kwa muda wa saa 24.

(b) Kwa kuwa hatua hiyo itasaidia kukabiliana na uhalifu ukiwemo wa kutumia silaha, kwa nini vituo vinajengwa bila ya kuwepo nyumba za makaazi ya askari na kusababisha usumbufu mkubwa kwa askari wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 52 lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwa kawaida vituo vya Polisi hujengwa kwa kuzingatia mahitaji yakiwemo ya kiuchumi na kiusalama. Mazingatio haya yalifanyika wakati wa ukoloni na hadi sasa. Kutokana na kuongezeka kwa shughuli za biashara na utalii katika ukanda wa Pwani ya Mashariki ya Zanzibar, Jeshi la Polisi lina mpango maalum wa kujenga nyumba za kuishi askari pamoja na vituo vya kufanyia kazi askari hao. Mpango huu unatekelezwa kwa mashirikiano ya karibu na wadau/wafadhili mbali mbali na pia kwa kushirikisha wananchi wenyewe.

Mhe. Spika, miongoni mwa mafanikio ya mpango huu ni kuanzishwa kwa vituo katika maeneo ya Nungwi, Kiwengwa na Paje. Aidha, Jeshi la Polisi kupitia mpango huu limekamilisha ujenzi wa jengo la makaazi ya askari hapo Paje. Kazi hii inaendelea ili kuyafikia maeneo yote muhimu katika ukanda huu wa utalii.
Mhe. Spika, pamoja na juhudi hizo Jeshi la Polisi linaendelea kushajiisha wananchi kushiriki katika Ulinzi Shirikishi/Polisi Jamii katika kulinda maeneo yote ya visiwa vya Unguja na Pemba. Aidha, Serikali imeanzisha kikosi maalum cha ulinzi katika ukanda wa utalii (*Tourism Patrol*) kwa ajili ya kumarisha ulinzi katika maeneo ya ukanda wa Pwani ya Mashariki ambayo hali ya biashara na Utalii imeimarika.

Hata hivyo Mhe. Mwenyekiti serikali imo katika kuandaa utaratibu ulio bora zaidi utakaohakikisha kuwa tatizo la uhalifu katika Ukanda wa utalii unadhibitiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri kwa nini vituo vya Polisi havijengwi sambamba na nyumba za makaazi ya askari jambo ambalo linasababisha kukosekana kwa ulinzi masaa 24 katika maeneo ya sekta ya utalii na ukizingatia hata hii leo huko Pwani Mchangani umetokea ujambazi.

Pili, kwa kuwa nyumba za askari katika maeneo mbali mbali zimekuwa chakavu, tukiangalia nyumba ya Mazizini, Ziwani kwenyewe hata kwa upande wa Pemba Madungu katika bajeti ya mwaka 2013/2014 mna mpango gani angalau nyumba ngapi mtazisaidia.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako ni kweli umuhimu wa kujenga vituo vya Polisi sambamba na kujenga nyumba za makaazi ya askari ili askari waweze kufanya wajibu wao kwa mujibu wa sheria ziliopo. Lakini kutokana na ufinyu wa bajeti ndio ambao unasababisha uwezo mdogo wa kuweza kufanya mambo mawili wakati mmoja. Lakini ushauri huu tunaupokea na utazidi kufanyiwa kazi na serikali ili kuona kwamba askari wetu wanapata nyumba bora za kisasa ili waweze kufanya wajibu wao vizuri na wakati wote kuwahudumia wananchi.

Pili, kuhusu nyumba chakavu za makaazi za askari polisi katika nchi yetu; ni kweli tatizo hili lipo Mheshimiwa lakini hivi sasa katika utaratibu mzima wa uboreshaji wa Jeshi la Polisi nia ni pamoja na kuimarisha na kuwa na majengo ya kisasa yatakayoweza kukidhi mahitaji ya makaazi ya polisi na kuyafanyia ukarabati yale ambayo yapo katika hali mbaya. Mahitaji halisi kwa nia ya kufanya maboresho katika Jeshi la Polisi ni pesa za kitanzania bilioni 294 na Jeshi la Polisi wamekubaliana na serikali ya Jamhuri ya Muungano kwamba kila mwaka waweze kupata bilioni 58 kwa ajili ya maendelezo hayo. Lakini kutokana na ufinyu wa bajeti Mhe. Ndio sababu ambayo inasababisha hadi sasa kazi hii haijafanyika vizuri, lakini tutachukua jitihada kuhakikisha kwamba hatua kwa hatua nyumba hizo zinafanyiwa ukarabati ili askari wetu waweze kukaa vizuri zaidi.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alisema kwamba Wizara yake au serikali haina mpango wa kujenga vituo kwa sasa. Lakini na serikali yetu inajivunia sana na sekta ya utalii na hivi sasa wahalifu wameenea sana katika mwambao wa pwani kuhatarisha maisha ya wawekezaji pamoja na mali zao.

Je, Mhe. Waziri Wizara yako itachukua mpango wa dharura angalau wa kuwakodia nyumba hao polisi wakawepo saa 24 wakafanya kazi zao vizuri.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, sikusema kuwa serikali haina mpango wa kujenga vituo vya Polisi lakini nilichosema serikali ina mpango huo na nia ni kujenga vituo vya Polisi katika maeneo yote ambayo yana uhitaji wa kufanya hivyo, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti ndio inabidi kwenda hatua kwa hatua. Lakini pale tunapopata nguvu za wananchi na wadau basi jitihada hizo huimarishwa zaidi.

Kuhusu mpango wa dharura nilisema hapa kwamba hivi sasa serikali imeandaa mpango maalum au kikosi maalum cha kushughulikia ulinzi katika ukanda ule wa Utalii. Na hivi sasa serikali imo katika mchakato mkubwa sana wa kuhakikisha kwamba inakuja na utaratibu mpya utakaowezesha ulinzi mkubwa zaidi katika maeneo haya ya ukanda wa utalii ili kupiga vita suala zima la uhalifu katika ukanda huo. Mhe. Mwakilishi na Waheshimiwa wananchi tuzidi kuvuta subra wakati serikali inalifanyia kazi jambo hilo, lakini mpango wa dharura upo na hivi sasa inafanyika kazi hiyo.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti kituo cha Matangatuani ni miongoni mwa vituo vikongwe sana vya Polisi hapa Zanzibar, lakini Mhe. Mwenyekiti ukiangalia majengo yake kwa kweli yanasikitisha mno yanamong'onyoka, je serikali ina mpango gani wa kituo kile kukiimarisha kikawa kituo cha kisasa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti nilikuwa naomba arudie kituo cha Matangatuani au kituo gani.

Mhe. Mwenyekiti: Matangatuani.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako kama nilivyosema katika jibu la msingi nia na madhumuni ya serikali ni kuimarisha vituo vya polisi nchini kikiwemo hiki cha Matangatuani. Ni kweli hali yake si nzuri na kinahitaji kufanyiwa ukarabati na nataka mimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba mpango wa jumla wa kuviimarisha vituo hivi upo katika Jeshi la Polisi; tatizo kubwa ni ufinyu wa bajeti, lakini mara zitakapopatikana fedha kituo hiki kitapewa mkazo ili tuwe na kituo kizuri zaidi kiweze kutoa huduma bora kwa wananchi.

Nam. 62

Sekta ya Utalii

Mhe. Jaku Hashim Ayoub Aliuliza:-

Zanzibar inategemea sekta ya utalii kama nguzo kuu ya uchumi, lakini Mei na Oktoba mwaka jana kumetokea vurugu na baadhi ya wageni kusitisha safari zao.

(a) Je, Serikali imepoteza kiwango gani cha mapato yake katika kipindi hicho kabla ya Serikali kufanikiwa kudhibiti vitendo hivyo vya vurugu.

(b) Kwa kuwa vijana wengi hawafahamu madhara ya vurugu, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu kupitia vyombo vya habari kwa manufaa ya Zanzibar na wananchi wake.

(c) Je, wageni wangapi kutoka nje ya nchi walisitisha safari zao baada ya kutokea matokeo hayo ya vurugu Zanzibar.

Mhe Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:

Kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi suali lake namba 62 lenye vifungu 'a' na 'b' kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, hali ya amani na utulivu katika nchi yoyote duniani ni jambo la msingi kwa wananchi wake na wageni wanaotembelea. Kuvurugika kwa hali ya amani na utulivu kunapelekea kuporomoka kwa uchumi wa nchi na hivyo kudumaza maendeleo.

Kwa wageni wanaotembelea nchi hususan watalii ni kawaida kwao kabla ya kupanga safari hutaka kujua hali ya nchi hiyo kiusalama na bila shaka kwa nchi yenye vurugu, wageni hawataichagua kuwa miongoni mwa sehemu ya matembezi na mapumziko yao. Baada ya kutoa maelezo hayo, sasa naomba kujibu kama ifuatavyo:-

a) Wizara yangu kupitia Kamisheni ya Utalii imekusanya sehemu ndogo ya mapato yanayotokana na utalii kupitia ukataji wa leseni pamoja na vibali vya Magari yanayotembeza watalii. Kwa kuwa zoezi la ukataji wa leseni linafanyika mwanzoni wa mwaka katika mwezi wa Januari ni dhahiri kuwa mapato yanayokusanywa kupitia Wizara yangu hayakuathirika. Hata hivyo kwa upande wa makusanyo ya mapato ya ZRB mwezi wa Mei, 2012 mapato yetu yamepunguka kufikia TShs. 8 bilioni ukilinganisha na Makusanyo ya TShs. 10 bilioni kwa mwaka huo huo 2011. Kwa upande wa mwezi wa Oktoba, 2012 takwimu hizo zinaonesha kuwa makusanyo ya ZRB yameongezeka kwa asilimia 4.6% kutoka TShs. 12.2 bilioni kwa 2011 na kufikia TShs. 12.8 bilioni mwaka 2012.

b) Serikali kupitia Taasisi zake inaendelea kutoa elimu kwa vijana na wananchi kwa ujumla juu ya madhara yatokanayo na vurugu na uvunjifu wa amani kwa ustawi wa nchi yetu. Aidha Wizara yangu kupitia Kamati za Utalii za Wilaya tupo katika hatua za kukamilisha maandalizi ya semina na makongamano katika vijiji na mitaa ili kuelimisha wananchi juu ya athari ya vurugu na umuhimu wa kudumisha hali ya amani na utulivu nchini kwa maendeleo ya sekta ya utalii na nchi kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia Baraza hili Tukufu naomba nitoe wito kwetu sisi sote Waheshimiwa Wawakilishi, Wabunge, Madiwani, Viongozi wa kijamii na wananchi kwa jumla kuchukua jukumu na dhima tuliyonayo kuwaelimisha wananchi tunaowaongoza kudumisha amani na utulivu na utengamano kwa nchi yetu.

c) Ni kweli kwamba wakati ule wa vurugu kulikuwepo usitishaji wa safari kwa wageni kwa kuhofia usalama wao. Takwimu zinaonesha kwa kulinganisha vipindi vya viezi inayofuatana takwimu zinaonesha kwamba takwimu zinaonesha kwamba watalii walipungua kwa asilimia 2.5% kwa mwaka 2012 ukilinganisha na mwaka 2011.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri sana ya injinia Mhe. Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Zanzibar kuitangaa Utalii ni maonesho dunia je serikali imejipanga vipi mwaka huu kuyatangaza maonesho hayo kuondoa hofu wageni.
(b) Wizara imetayarisha programu ngapi mwaka huu za kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa amani na utulivu wa visiwa hivi.

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru. Suala la kwanza kwamba kupitia maonesho hayo ambayo Kamisheni ya Utalii na Taasisi za kibinafsi zinahudhuria suala la usalama linazungumzwa kwa kina na tunachukua muda mwingi kuwaelimisha na kutoa taaluma katika maonesho hayo kwamba Zanzibar ni nchi iko salama na haina matatizo. Na niseme kwamba katika maonesho ya karibuni yaliyofanyika Ujerumani kwa kweli washiriki wengi wa utalii wa nje walikuwa wanauliza suala hilo kufuatia vurugu za mwaka jana.

Hata hivyo kwa ustadi mwingi waliweza Wawakilishi kuwafahamisha na kuwatosheleza kwamba Zanzibar iko salama na baada ya kurudi kwao tumeanza kuona matunda ya taarifa waliyoitoa.

Kuhusu vipindi vingapi tumeviandaa mwaka huu Mhe. Mwenyekiti kama nilivyosema katika jibu langu kwamba kuanzia Jumamosi ya kesho kutwa tunategemea kuzindua Kamati za utalii za Wilaya. Kamati hizo zitakuwa na jukumu kubwa sana kuona kwamba katika Wilaya zao shughuli za utalii na hasa masuala ya ulinzi na usalama yanazingatiwa. Kwa hivyo baada ya uzinduzi wa Kamati hizi, sisi na Kamati hizo tutakaa kwa pamoja kupanga ni namna gani tufanye na vipindi vingapi kwa kutumia vyombo gani vya habari viweze kurushwa kwa mwaka 2013/2014.

Tumezizindua hivi sasa kabla ya bajeti wakati matayarisho ya bajeti yanaendelea ili tuweze kupanga pamoja, wao ni kama wadau muhimu katika sekta ya utalii.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti sekta hii ya utalii ni sekta ambayo serikali inategemea sana kuingiza pato la taifa, na tumekuwa tukiona nchi mbali mbali zikitangaza nchi zao katika kuutangaza utalii kupitia vyombo kama vile CNN, BBC, na vyombo vyengine vya kimataifa. Je Wizara ina mpango gani kuitangaza sekta ya utalii au kuitangaza Zanzibar katika vyombo vya kimataifa.

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti ninakushukuru. Ni kweli Mhe. Mwenyekiti shughuli za utalii ni shughuli ambazo zinahitaji kutangazwa sana; ni biashara ambayo bila ya kuitangaza mara kwa mara kwa kweli mafanikio yake huwa kidogo sana. Kwa hivyo na sisi kama Zanzibar kwa sababu tumeamua kwamba Utalii ndio sekta kiongozi kiuchumi lazima tuchukue jitihada hizo kuona kwamba utalii tumeutangaza sana.

Sasa sisi katika Wizara tunafanya kazi hiyo kupitia bajeti ya serikali. Mwaka jana tuliomba hapa bajeti ya kutangaza utalii nchi za nje. Bahati mbaya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliona kama ni safari za kikazi wakazungumza sana hapa katika Baraza la Wawakilishi jambo ambalo Mhe. Waziri wa Fedha kalipokea kwa sababu ni agizo la Baraza hili tukufu, kwa hivyo fedha zile kidogo zikapunguzwa. Kwa hivyo naomba tutazipanga tena, naomba musaidie kusema kwamba hizo fedha ni muhimu zipatikane kwa ajili ya kutangaza Zanzibar nchi za nje na ndipo hapo zitatumika katika pia kupata pesa kutangaza katika vyombo vya habari vya nchi za nje.

Ninakushukuru sana Mheshimiwa kwa *concern* yako.

Nam. 71

Mapambano Dhidi ya Ukimwi

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:

Kwa kuwa malengo ya *Millenium* katika mapambano dhidi ya ukimwi ni kufikia 0-3 (sifuri tatu) kwa maana ya (i) kuondosha unyanyapaa (ii) kuondosha maambukizi mapya na (iii) kutowepo kwa wagonjwa wapya wa ukimwi.

Je, ni kwa kiasi gani Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imejitayarisha kufikia azma hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Alijibu:
Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kwa ujasiri mkubwa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 71 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa Mkakati wa Kimataifa wa mapambano dhidi ya UKIMWI unalenga kuzifikia zero 3 kufika mwaka 2015. Utelekezaji wa mkakati huo ulianza mwaka 2011 na malengo yake ni kuzifikia zero katika maambukizi mapya ya VVU, zero katika unyanyapaa kwa maana ya kusiwepo kabisa unyanyapaa ndani ya jamii yetu na zero katika vifo vinavyoambatana na UKIMWI.
Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa wito huo wa Kimataifa, Mhe Mwenyeiti naomba unilinde Serikali yetu imejipanga kama ifuatavyo:-

1. Tumeshaufanyia mapitio mkakati wetu wa Kitaifa ili kuelekeza nguvu za mapambano katika makundi maalum yenye viwango vikubwa vya maambukizi (zaidi ya asilimia 10%) ukilinganisha na maambukizi katika jamii kwa jumla lakini vile vile mkakati ambao utawashirikisha wadau wote zikiwemo taasisi binafsi.

2. Tunaendelea kuifanyia mapitio Sera yetu ya Kitaifa ya ukimwi ili iendane na mabadiliko ya Mkakati wa Kitaifa ili iwe ndio dira ya mapambano yetu itakayofuatwa na wadau wote katika mapambano hayo. Rasimu iko tayari na karibuni na Mhe. Mwenyekiti Wajumbe wa Baraza lako tukufu walipata fursa ya kupitishwa na kuelekezwa juu ya rasimu hiyo na wao wakatoa maoni yao na hivi karibuni itaweza kufikishwa Serikalini kwa kupitishwa.

3. Tumeshapitia Mkakati wa Mawasiliano na utetezi ili kwenda sambamba na Mkakati wa Kitaifa wa mapambano dhidi ya UKIMWI ambao utekelezaji wake ndio umeanza.

4. Tumo katika mchakato wa kuandaa Mkakati wa utafutaji wa fedha za mapambano dhidi ya UKIMWI (*Resource Mobilization Strategy*) hasa tukitilia maanani kushuka kwa upatikanaji wa fedha kutoka kwa wafadhili za ziada katika kuongeza nguvu za mapambano ili tuweze kufanya utekelezaji zaidi.

5. Tunachukua juhudi za kuwapatia ujuzi na uwezo wadau wetu wote wakiwemo Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti ambao tunashirikiana nao katika mapambano hayo. Aidha walengwa wetu wa huduma zinazotolewa iwe kwa wanaoishi na VVU au makundi maalum wanashirikishwa kikamilifu katika mapambao hayo.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana na ya ujasiri wa hali ya juu yaliyotokana na Waziri wetu jasiri naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa ngono ni moja kati ya mambo yanayosambaza ukimwi nakusudia ngono kwa maana ya *sexual intercourse* na kwa kuwa taaluma ya viumbe inaonesha wazi kwamba *sexual intercourse* ni *hormonal controlled process* yaani ni njia inayoshawishiwa na *hormones*. Na kwa kuwa mavazi huchangia sana kishawishi cha kufanya ngono kwa maana macho huona halafu yakapeleka ujumbe kwa ubongo kupitia mambo yake tena ikabidi ikatoa *testosterone* ambae atakushawishi wewe kwenda kufanya ngono, na kwa kuwa hakuna sheria Mhe. Mwenyekiti katika nchi yetu inayodhibiti nguo za kubana kwa maana ya *tight* pamoja na vimini je, ni lini Mhe. Waziri Wizara yako kwa kushirikiana na Wizara ya Sheria na Katiba pale mkatunga sheria madhubuti sana itakayodhibiti mavazi kwa maana ya hivi vimini kama vile sisi katika Afro Shirazi tulivyomudu kudhibiti mabuga pamoja na chupa.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri alikuwa anasikiliza swali la Mhe. Mjumbe ili aweze kulijibu lakini kutokana na maongezi yetu tunayoendelea nayo inampa tabu Mhe. Waziri kuweza kusikia masuali ya Wajumbe, naomba tu-*concentrate* katika kazi zetu ambazo zimetuleta hapa. Mhe. Mjumbe uliza tena swali lako.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, narudia tena ngono kwa maana ya *sexual intercourse* ni sababu kubwa inayosababisha ukimwi katika nchi. Kwa kuwa ngono kwa maana ya *sexual intercourse* is a *hormonal controlled process* ni *process* inayoshawishiwa na *hormones*, na kwa kuwa kinamama wameshamiri vile viguo vya kubana vile *skin tight* pamoja na vimini ambavyo mwanamme akiona kwa macho hupeleka taarifa kwenye ubongo, na ubongo ukaanza kufanya vitu vyake vya kutoa *testosterones* ambaye anamshawishi mwanamme *either* ende akafanye ngono. Na kwa kuwa hakuna sheria madhubuti inayodhibiti mavazi katika nchi hii, kwa hivyo akina mama mko huru katika suala zima la kuvaa vimini na *skin tight.*

Je, ni lini wizara yako kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria itatunga sheria kali itakayodhibiti vimini pamoja na *skin tight* kama sisi katika Afroshirazi tulivyoweza kumudu kudhibiti mabuga pamoja na chupa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, anayozungumza Mhe. Mwakilishi ni ya kweli, kwamba tendo la ndoa huwa linashajihishwa na mambo fulani. Lakini naomba nimuarifu Mheshimiwa kwamba ndani ya nchi hii tunayo sheria inayokataza vimini, kwa sababu tu suala la mavazi ya *skin tight* ambayo yameingia hivi sasa hili ni jipya halikuweko awali. Lakini nafahamu fika kwamba ipo sheria inayokataza watu kutembea wakiwa hawakujistiri vyema ikiwemo kuvaa vimini. Naomba nimuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba, ofisi yangu kama alivyoshauri itakaa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria kuangalia ni jinsi gani inaweza kurekebisha sheria hii ili iendane vyema na mila na silka za nchi yetu. Lakini vile vile tunaviomba vyombo ambavyo vinasimamia utekelezaji wa sheria kwa hii sheria ambayo ipo inayokataza mavazi ya vimini basi ichukue hatua.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa waziri mwenzangu nimelazimika kutoa maelezo zaidi kwa sababu na sisi Wizara ya Afya suala hili linatuhusu. Naomba kumhakikishia Mhe. Saleh Nassor Juma kwamba suala la mavazi sio sababu ya msingi ya kuongezeka UKIMWI katika jamii. Inaweza ikaonekana tu kwamba ni sababu lakini si vizuri kutoa mfano mbaya hakuna watu wanaojificha nguo kuliko wale wananchi wa Arabuni na India na hawaonekani chochote, lakini bado nchi hizo UKIMWI upo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la maambukizi ya UKIMWI huambatanishwa na tendo la ngono ni moja katika sababu kubwa, lakini sababu kubwa na ngumu ni vita vya nafsi. Kuna kitu Mheshimiwa kinaitwa uhuru na kuna kitu kinaitwa *liberty*, yaani mimi kusimama kusema hapa niliamua niseme, Mhe. Mwenyekiti unaweza ukanambia nisiseme lakini kwa kiburi nikasema. Hili ni gumu, sasa kukwambia wewe unajua kwamba njia ya kutolea choo sio njia ya kufanya tendo la ngono na bado ukafanya huo ni uhuru wako, huna mtu utakaemwambia akaweza kuliweza hilo. Kila mmoja anajua kwamba njia ile ilikusudiwa kitoke kitu sio kingie, mwanadamu yeyote anajua hivyo lakini bado wewe ukaamua kutumia njia ile kuingiza badala ya kutoa hakuna chochote kinachoweza kukuzuia isipokuwa vita vya nafsi yako.

Kwa hivyo, vita vya kupunguza UKIMWI kwa wizara ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Wizara ya Afya ni kuongeza kampeni ya kuwaelimisha wananchi kwamba jambo hilo ni baya. Hakuna asiyejua kwamba ukivuta sigara unapata kensa na tuna madaktari wakubwa wanaojua hivyo na bado wanavuta, utamkatazaje huyo kama si nafsi yake.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kupunguza maambukizi ya UKIMWI ni vita vya nafsi na *moral values* za kidini na ndio maana Wizara ya Afya inawashirikisha mpaka Masheikh kutusaidia katika misikiti na kueleza aya za Qur-an *laa takrabu zzinaa* na bado haijasaidia kwa sababu ni vita vya nafsi. Wananchi kwa kutumia nafasi hii masuala haya ni vita vya nafsi tujitahidi kujikinga wenyewe, mtu anaweza kwenda uchi na bado ukamwambia twende tukafanye tendo la ndoa akakupinga hataki. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Lakini kwa ruhusa yako kabla sijauliza swali ningeliomba kutoa kama indhari tu, kuwa Mwenyezi Mungu katujaalia kuwa na mambo ambayo hayamo katika uwezo wetu. Kwa mfano, haitokezei mtu akafurahishwa asicheke japo kidogo, au akafanyiwa mambo ambayo yanamuathiri na kumuumiza asipige kelele, na mtu aliyekuwa ni makini kama atamkuta mtu ambaye umbile lake ni kama kuwa hakuvaa kitu lazima kutakuwa na *involuntary action* kwa hivyo ipo haja ya kuona kuwa hili suala limepigwa vita.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niulize swali langu la nyongeza. Kwanza nashukuru sana kwa wizara kwa kuweka malengo ya kufikia *zero* katika maambukizi mapya ya UKIMWI, kufikia *zero* katika unyanyapaa na kufikia *zero* katika vifo vilivyokuwa vinasababishwa na UKIMWI. Kwa sababu suala hili la kupambana na UKIMWI halikuanza leo na katika nchi hii takriban kila shehia kuna bango limewekwa linalohusiana na vita dhidi ya UKIMWI. Kwa kazi hii kubwa iliyofanywa hapo nyuma na fedha nyingi iliyotumika. Je, wizara imefanya tathmini gani kuona ni kiasi gani tumefanikiwa katika mapambano haya.

Halafu la pili, kama kweli wizara kwa kushirikiana na wizara husika kama alivyoeleza Mheshimiwa muasisi wa Wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya habari kwa sababu inahusika na kulinda tamaduni zetu, silka na desturi haoni kuwa kwa kuacha huhuru kama ulivyo na kupigana na binafsi tu bila ya kuwa na vitendo ambavyo vinapinga ule ubinafsi wako ulionao suala hili halitoondoka maisha katika nchi hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ofisi yetu kupitia Tume ya UKIMWI imefanya tathmini juu ya shughli nzima ya mapambano na kampeni mbali mbali tokea gonjwa la UKIMWI lianze na shughuli za mapambano zianze kufanyika ndani ya visiwa vyetu. Na ndio maana katika kujibu swali langu mama nimesema kwamba sasa hivi tumeondokan ana ule mkakati wa kwanza wa kitaifa tuliokuwanao ambao ulianza mwaka 2004 na ulimalizika mwaka 2009. Baada ya kufanya tathmini na kugundua sehemu ambayo tumefanikiwa na matatizo yaliyopo tumeweza kuja na mkakati mpya ambao ni mkakati wa pili na ambao umeanza mwaka 2011 na unategemewa kumalizika mwaka 2016.

Kati ya mambo ambayo yameweza kuonekana katika tahmini ni kwamba tumeweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kuweza kuzuia maambukizi ya watu ambao wanaambukizwa UKIMWI na kuyaweka bado kuwa chini ya asilimia moja kwa jamii kwa ujumla, lakini tulichoweza kugundua ni kwamba kuna makundi maalum matatu ambayo ni ya wale wanaotumia matumizi ya dawa haramu hasa kwa kutumia sindano maambukizi yake ni makubwa ni kama asilimia 16, lakini wanaofanya tendo la ngono wanaume kwa wanaume maambukizi ni asilimia 12.3, lakini hata wanawake ambao wanauza miili yao kwa shughuli za kujipatia maisha wao maambukizi ni asilimia 10.8. Kutokana na matatizo hayo mkakati wa pili huu unalenga zaidi kupambana na maambukizi na jinsi gani tunaweza kuondosha tatizo katika makundi haya maalum.

Mhe. Mwakilishi swali lake la pili ameuliza ni jinsi gani tunaweza tukatunga sheria kudhibiti mambo haya ili UKIMWI usienee. Mimi napenda nimshukiri sana Mhe. Waziri wa Afya kwa majibu ya wazi na ya nyongeza aliyoyatoa kutokana na suala la ziada ya Mhe. Saleh Nassor Juma kwamba, na nitapenda sana ninukuu maneno ya Rais wetu Mstaafu Mhe. Abeid Amani Karume alisema hivi: "Kwa bahati mbaya sana UKIMWI umeingia pahala pabaya, paala ambapo panahitaji vita vya nafsi", na ndio hivi Mhe. Waziri wa Afya amezungumzia. Hata tukiwa na sheria kwa sababu tendo la ngono halifanywi hadharani ni la usiri sana ni vigumu kuweza kutumia sheria kulidhibiti, lina ugumu sana. Kwa hivyo, tunachohitaji ni watu kupambana na nafsi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibiwa swali langu Nam. 77 naomba niweke sawa tu kitu kimoja. Wakati waziri anajibu swali la nyongeza alisema anamnukuu Mhe. Rais wa Kwanza Mhe. Abeid Amani Karume wakati Mhe. Karume alipokuwepo ilikuwa UKIMWI hakuna na aliyefanya *quotation* ile ni ya Mhe. Ali Hassan Mwinyi. Hilo ni kwa ajili ya kuweka hansard sawa Mhe. Mwenyekiti.

Baanda ya maelezo hayo sasa naomba swali langu Nam. 77 lijibiwe.

Nam. 77

Vituo vya Kuwatunza Walemavu

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Mara baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha utaratibu wa kuwatunza wazee wasiojiweza kwa makaazi, kuwatunza, kuwaenzi pamoja na kuwapatia mambo yote muhimu katika nyumba za wazee Sebleni. Aidha kulifunguliwa kituo cha kulelea watoto wenye mazingira magumu Forodhani jambo ambalo limeipandisha hadhi Zanzibar katika medani ya kundi la Walemavu lina matatizo mengi na linahitaji msaada sio tu wa kifamilia bali wa Kitaifa na Kimataifa.

Je, ni lini Serikali ya Mapinduzi itaanzisha vituo vya kuwatunza walemavu ambao wanaishi katika mazingira magumu ya hatari.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 77 kama ifuatavyo na kabla ya kumjibu naomba nitoe maelezo ya utangulizi machache sana.

Mhe. Mwenyekiti, Tanzania ni moja kati ya nchi zilizoridhia mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu unaojulikana kwa jina la kigeni *The United Nations Convention of the Rights of the People with Disability*. Tanzania iliridhia mkataba huu mwezi wa Oktoba mwaka 2010.

Mhe. Mwenyekiti, katika ibara ya 19 ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu kuna kifungu na mimi napenda nikinukuu. "Nchi zilizoridhia mkataba huu zinatambua haki sawa kwa watu wote wenye ulemavu kuishi katika jamii wakiwa na maamuzi sawa na wengine, na zitachukuliwa hatua sahihi na zinazofaa kuwawezesha watu wenye ulemavu kufaidi haki hii kikamilifu na kuingizwa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii".

Mhe. Mwenyekiti sasa naomba kujibu swali kama ifuatavyo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina mpango wa kuanzisha vituo vya kuwatunza watu wenye ulemavu kwa kuzingatia kwamba suala la ulemavu ni suala la haki za binadamu. Masuala haya yanahimiza zaidi ushiriki na ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu katika jamii na kuweka misingi ya uhuru, misingi ya kuwatambua, misingi ya kufurahia maisha na kuweza kuondolewa vizuizi vyote kwa sababu ya ulemavu au kutengewa maeneo maalum ya kuishi kutokana na ulemavu walionao.

Mhe. M wenyekiti, watu wenye ulemavu wanahitaji kushiriki katika masuala yote ya kisiasa, kiuchumi na kijamii; wanahitaji kuwajengea maeneo maalum ni sawa na kwenda kinyume na mkataba wa kimataifa wa watu wenye ulemavu na pia sheria yetu Nam. 6 ya mwaka 2006 ya watu wenye ulemavu ya Zanzibar ambayo inakataza ubaguzi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri ambaye juzi tu alipewa nishani ya Mwanamke Jasiri na Wamarekani naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Amesema kwamba serikali haina mpango wa kuwaweka pamoja walemavu kama wanavyofanya kwa wazee na watoto walio katika mazingira magumu. Nashukuru kwamba Mhe. Waziri katika jibu lake la msingi amesema kwamba Sheria Nam. 6 inawataka walemavu washiriki katika mambo kadhaa yakiwemu masuala ya maamuzi na mambo mengine.

Je, ni lini katiba ya nchi itaweka nafasi maalum kwa walemavu katika vyombo vikubwa vya maamuzi likiwemo hili Baraza la Wawakilishi pamoja na mambo ya Madiwani huko. Ni lini serikali itatamka rasmi kwamba kuna *specific amount* za hizi *post* kwa ajili ya walemavu katika Baraza na katika Manispaa na Halmashauri za Wilaya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ndani ya nchi yetu hatuna sheria ambayo inatamka wazi ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu kwenye vyombo vya maamuzi katika ngazi mbali mbali. Wazo alilolitoa sio baya lakini naomba vile vile amezungumzia kwamba ni lini serikali itaweza kuingiza katika katiba na kutambua uwepo wa watu wenye ulemavu katika vyombo hivi. Hili ni wazo ambalo chombo chako hiki kitukufu Mhe. Mwenyekiti, kina uwezo wa kulitafakari na ndilo lenye uwezo wa kuweza kufanya mabadiliko ndani ya katiba ikiwa haja ya kufanya hivyo inaonekana ipo.

Tunachosisitiza sisi ni kwamba, bado tuwaone watu wenye ulemavu ni watu wenye uwezo, watu ambao wanaweza kufanya maamuzi na kushiriki katika shughuli hizi na tayari tunayo mifano katika viongozi wetu kwenye sehemu mbali mbali, katika vyombo vya serikali, lakini hata katika vyombo hivi vya siasa mfano Baraza la Wawakilishi tunao watu wenye ulemavu. Lakini kwa nia ya kuwapa upendeleo maalum nasema hili ni suala ambalo linaweza kuzingatiwa.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuwasaidia walemavu ni pamoja na kuwasaidia kimitaji na karibuni Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilizindua Mfuko wa kusaidia walemavu. Je, ni kiasi gani cha fedha kilichopatikana na ni utaratibu gani utakaotumika kwa kuwasaidia walemavu hao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilichangisha fedha kwa ajili ya kupata Mfuko wa Fedha kwa ajili ya kuwasaidia watu wenye ulemavu. Kiasi kilichopatikana hadi sasa kwa kukadiria ni kama shilingi 250 milioni.

Mhe. Mwenyekiti, ninachelea kutoa *figure* hii kwamba ndio yenyewe kwa sababu wale walioahidi wakiwemu Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wa Baraza lako hili tukufu kuchangia katika mfujo ule bado wengine hawajawasilisha michango yao kwa hiyo kila siku Mfuko unabadilika katika kiwango cha fedha ulichonacho lakini hakipungui shilingi 250 milioni. Tunashukuru kwa hilo lakini nitoe wito hapa kwa wananchi wote na vyombo mbali mbali wakiwemo Wajumbe wa Baraza lako tukufu ambao walitoa ahadi ya kuchangia katika Mfuko huo basi wafanye hivyo.

Pia nieleze kwamba Mfuko huu ni endelevu wakati wowote ule taasisi au mtu binafsi anayehisi anaweza kuchangia katika Mfuko huu ili kuwasaidia ndugu zetu ambao wanaishi na ulemavu tunawaomba wafanye hivyo kwa sababu Mfuko huu unatarajiwa uwe Mfuko endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, awali kabisa tulikusudia Mfuko huu uweze kusaidia kiununua visaidizi mbali mbali ambavyo vinahitajika kwa matumizi ya watu wenye uelemavu. Kwa mfano bakora ambazo zingetumiwa na watu wasiyoona, vingeweza kununuliwa visaidizi vya kuweza kuwafanya wale ambao hawasikii kuweza kusikia, tungenunua baadhi ya vigari kuwasaidia hasa watoto ambao wanakwenda skuli na wanahitaji mahitaji hayo pamoja na vifaa vyengine vikiwemo vya skuli katika kufundishia kwenye masomo ya elimu mjumuiko.

Lakini fedha iliyopatikana ni ndogo kulinga na mahitaji, ofisi hivi sasa inakaa nakupanga jinsi gani Mfuko huo utaweza kutumika kuuwekea malengo, malengo yake yanajulikana lakini kuweza kuuwekea mpango wa utekelezaji wa matumizi ya fedha hizo. Cha kwanza kabisa ambacho ni kipaumbele ni haya niliyozungumza kuwatafutia visaidizi ndugu zetu wenye ulemavu.

Vile vile naomba nimuarifu Mhe. Salma kwamba watu wenye ulemavu wanaweza kupata msaada wa kusaidiwa katika shughuli zao mbali mbali na kupatiwa mitaji ya kufanya shughuli zao kupitia Wizara ya Uwezeshaji

Wananchi Kiuchumi na Ushirika kama wananchi wengine, hawabaguliwi na kwa kweli tunaomba muwasaidie kuweza kufikia ofisi hii ili na wao wafaidike, lakini vile vile kupitia Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto ambako pia kuna baadhi ya fedha zinaweza kupatikana kwa ajili ya kuwasaidia.

Mhe. Hija Hassan Hija: mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Waziri awali ya mchango huu wa walemavu iliambiwa kwamba ni Mfuko wa kuchangia maendeleo ya walemavu. Sasa leo Mhe. Waziri anatwambia kwamba lengo la mwanzo la Mfuko huu ni kuwasaidia walemavu katika kuwapatia vifaa kwa wale wasiyoona, wasiosikia, vigari na vifaa vya masomo. Huoni kwamba kutumia fedha hii kwa malengo hayo ni kukwepa kwa serikali kutoa mchango wa maendeleo kwa walemavu. Wajibu wa kutoa vifaa hivi ulikuwa ni wa serikali kuwapatia vifaa vya masomo na huu Mfuko ungefaa zaidi kuwasaidia walemavu hawa kwa mikopo badala ya kutumia kwa bakora yao. Pengine fedha hizi za kuwapatia vifaa walemavu ni sawa sawa na walemavu kuwapiga kwa bakora yao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba ifahamike vizuri kwamba Mfuko inawezekana jina lake ni hilo la Maendeleo ya Walemavu. Mhe. Mwenyekiti, ili watu wenye ulemavu waweze kuendelea basi kwanza wanahitaji kuwezeshwa wao wenyewe kuweza kujihudumia. Kwa mfano, mtu kama hawezi kutembea cha kwanza cha kumsaidia ni kuweza kumpatia uwezo aweze kutembea kama ni magongo au kigari. Lakini kwa ambaye haoni ni kuweza kumsaidia kisaidizi ili aweze kutoka. Hiyo ni hatua ya kwanza katika kuleta maendeleo kwa watu wenye ulemavu mengine yatafuata baadae, na kwa sababu Mfuko huu ni endelevu kwa hivyo tunaanza na lengo la kwanza kabisa. Ofisi yetu imeona umuhimu wa kutoa kipaumbele kwanza kabisa ni kuwawezesha watu wenye utemavu waweze kupata visaidizi ili na wao waweze kushirikiana na jamii kikamilifu.

Suala la kuwapatia elimu Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Hija atakuwa amenisikia katika fedha hizi zimo fedha ambazo tunanunua vifaa kwa ajili ya kuwapelekea wanafunzi katika skuli zinazofundisha elimu mjumuisho hasa wale ambao wanatumia brain kwa ajili ya kuwasaidia.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo kutoa tanbihi kabla ya kujibiwa swali langu. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kutemblea Kisiwani Pemba kuonana na Wakuu wa Wilaya pamoja na Masheha kuhusu suala la vitambulisho. Hili nampongeza Mhe. Waziri na asione kama ninamkwaza kwa sababu hili suakla ni la kiaifa na wananchi wanahitaji kupata Vitambulishi ili kuielewa serikali yo kwamba inawajali wananchi wao. Baada ya hayo namuomba Mhe.Naibu Waziri ajibu swali langu Nam. 66 ahsante.

Nam. 66

Mchakato wa Vitambulisho vya Taifa

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi – Aliuliza:

Hivi sasa nchi yetu inaanza mchakato wa kupatikana kwa vitambulisho vya Mtanzania, lakini kwa bahati njema Zanzibar yenyewe tayari ina vitambulisho vyake na wazanzibari wengi tayari wamefikia umri wa kuwa na kitambulisho hicho cha Mzanzibari na hawajafanikiwa kukipata na wakati mwengine ni kutokana na usumbufu wa baadhi ya masheha tu.

(a) Je, hatuoni kwamba tutawafanya wananchi wetu hasa wake ambao hata kile cha Mzanzibari hawajawanacho wachanganyikiwe.

(b) Kwa nini serikali haifanyi juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba Wazanzibari wote wenye sifa wanapata vitambulisho vyao vya Mzanzibari kabla ya kutengeneza utaratibu wa vitambulisho vyengine.

(c) Kwa nini baadhi ya Masheha wana misimamo ya ajabu inayojenga usumbufu wa kupatikana kwa vitambulisho hivi, mwananchi anaweza kupata njia nyengine hii ya kwao.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi swali lake Nam. 66 lenye vifungu a, b na c kama ifuatavyo:

Na mimi naungana na Mhe. Mwenyekiti kumpongeza sana Mhe. Mwanajuma na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kuanzia kwa majimbo ya Pemba ambaotulifanya ziara ilikuwa mafanikio sana ya kuona matatizo ya upatikanaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi kule Pemba. Kwa kweli tumeona pale palikuwa na matatizo kwa pamoja tumeweza kutoa miongozo ili kufanikisha zoezi lili

Sasa kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa swali lake nambari 66 kama ifuatavyo:

(a) Ni kweli kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeanzisha mchakato wa utoaji wa vitambulisho vya taifa. Vile vile Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutoa vitambulicho vya Mzanzibari Mkaazi. Vitambulisho vyote viwili vinatokana na haki ya kisheria zilizotungwa na Baraza lako la Wawakilishi Zanzibar na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, kila kitambulisho kina lengo lake liliwekwa ndani ya sheria hiyo husika. Si kweli kwamba kwa baadhi ya wananchi kupata kitambulisho cha taifa kinawafanya wachanginyikiwe kwa vile bado hawajakamilisha utaratibu wa kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Ninakubali umuhimu wa wananchi wa Zanzibar kuwa na vitambulisho vyote viwili kama Watanzania.

b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kufanya juhudi kubwa tena za makusudi katika kuhakikisha kwamba kila Mzanzibari Mkaazi aliyetimiza sifa anapata haki ya kupata kitambulisho hicho. Miongoni mwa jitihada hizo ni pamoja na kuweka afisi za usajili katika kila wilaya ili ziwe karibu na wananchi.

Aidha, serikali inatoa elimu kwa njia za vipindi vya redio na televisheni kuhusu wajibu wa wananchi kujiandikisha na kupata kitambulisho hicho.

c) Mhe. Mwenyekiti, sheria ya vitambulisho ya Mzanzibari Mkaazi inampa jukumu Sheha kuthibitisha ukaazi wa muhusika. Hii ni moja ya sifa ya msingi ya kuwa na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Hata hivyo, iwapo Mzanzibari Mkaazi yeyote ambaye anahisi kuwa hakutendewa haki na Sheha kifungu nambari 13 (1), (2) cha sheria ya Usajili wa Mzanzibari Mkaazi inampa uwezo muhusika kukata rufaa kwa Mkurugenzi wa Usajili na iwapo hakuridhika anaweza kukata rufaa kwa Waziri husika. Rufaa zote hizo zitasikilizwa kwa mujibu wa taratibu na sheria ziliopo.

Naomba kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi pamoja na kulihakikishia Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, kwamba hakuna mwananchi yeyote atakayenyimwa haki yake ya kupata kitambulisho hicho iwapo atatimiza masharti yaliopo katika sheria.

Si kweli kwamba Masheha wana misimamo ya ajabu bali wanajitahidi kusimamia sifa na taratibu zilizoekwa katika sheria ya Mzanzibari Mkaazi. Uzoefu umeshaonesha wazi kwamba wapo baadhi ya watu wanaotaka kuvunja taratibu na kupata vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi kwa njia ya hadaa.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri labda mimi nichukue fursa hii kukupongeza sana kwa ziara uliyofanya kisiwani Pemba wilaya zote nne. Siku ya mkutano wako na Wawakilishi, Madiwani, Masheha na Afisa Vitambulisho pamoja na wewe mwenyewe pale ukumbi wa Benjamin Mkapa, maafisa wa vitambulisho wa Wilaya ya Wete walivileta vitambulisho mbele yetu kama vitambulisho hivi havijachukuliwa.

Lakini kutokana na ziara yako ile na mafanikio makubwa lakini bado utata upo mkubwa sana. Wananchi wanapokwenda kuvifuata vitambulisho vyao wanaambiwa havipo na siku ile ya mkutano wetu tulioneshwa hadharani.

Je, kama havipatikani na wananchi wanashindwa kwenda kuvipata vimekwenda wapi na siku ile vyote vimeletwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Hassan swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.
Kwa kweli hilo suala unalolinipa hivi sasa ni jipya kwangu. Sasa kwa sababu tulikwenda tukakubaliana sote na tukaagiza utaratibu wa kufuatwa. Sasa kama kuna mambo yametendeka kinyume basi wacha Mhe. Mwenyekiti, tufuatilie tuone kwamba tatizo lipo wapi, tulikwamue kama yule ambaye kitambulisho chake kipo na akaweka finger print pale kikamruhusu kama kweli ni yeye, apewe tu hakuna tatizo.

Kwa hivyo namshukuru Mhe. Mwakilishi kwa kunitanabahisha tutafuatilia kwa pamoja.

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuuliza swali la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Waziri alipotueleza alitupa takwimu ya vitambulisho ambavyo havijachukuliwa katika sehemu mbali mbali za Zanzibar hii. Jee, kwa kipindi hiki ambacho ametupa takwimu hizo ni vitambulisho vingapi wenyewe wamekuja kuvichukua na ambavyo havijachukuliwa; serikali ina mpango gani kwa vitambulisho hivyo na pengine wenyewe wahusika hata hapa nchini hawapo. Kwa hivyo serikali ina mpango gani kwa vitambulisho hivyo, vitakaa mpaka lini.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Marina Joel Thomas swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kweli kwa sasa sina takwimu sahihi ya vitambulisho ambavyo vimeshachukuliwa tokea baada ya ziara yetu ile. Lakini tulichogundua wakati ule kwamba vitambulisho ambavyo havijachukuliwa ni pale tulipobadili baada ya mwanzo vile tulichapisha vyengine, sasa watu wakachukue hivyo vyengine wengi hawakwenda, hao ni aina moja ya watu.

Aina ya pili ya watu, wengine hawapo nchini, wapo Dubai, Mombasa, Tanga, sasa wale nao kwenye orodha wapo lakini Masheha wanawatambua kwamba hawapo nchini lakini hawajaja kuchukua vitambulisho vyao. Kwa hivyo *category* hiyo ya watu hao ipo. Sasa sisi tulichofanya tulichokubaliana kwamba orodha yote itayarishwe kila Shehia, halafu Sheha achukue orodha ile kuwatafuta hao watu.

Lakini kama nilivyosema kwamba wengine hawajajitokeza kama Mhe. Mwakilishi alivyosema labda wengine havionekani, hata hivyo tutakwenda awamu ya pili kuona na zoezi hili baada ya Pemba sasa tutafanya na Unguja pia kuweza kuhamasisha nao wananchi wachukue vitambulisho vyao.

Mhe. Omar Ali Shehe: Nikushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kwa kufanya ziara kwenye kisiwa cha Pemba katika Wilaya yangu kwa suala zima la kuhamasisha vitambulisho.
Mhe. Mwenyekiti, mgogoro tunaozungumzia wa masuala haya ya vitambulisho katika Baraza lako hili linatokana na ugumu wa masharti yaliomo katika sheria ya vitambulisho ambapo muhusika hulazimika katika masharti hayo, muhusika hulazima ni lazima kuwa na cheti cha kuzaliwa.

Kitu ambacho tunakubali kwamba kabla ya masuala haya muamko wa wananchi wa kuwa na vyeti vya kuzaliwa katika nchi yetu ulikuwa ni mdogo sana, kitu kilichopelekea kuna wimbi la vijana wengi waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi hawana vyeti vya kuzaliwa.

Sasa kwa vile suala la kuwa na vitambulisho ni suala la kisheria na kukosa kitambulisho ni kosa la kisheria. Kwa nini serikali haifikirii kufanya mabadiliko au kufanya marekebisho ya sheria ili kuilainisha sheria na ukamuwezesha mtu kutumia kitambulisho cha aina yoyote ile kinachoweza kuthibitisha Uzanzibari wake pamoja na umri wake kama vile wanavyofanya Bara kule ama Tanzania kwa jumla.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Ali Shehe swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kweli ukilinganisha na masharti ya kitambulisho cha Mtanzania ambapo juzi sote hapa tulikwenda tulitakiwa mpaka *certificate* za skuli, *certificate* gani. Mimi naona haya ya Mzanzibari Mkaazi ni ya msingi na ni mepesi mno.

Ulilosema Mhe. Mwakilishi kwamba kama hana cheti cha kuzaliwa imeekwa provision akale kiapo. Sasa hata hiyo kwenda kula kiapo anaona taabu, labda gharama basi Mhe. Mwakilishi wasaidie watu wako zile gharama zilizoekwa wale kiapo kuthibitisha.

Sasa tutaamini vipi, hiyo ndio *principle* kama huna cheti ule kiapo. Sasa kula kiapo tu hawezi. Mimi nafikiri haya ndio mambo ya msingi kabisa na baya zaidi Mhe. Mwenyekiti, anachogomba kuwa watu wanadanganya, tumekamata *birth certificate* kwa maelfu *forgeries* kabisa, mtu anaandika saini za Topewala kishaondoka siku ngapi kabisa, vyengine havina hata vile muhuri.
Na hii *trend* ndio tuliyonayo watu wanadanganya vyeti vya skuli na hivyo vyeti vya kuzaliwa vinadanganywa hatari kabisa. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Nam. 78

Uvamizi wa Eneo la Skuli ya Shamiani

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza**:-**
Eneo la Skuli ya Sekondari ya Shamiani mpya tayari limevamiwa na wananchi wakiwemo baadhi ya Maafisa Waandamizi wa Serikali waliomo kazini na wengine wameshastaafu. Kwa kuwa baadhi yao wameshajenga majengo ya kudumu katika ardhi ya skuli hiyo jambo ambalo linapunguza eneo la skuli na hatimae linaweza kuharibu hata mazingira ya kujifunza katika skuli hiyo.

(a) Je, Serikali inalifahamu jambo hilo.
(b) Kama inalifahamu ni hatua gani za kisheria zimechukuliwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:-**
Mhe. Mwenyekiti**,** kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 78 lenye sehemu (a) na (b) kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, eneo la Skuli ya Sekondari ya Madungu iliyopo Chake-Chake limejengwa wakati majengo yanayozungumzwa tayari yameshajengwa na yamepata kibali au hati miliki za serikali. Kwa hivyo inaonekana eneo lililotolewa hati miliki kwa matumizi ya ujenzi wa skuli, eneo hilo hilo likatolewa hati miliki kwa ujenzi wa nyumba hizo zilizojengwa.
Baada ya maelezo hayo, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi Kusini hivi ifuatavyo:-

a) Serikali inalifahamu jambo hilo.

b) Mhe.Mwenyekiti, hakuna hatua za kisheria zilizochukuliwa dhidi ya taasisi hizo au muhusika kwa sababu taasisi hizo zimejenga nyumba zao kabla ya Wizara ya Elimu haijajenga hilo jengo la *secondary* school iliopo hapo. Hatua za ufuatiliaji tunazozichukua sasa si za kisheria bali za makubaliano kati yetu sisi na huyu mjumbe mmoja aliyejenga nyumba binafsi katika eneo la skuli. Huyu naye pia alikuwa anayo hati miliki. Sasa kama tutachukua hatua za kisheria ni sawa sawa na wizara moja kuishtaki wizara ya pili jambo ambalo kwa maadili yetu halifanyiki wala halikubaliki.
Tunachokizungumza sasa ni kuonana na Mwanasheria Mkuu atusaidie kutupa ufafanuzi wa suala hili ili mazungumzo yetu tunayozungumza kati yetu sisi na huyu mtu binafsi aliyejenga tulimalize suala hili. Lakini pia katika eneo hilo kuna nyumba za serikali, kuna nyumba iliyojengwa kwa ajili ya makaazi ya Mkuu wa Polisi lakini vile vile kuna nyumba iliyojengwa kwa ajili ya Mkuu wa Afisa wa Mahakama. Sasa tunalifuatilia kwa utaratibu uliokuwa nje ya kushtakiana. Ahsante sana.

Mhe.Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jibu zuri la Mhe. Waziri mzee wangu pale na makini sana naomba kuuliza swali moja dogo sana la nyongeza.
Kwa kuwa kuna taarifa kuwa skuli ilipata hati miliki mwanzo kuliko taasisi nyingi alizozitaja. Jee, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba taasisi iliyotoa hati miliki kwa mara nyengine kwa taasisi nyengine zilifanya makosa na sio mjenzi.

Pili, kwa kuwa ardhi nyingi za skuli za serikali na vyuo vya elimu kwa kiasi kubwa vimevamiwa na wafanyabiashara na wananchi na wengine tayari wamejenga majengo kama vile ma-*hall* ya mikutano na starehe nyengine pamoja na maduka, jambo ambalo lina-intevene yale mazingira ya kujifunza na kufundishia.

Jee, kuendelea kuyaacha majengo yale ya starehe karibu na skuli si kuzidisha kuteremsha kiwango cha elimu katika nchi hii.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kujibu swali la Mhe.Mwakilishi lenye vifungu (a) na (a) kama ifuatavyo.

a) Ni kweli kabisa kama nilivyosema na nilivyokuwa ninajibu suala la msingi kwamba wizara yangu ilikuwa ina hati miliki ya eneo hilo na baadhi ya sehemu ya eneo hilo limekuwa limeshaanza kutumiwa kujengwa Skuli ya Wawi, lakini kwa bahati mbaya sana taasisi hiyo hiyo ya ardhi ikatoa hati miliki kwa kuwapa watu wa Polisi, Mahakama pamoja na huyu mtu binafsi. Hilo nililisema na nakubali hoja kwamba ilikuwa ni kosa.

   Lakini nikasema suala hili hatuwezi kwanza kulipeleka Mahakamani au katika vyombo vya sheria kabla hatujapata kwanza kuonana na Mwanasheria Mkuu kuzungumza ili tukapata ufumbuzi uliokuwa nje ya Mahakama.

b) Ni kweli kabisa kuna taasisi za watu, mtu binafsi wanaojenga katika maeneo ya skuli au karibu na skuli na wanajenga nyumba za starehe na huko kufanya *disturbances* au kurudisha nyuma viwango vya elimu. Nakubaliana na wazo hilo.

   Lakini nasema hivi zile nyumba zinazojengwa katika maeneo ya skuli tunazizuia kadri tulivyojua na tulivyoambiwa na tulivyoona, almuradi nyumba hizi zilizojengwa maeneo hayo yanayojengwa hawana hati miliki. Masuala hayo tunayapeleka kwenye kesi ya ardhi, maana anayejenga ni mtu binafsi hana hati miliki ya eneo hilo na sisi wa skuli ndio wenye hati miliki, kwa hivyo jambo hilo tunalifuatilia na Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mwakilishi kama anazo nyumba au taasisi nyengine ambazo hatujazifuatilia kwa kuwa hatuzijui tusaidiane tuzifuatilie na tutafute maamuzi ya kisheria kwa eneo hili maamuzi yapo na ni rahisi kuyafuata.

Nam. 50

Ujenzi wa Kituo cha Afya Shehia ya Piki

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:
Wananchi wa vijiji vya Bagamoyo, Shenguju, Matuuni na Mchangani katika Shehia ya Piki – (Jimbo la Mtambwe) wanajenga kituo cha afya ambacho kimo katika hatua ya kumalizika, lakini bado hawajapata msaada wa kumalizia kama walivyoomba.

a) Wizara imelichukuliaje suala la ujenzi wa kituo hicho.

b) Uamuzi wa wananchi hao kuchukua jitihada ya kuanza kujenga kituo hicho ili kujiondolea shida katika huduma za afya, haukuwa sahihi.

c) Wananchi wajitahidi vipi zaidi ya walivyoonesha katika kujiondolea shida ndio wapate kusaidiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 50 kama ifuatavyo.

Kwanza ningependa kutoa maelezo kidogo kwamba ninapenda nimpongeze Mhe. Mwakilishi kwa juhudi na wananchi wa Kijiji cha Bagamoyo Shengejuu, Matuuni na Mchangani kwa uamuzi wao waliochukua wa kutaka kujiletea afya bora karibu nao. Kwa kuchukua jitihada ya kuanza kujenga kituo hicho ili kujiondolea shida katika huduma za afya katika Shehia yao ya Piki, uamuzi wao huo ulikuwa ni sahihi kabisa. Wizara inalichukulia jambo hilo ni la kimaendeleo ambalo wananchi hao wamelifanya.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya kwa kuthamini nguvu za wananchi na kutaka wawe na afya bora imekusanya takwimu kutoka wilaya zote za Zanzibar kujua ni vituo vingapi na nyumba ngapi za wafanyakazi ambazo zinajengwa na wananchi na zipo katika hatua gani. Baada ya kutambua zoezi hilo linalofuata ni makisio ya uamalizaji ujenzi na ifahamu idadi ambayo itamudu vituo na nyumba ngapi kumaliza kwa mujibu wa bajeti itakayokuwa nayo. Hatimaye kila mwaka wizara iweke bajeti ya shughuli hiyo, kwani kujenga ni jambo moja na kuvihudumia ni shughuli nyengine.

Baada ya hayo kufanyika vituo hivyo vinatakiwa vijumuishwe katika idadi ya vituo vya wilaya kwa ajili ya kupata samani, vifaa tiba, mgao wa madawa na wafanyakazi pia panahitaji nyumba ya wafanyakazi. Wizara ipo katika hatua ya kuratibu hayo na ili hayo yafanyike yanahitaji yawemo katika bajeti ya wizara. Baadae kwa kiasi gani kidogo kidogo wizara iyaweke katika mipango yake ikizingatia uwezo wa serikali.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na kuwa Mhe. Naibu Waziri leo sikumsikia vizuri katika majibu yake. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri anakijua hiki kituo kilivyo alikwenda ninashukuru sana, Kamati ya PAC hivi karibuni imekwenda na kukiona hiki kituo na Kamati imeona huruma sana mpaka ikamtaka maafisa wa kule Pemba wizarani waliokuwepo kutokana na hali ya kituo kilivyo, kwa hivyo angalau wasaidie kwa samani ili kituo kile kiweze kuhamiwa hivyo hivyo mashaka mashaka na nikianze kazi na mambo mengine yafuate baadae.

Mhe. Mwenyekiti, yule alikubali kufanya hivyo, ni sababu gani iliyofanya mpaka leo hakujapelekwa samani ya aina yoyote.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, vituo vinapojengwa na Wawakilishi na Wabunge yanakuwa ni maamuzi ya sehemu husika, wanakuwa tayari wao wenyewe wameshajipanga kwamba wanataka kujenga kituo, wengine wanakuja Wizara ya Afya kutaka ushauri, wengine wanaamua kujenga wanavyotaka wenyewe.

Hata hivyo, kituo chao cha Mtambwe walikuja Wizara ya Afya wakapewa ramani wakiwa wamejidhatiti wanajenga. Bahati mbaya wameshindwa kukimaliza. Sasa kama nilivyomueleza kwamba baada ya kuwaona wameshindwa na wametuomba tunafanya tathmini tutajenga.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuweza kunipa nafasi hii asubuhi kuweza kumuuliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri katika suala lake alisema kwamba wamefanya utafiti au wamefanya Wilaya zote vituo ambavyo vinajengwa pamoja na nyumba na madaktari zilizokuwa zinajengwa. Jee, Mhe. Naibu Waziri utatueleza ni hesabu ya vituo vingapi ambavyo tayari vimeshakamilika na nyumba ambazo za madaktari ambazo zimekwishakujengwa.

Lakini swali la pili, Mhe. Naibu Waziri aliwasifu sana wananchi ambao wenye kuanza ujenzi huo wa vituo pamoja na nyumba za madaktari. Jee, Mhe. Naibu Waziri wizara yake inatoa msaada gani ambao wananchi pale ambapo wanapokuwa wanaanza kujenga mpaka wanapofikia wizara yake inatoa msaada gani ili kituo kukamilika.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ninapenda nimjibu Mhe.Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Nimesema kwamba baada ya kuona hilo tatizo tumefanya tathmini, tumejua ni nyumba ngapi, vituo ni vingapi. Tunafanya makisio ili tujue vitahitaji kiasi gani na tukishajua tuweke kwenye bajeti, tukisha kuweka kwenye bajeti tutaangalia uwezo tutakaokuwa nao ndio utakaotuelekeza tujenge nyumba ngapi na vituo vingapi kwa mwaka ule.

Sijasema kwamba vituo vimeshajengwa wala nyumba zimeshajengwa, zile ambazo zimeshajengwa na wananchi au Wawakilishi katika sehemu zao, sikusema hivyo.

La pili anauliza tunawasaidiaje. Pale wanaporipoti na wanapoanza kujenga wenyewe kule vituoni hawaji kwetu kuomba msaada, wanaomba maelekezo wajenge vipi. Hakukuwa na taratibu kwamba wanapojenga sisi tunawasaidia. Lakini kwa kuwa vinawashinda vikiwashinda tutawasaidia tumeshaamua kufanya hivyo. Kwa hivyo kama ana kituo kimemshinda tutamsaidia.

UTARATIBU

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi niliuliza kuhusu vituo ambavyo vilivyokwisha, ina maana anataka kuniambia Mhe. Naibu Waziri mpaka hivi sasa hakuna vituo ambavyo vilivyokwisha kujengwa, nilitaka idadi yake na nyumba ambazo zilizokwisha kujengwa za madaktari, ina maana hivi serikali haikuwa na mpango wa kujenga kituo chochote katika wilaya zilizojengwa zikisha pamoja na nyumba. Nilikuwa ninataka kujua hivyo tu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, labda sikuwa nimefahamu lakini kama ni hivyo Kaskazini A kuna kituo cha Kikobweni kimemalizika, Chaani Kikobweni. Kati kituo cha Ghana na Mwera Pongwe. Kusini kuna *maternity* cha Bwejuu. Magharibi kuna kituo cha Chuwini. Pemba Micheweni, Msuka na Kifundi hivyo vipo katika maendeleo ya kumalizia. Wete vya Mjini Kiuyu, Maziwani na Bagamoyo ambavyo vipo katika stage vya kumalizwa. Mkoani ni Michenzani, Makombeni, Mizingani, Kiwani, Tasiri hivyo vipo katika stage vya kumaliza.

Chake-Chake ni Ndagoni, Mbuzini, Matale na Vikunguni. Hivyo ni vituo sasa hivi vimo katika mradi wa kumaliziwa. Lakini vilivyokwisha kumalizika ndio hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Waheshimiwa Wajumbe muda wa maswali umemalizika.

Sasa naomba kumwita Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais kuendelea na utaratibu.

TAARIFA ZA SERIKALI

Taarifa ya Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2011/2012

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, awali kabisa naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu mwingi wa Rehma, kwa kutujaalia kuwa na afya njema leo na kuweza kukutana tena katika Baraza letu hili tukufu.

Aidha, nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuwasilisha taarifa hii muhimu inayohusu Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa mwaka 2011/2012.

Pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa kazi yao nzuri ya kutuongoza katika mambo mbali mbali.

Vile vile niwashukuru na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri ya kusimamia shughuli za kujenga nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kusikiliza na kupokea mambo mbali mbali yanayoibuliwa na Kamati za kudumu na Kamati nyengine za Baraza hili, kwa ajili ya kuzifanyia kazi na kutafuta ufumbuzi wa matatizo mbali mbali yanayowakabili wananchi wetu, ili kujenga mustakbali mwema wa nchi yetu.
Mhe. Mwenyekiti, serikali itaendelea kulipongeza Baraza lako na Wajumbe wa Baraza hili katika kuhakikisha kuwa maovu yote yanapigwa vita na utendaji kazi wa serikali unakuwa wa ufanisi na tija, ili kuwahakikishia kwamba tunatoa huduma bora kwa wananchi wetu, kwa ajili ya maendeleo ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Nia ya serikali ni kuleta mabadiliko makubwa ya kiutendaji ndani ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga kupambana na maovu yote na kuhakikisha kwamba utekelezaji unakua kwa uadilifu na haki inatendeka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa nitoe kwa muhtasari maelezo ya utekelezaji wa maagizo yanayotokana na Ripoti ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara yetu hasa hasa yalikuwa ni maagizo manne makuu kama yafuatavyo:

1. Baraza la Wawakilishi likamilishe ujenzi wa ofisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba, kwani mjenzi tayari ameshalipwa fedha zote za ujenzi za shilingi milioni 5.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa ofisi ya Baraza la Wawakilishi huko Pemba tayari umekamilika na ofisi hiyo tayari inatumika kwa shughuli hizo zilizokusudiwa.

2. Ujenzi wa Ofisi ya Tume Pemba usimamiwe na Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Pemba na usisimamiwe na Makao Makuu Unguja.

Utekekezaji

Mhe. Mwenyekiti, ujenzi wa ofisi hiyo utasimamiwa na Ofisi ya Tume ya Uchaguzi Pemba. Lakini matayarisho ya ujenzi huo, kama kuitisha zabuni, malipo ya fedha na huduma nyengine za ujenzi huu zitasimamiwa na Tume Makao Makuu Unguja.

Maelezo ya ziada, kutokana na Ofisi ya Tume Pemba haina bodi ya zabuni wala *vote* yake ya fedha, kwa hivyo itakuwa ni vigumu kwa shughuli nyengine kufanyika Pemba na ndio maana Ofisi Makao Makuu inasimamia baadhi ya shughuli hizo.

3 Tume ya Uchaguzi iongeze juhudi katika kutoa elimu ya uraia na elimu ya kujiandikisha katika daftari la kudumu la kupiga kura.

Utekelezaji

Tume ya Uchaguzi imeandaa mpango wa kutoa elimu ya juu, juu ya umuhimu wa daftari la kudumu la kupiga kura. Adha, kwa kushirikiana na Wizara husika, pia itaendeleza mipango na juhudi katika kutoa elimu ya uraia.

Kwa upande wa daftari la kudumu la kupiga kura, Tume ya Uchaguzi imeandaa mpango wa kutoa elimu hiyo, ili wananchi waelewe umuhimu wao wa kujiandikisha.

4. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais isiwasahau wananchi walio hai na ambao wameathirika na maafa ya MV Spice Islander One.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya zoezi la kuwalipa waliopatwa na maafa kukamilika, waliohusika wote walio hai na waliokufa wataorodheshwa na serikali, ili kuwekwa katika kumbukumbu maalum. Pia taratibu za ujenzi wa uzio katika makaburi ya waliopatwa na maafa huko Kama ili kulihifadhi eneo hilo inaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Taarifa ya Utekekezaji wa Maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi, katika ofisi yetu ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kipindi cha *quarter* mbili zilizopita.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa tukiwa na afya njema. Aidha, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha utekelezaji wa maagizo mbali mbali yaliyotolewa na Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, natoa shukrani za pekee kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa na Kamati ya Kusimamia Hesabu za Serikali. Kamati hizi chini ya uongozi wa Wenyeviti wao, kwanza ni;

1. Mhe. Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura
2. Mhe. Omar Ali Shehe Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake kwa ile Kamati ya (PAC)

Mhe. Mwenyekiti, Kamati zimekuwa zikitusaidia sana katika kutuongoza na kutushauri, ili kufanikisha utendaji wa shughuli zetu kwa ufanisi mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu, kwa kuweza kuchangia hotuba zetu na hoja ambazo tunazowasilisha hapa Barazani na kutoa miongozo inayotusaidia katika utendaji wa kazi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya maagizo 41 yalitolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati au Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza. Maagizo yote yameweza kufanyiwa kazi na ofisi yangu. Aidha, michango na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wajumbe, imekuwa chachu kwa ofisi yangu katika kutekeleza mipango ya serikali kwa wakati na ufanisi.

Utekekezaji wa Maagizo

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kwa ruhusa yako niwasilishe kwa ufupi utekekezaji wa maagizo yote 41 yaliyotolewa na Baraza lako tukufu. Aidha, jadweli lililoambatanishwa limeeleza kwa kina utekekezaji wa agizo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi yetu imeendelea na juhudi za utoaji wa elimu kwa wananchi, juu ya umuhimu wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na taratibu za upatikanaji wake kwa mujibu wa sheria. Elimu hiyo hutolewa kwa kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar, yaani ZBC pamoja na redio binafsi ambazo ni Zenji FM na Hits FM. Aidha, vipindi hivyo hurushwa hewani na ZBC mara mbili kwa wiki. Siku ya Jumanne na Jumapili kuanzia saa 1:30 usiku.

Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, imo katika hatua za mwisho za maandalizi ya kuwasajili wageni, baada ya kufanyiwa marekebisho sheria nambari 7 ya mwaka 2005. Hatua hii Mhe. Mwenyekiti, itaweza kuondosha tatizo la raia wa kigeni kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Mhe. Mwenyekiti, mtaro wa Msingini Chake Chake umefanyiwa matengenezo makubwa kwa mashirikiano na Idara ya Mazingira, ambayo ndiyo iliyotoa fedha za kazi hiyo. Kazi hiyo kwa sasa imekamilika kwa hatua za awali. Idara ya Mazingira itaukabidhi rasmi mtaro huo kwa Baraza la Mji Chake Chake Pemba mwezi Aprili, 2013.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi yetu inaendelea na jitihada za kuwapatia hati miliki majengo ya Ikulu. Hivi sasa majengo hayo yameshapimwa na Idara ya Upimaji. Aidha, jengo la Ikulu ya Mnazi Mmoja tayari limeshapatiwa hati miliki na Msajili wa Ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, mkakati maalum umewekwa wa kuzifanyia matengenezo makubwa nyumba zote za Ikulu pamoja na nyumba za serikali. Bodi ya zabuni tayari imeshatoa maamuzi ya kuanza kwa ujenzi wa baadhi ya nyumba ikiwemo Ikulu ya Mkoani. Ikulu ya Wete itafanyiwa matengenezo na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, barabara iendayo katika jengo la Ikulu ya Chake Chake, imeshafanyiwa matengenezo katika hatua ya kiwango cha lami.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi yangu iliwasilisha maombi Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ya kupatiwa eneo katika kiwanja cha ndege cha Pemba, ili kujenga kituo cha Zimamoto. Kiwanja hicho tayari kimeshapatikana na mazungumzo yanaendelea ili ujenzi huo uanze mara moja.

Aidha, jitihada zinaendelea kwa kujenga vituo vya Zimamoto katika kila Wilaya. Kwa sasa tayari jumla ya vituo vitatu vimeanzishwa na kuanza kutoa huduma ya Zimamoto na Uokozi. Vituo hivyo ni Mwanakwerekwe Wilaya ya Magharibi Unguja, eneo la Bandari ya Malindi Unguja na eneo la Bandari ya Mkoani kwa Pemba. Kituo cha Bandari ya Mkoani kwa sasa kitakuwa kituo cha huduma ya Zimamoto na Uokozi katika Wilaya ya Mkoani na maeneo ya jirani. Hatua za ujenzi wa kituo cha Marumbi Wilaya ya Kati zimeshaanza.

Vile vile hatua zimechukuliwa za kupatikana eneo katika Wilaya ya Micheweni Mkoa wa Kaskazini Pemba. Pia eneo la jirani na kiwanja cha Mnazi Mmoja pale Wete.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi yetu inaendelea na utekekelezaji wa mageuzi ya Serikali za Mitaa. Miongoni mwa mambo yaliyopewa kipaumbele katika mageuzi ya Serikali za Mitaa ni kuwa na watumishi wa kutosha na wenye ujuzi. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya watumishi 26 wataajiriwa wenye fani za sheria, mipango, utumishi, manunuzi, wahandisi wa majengo na wakusanyaji mapato. Aidha, ofisi yetu itawasilisha mswada wa sheria wa serikali za mitaa hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, nyumba wanazoishi Wakuu wa Wilaya za Wete na Micheweni ambazo zilikuwa katika hali mbaya, kwa sasa zimeezekwa na zitafanyiwa matengenezo madogo madogo ya ndani katika bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza sheria nambari 9 ya mwaka 2005, ofisi yetu imeshaanzisha bodi za zabuni na vitengo vya PMU katika kila idara au katika idara zake zote. Kamati ya ukaguzi wa ndani inafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria. Sambamba na hilo, daftari la kuhifadhia mali za kudumu za serikali limeanzishwa na tayari mali zote zimeshaorodheshwa kwa mujibu wa muongozo ambao umetolewa na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi yetu itaendelea kupokea ushauri na maelekezo kutoka katika Kamati zako za kudumu na Wajumbe wa Baraza lako tukufu. Hatua hii itaiwezesha ofisi yangu kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kusaidia kutatua changamoto zinazotukabili. Ni matarajio yangu kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu wataendelea kushirikiana na sisi katika jukumu letu la kuwahudumia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, hili halimo lakini nimeona niliongeze suala la agizo kubwa la utekelezaji wa maagizo ya Kamati Teule kuhusu Baraza la Manispaa. Mhe. Mwenyekiti, lile tayari serikali imeunda jopo la wanasheria kupitia maagizo yote na taratibu za kisheria za kufuata. Kazi hiyo sio ndogo inaendelea na taratibu zetu tukimaliza kamati ile tutaipeleka serikalini BLM, baada ya kukamilika BLM halafu itawasilishwa hapa rasmi. Suala hili nimeona bora nilitamke kabisa, isije kuonekana kama tumelisahau, hatukulisahau.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kiambatanisho chengine kinaonesha utekekezaji wa ahadi zilizotolewa Barazani katika mkutano wa bajeti wa mwaka 2012/2013 na yale mengine ya Kamati, yote kuanzia nambari moja mpaka nambari 41. Kwa kuokoa muda wako Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wanaweza kuyapitia moja baada ya jengine kama inavyooneshwa katika kiambatanisho hicho.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa wazima wenye afya njema na kuweza kuhudhuria katika kikao hiki.

Aidha, naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maelezo ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais juu ya Utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, inayoongozwa na Mhe. Hamza Hassan Juma Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, kwa miongozo na maagizo wanayotupa ambayo kwa hakika yamekuwa dira ya kufikia malengo ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi kwa kutoa ushirikiano wao wa dhati kwangu mimi binafsi, pamoja na watendaji wa ofisi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo. Sasa naomba nitoe maelezo ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa kwa mwaka 2011/2012 na Kamati yetu ya kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati iliagiza ofisi yetu kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kuhakikisha kwamba mifuko ya plastiki haitumiki.

Utekelezaji

Mhe. Mwenyekiti, ofisi yetu inashirikiana na Jeshi la Polisi katika kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki hapa visiwani. Katika mashirikiano hayo kikosi maalum ambacho ni kikosi kazi cha kufanya operesheni ya mifuko ya plastiki cha watu 10, wakiwemo Jeshi la Polisi kimeundwa kwa upande wa Unguja na kinasimamiwa na Mkuu wa Operesheni wa Jeshi la Polisi Zanzibar.

Aidha, kikosi kazi cha watu 9 kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, ambacho kinasimamiwa na Mkuu wa Operesheni wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba na kikosi kazi cha watu 8 kwa upande wa Mkoa wa Kusini Pemba kinachosimamiwa na Mkuu wa Operesheni wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kusini vikosi hivi vimeundwa. Vikosi vyote hivyo vina jumla ya askari polisi 12 ambapo kila kikosi kazi kina askari polisi 4. Vikosi kazi vyote hivyo vinafanya operesheni za mara kwa mara za mifuko ya plastiki na vimewezesha kwa kiwango kikubwa kupatikana kwa mafanikio yaliopo hivi sasa ya kupungua kwa matumizi ya mifuko hiyo.

Vile vile Kamati iliiagiza ofisi yetu kumpatia kila Mjumbe wa Kamati nakala yake ya kanuni ya kudhibiti matumizi ya msumeno wa moto na kanuni ya kudhibiti matumizi ya mifuko wa plastiki, mara tu itakapokuwa tayari.
Mhe. Mwenyekiti, kila Mjumbe wa Kamati amepatiwa nakala moja ya kanuni ya kudhibiti matumizi ya msumeno wa moto na nakala moja ya kanuni ya kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki.

Mhe. Mwenyekiti, agizo jengine lilikuwa ni ahadi ya kufanya tathmini ya kimazingira kwa miradi inayolazimika kisheria kufanyiwa tathmini hiyo. Mashirikiano kati ya Idara ya Mazingira na ZIPA pamoja na Kamisheni ya Utalii yameimarishwa zaidi. Sharti la kufanya tathmini ya kimazingira kwa miradi inayohusika, huingizwa kwenye masharti yanayokuwemo kwenye vyeti vya muda, wanavyopewa wawekezaji.

Jumla ya miradi 65 imekaguliwa na ushauri wa uhifadhi wa mazingira kwa miradi hiyo umetolewa ambao unahusiana na usimamizi wa taka, maji machafu na mmong'onyoko wa fukwe.

Pia miradi 15 ya uwekezaji imefanyiwa tathmini ya athari za kimazingira na kutolewa vyeti vya kimazingira. Kanuni ya tathmini za kimazingira inafanyiwa marekebisho ili kurahisisha utekelezaji wa tathmini za athari za kimazingira hapa Zanzibar.

Kufanya Marekebisho ya Sheria ya Mazingira

Mhe. Mwenyekiti, vikao vya marekebisho ya sheria hiyo vilivyohusisha wataalamu wa mazingira, Ofisi ya Tume ya Marekebisho ya Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka tayari zimefanyika. Maeneo yanayostahiki kufanyiwa marekebisho yameorodheshwa na rasimu ya kwanza mpya inayozingatia marekebisho yaliyopendekezwa katika vikao hivyo inatayarishwa. Mchakato wa kuwasilisha rasimu hiyo kwa wadau wote muhimu utafanyika, ili kupata maoni ya wadau juu ya marekebisho ya sheria hiyo.

Pia Kamati imeagiza kufukiwa kwa shimo la Bumbwini lililochimbwa kifusi na Kampuni ya MECCO kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Bumbwini kwa kufuata taratibu za kimazingira.

Mhe. Mwenyekiti, wanaopaswa kufukia shimo hilo ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kupitia Kampuni ya MECCO ambayo ilihusika katika ujenzi wa barabara ya Bumbwini. Wizara hiyo inaendelea na mazungumzo na MECCO kuhusu baadhi ya masuala ya mkataba ili kukabiliana na kuendeleza upandaji wa miti kwenye eneo kabla ya mwezi wa Juni, 2013.

Aidha, hivi sasa wakulima wamepata fursa ya kupanda mazao ya muhogo pembezoni mwa shimo hilo ambao umeanza kunawiri vizuri. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imetayarisha kanuni ya kusimamia maliasili zisizorejesheka, ambayo itaongeza ufanisi katika udhibiti wa uvunwaji wa maliasili hizo, pamoja na uendelezaji wa maeneo yaliyochimbwa. Kanuni hii imechapishwa hivi karibuni.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iliahidi kufuatilia uharibifu huo na kuchukua hatua za kisheria, ikiwemo kulipwa asilimia 10 itokanayo na uharibifu huo. Ofisi yetu imelifuatilia suala hili na kuona kuwa kuna haja ya kubadilisha kanuni inayohusika. Hivyo, ofisi imo katika hatua za kutayarisha kanuni ambayo itakuwa ni rahisi kutekelezwa sambamba na kanuni mpya ya maliasili zisizorejesheka.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mazingira huchukua hatua za kisheria juu ya mkahawa uliojengwa ndani ya fukwe katika hoteli ya Zanzibar Beach Resort. Kisheria ujenzi unaofanywa ndani ya eneo la mita 30 kutoka alama inayofikiwa na maji wakati yanapojaa, unasimamiwa kwa mujibu wa kanuni ya kudhibiti ardhi kwa wawekezaji ya mwaka 2006, ambayo msimamizi wake mkuu ni Idara ya Mipango Miji na Vijiji. Hivyo, idara ya mazingira ilimuandikia muwekezaji kufuata kanuni hiyo na pia ililiwasilisha suala hilo kwa Idara ya Mipango Miji na Vijiji kwa ajili ya kuchukua hatua za kisheria zinazohusika. Baada ya Idara ya Mipango Miji na Vijiji kupata barua ya Idara ya Mazingira, ililifuatilia suala hilo na kutoa muongozo wa ujenzi wa mkahawa huo.

Vile vile Kamati ilimuagiza Sheha wa Shehia ya Mzuwaridini kuhakikisha njia ya kuelekea pwani inafunguliwa na kushughulikiwa suala la ukaaji wa wageni katika nyumba za wageni inaomilikiwa na ndugu Khatib Jecha. Idara ya Mazingira imelipeleka suala hilo kwa taasisi husika, ambazo ni Idara ya Mipango Miji na Vijiji, Idara ya Ardhi na Usajili, Halmashauri ya Wilaya ya Kusini na Sheha wa Mzuwaridini kwa hatua.

Agizo jengine lilikuwa ni kudai hoteli ya Muyuni iliyoko Makangale Pemba fidia ya kuanza mradi bila ya kufanya tathmini za athari za kimazingira kwa kusababisha uharibifu wa mazingira. Mhe. Mwenyekiti, sheria na kanuni ziliopo hivi sasa, hazitoi fursa kwa Idara ya Mazingira kudai fidia au malipo ya uharibifu na uchafuzi wa mazingira uliofanywa.

Mhe. Mwenyekiti, marekebisho ya sheria ya mazingira yanayofanywa hivi sasa, yatazingatia dhana ya kwamba anayechafua au kuharibu mazingira alipe uharibifu wa uchafuzi wa mazingira aliofanya.

Agizo la mwisho Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Idara ya Mazingira iliagizwa kuwapatia elimu na mizinga ya ufugaji nyuki ya kisasa kikundi cha JIPE, kiliopo Mwambe Kengeja. Mhe. Mwenyekiti, ofisi yetu ikiongozwa na Waziri mwenyewe pamoja na Mwakilishi wa Jimbo la Kengeja, walishiriki katika kujumuika na kikundi hicho. Vikundi vyengine vya mazingira vya eneo hilo pamoja na wananchi kupanda miti ya mikoko ipatayo 3,000 kwa ajili ya kuimarisha mazingira. Baadae nasaha za elimu ya mazingira zilitolewa kwa washiriki walioshiriki katika shughuli hiyo. Ofisi yetu pia imetoa msaada wa seti moja ya nguo za kisasa za kuvunia asali ili kupunguza uharibifu wa misitu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nikasimama mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kutoa maoni ya aina mbili.

Kwanza kutoa muhtasari wa utekelezaji wa maoni na maagizo ya Kamati katika Wizara zetu tatu. Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Lakini baadae nitakuomba uniruhusu kutoa muhtasari wa ripoti ya utekelezaji wa Kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia naanza kwa uwasilishaji wa maagizo ya Kamati ambayo ilitolewa na Mawaziri watatu. Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, nataka nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lakini vile vile pamoja na Mhe. Waziri wake, pamoja na watendaji wote wa Wizara yake ambao wametupa mashirikiano makubwa katika kipindi chote cha mwaka 2012, na mpaka hivi sasa Mhe. Mwenyekiti nakuthibitishia kwamba Kamati yangu inaendelea vizuri kwa mashirikiano makubwa.

Kwa hivyo, kwa niaba ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa tunashukuru na tunapongeza sana kwamba yale ambayo tuliyoyaagiza yatekelezwe na Wizara kama Mhe. Waziri alivyoeleza mwenyewe yote wameyatekeleza na kama ripoti inavyosema.

Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa hii nataka kusema kwamba Taarifa hii ya Utekelezaji wa Ofisi za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Kamati yangu imeipokea na wala haina matatizo nayo. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mwenyezi Mungu na hizi nyengine zitakazokuja pia tuendelee kushirikiana katika kuwatumikia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nakuja katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kwanza nimpe pole sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa majukumu makubwa ambayo ni mazito tuliyompa ya ulezi hasa katika vitengo ambavyo vimekabidhiwa wizara yake, kwa sababu vitengo alivyokabidhiwa ni vyenye matatizo mengi, vinahitaji msaada mkubwa pamoja na ukaribu wa watendaji wetu kuwasaidia.

Kwa mfano, ukiangalia mazingira hasa katika eneo la walemavu kwa kweli wizara yake inasaidia sana kuweza kutafuta haki za walemavu pamoja na kuweza kutoa miongozo na kuwaendeleza walemavu.

Vile vile kutokana na majawabu ambayo Mhe. Waziri aliyotusomea hapa, mimi nathibitisha kwamba mimi pamoja na Kamati yangu hatuna pingamizi nayo na kama walivyoeleza kwenye maelezo yao mengi ambayo tuliyoyaagiza au takriban yote wameyatekeleza.

Kwa kweli jambo moja Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tatizo la Wizara hii ni kwamba majukumu yake mengine hayako moja kwa moja ambayo yanayohusika kwenye wizara husika na majukumu mengine yanakuwa ni sekta mtambuka, ambapo ofisi kupitia idara fulani inakuwa inashughulikia eneo fulani, lakini utekelazaji wake unahusisha na wizara nyengine.

Sasa jambo ambalo ninaloliomba Mhe. Mwenyekiti kuna eneo moja hili ambalo tulitembelea Bwejuu katika Shehia ya Mzuwaridini. Mhe. Mwenyekiti, suala hili limekuwa ni tete sana lakini pia suala hili linashughulikiwa na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kusini.

Mhe. Mwenyekiti, matatizo haya yamekuwa kama ni donda ndugu, hivi sasa kuna tatizo kwamba wawekezaji wetu ikiwa wazalendo au hata wa kigeni wakishakabidhiwa maeneo ya ukanda wa pwani, basi wanaanza kuwanyanyasa wananchi, kuwazuia na kujenga makuta makubwa pamoja na mageti, ili wananchi wasiweze kutumia fukwe za bahari yetu kwa ajili ya shughuli zao za kiuchumi.

Suala hili kwa bahati nzuri pia lipo kwenye Ripoti ya Kamati Teule ya kuhusu masuala ya Ardhi. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe walioteuliwa katika Kamati ile inayoshughulikia masuala ya ardhi na eneo hili lilikuwa kama ni mgogoro, basi naomba sana Kamati ile waweze kulifuatilia, ili watakapoleta ile ripoti basi na utekelezaji wa kufunguliwa ile njia ya kuelekea baharini iwe limeshatekelezwa.

Lakini pamoja na hayo Mhe. Waziri nakushukuru sana watendaji wako, isipokuwa bado naomba waendelee kujitahidi hasa kurekebisha hizi sheria za mazingira, ili waweze kufanya kazi kwa vizuri zaidi pamoja na Idara ya Mazingira iweze kuwa na nguvu ya kuweza kutoa adhabu kwa mtu yeyote ambaye waliyempa notisi, ambaye ikiwa baadaye hakuweza kuheshimu notisi zile.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo linajitokeza kwamba notisi zinatolewa, ili pale panapoonekana uharibifu wa mazingira umejitokeza, lakini matokeo yake Mhe. Mwenyekiti na kwa kuwa idara inakuwa haina nguvu ya kuweza kumchukulia hatua yoyote isipokuwa ni kutoa notisi tu. Kwa hiyo, wananchi au wawekezaji wale huwa wanaendelea kuharibu mazingira.

Pamoja na yote Mhe. Mwenyekiti nakuthibitishia kwamba Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake Kamati yangu wametupa mashirikiano mazuri na namuomba Mwenyezi Mungu na hii ripoti ya mwaka huu waweze kuitekeleza kama ilivyo ripoti ya mwaka uliopita, naamini Kamati yetu itatoa mashirikiano zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maelezo haya kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili hatuna pingamizi nayo tunaipokea. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namalizia Ripoti ya Maagizo ya Kamati ambayo tuliyatoa kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa kweli nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kama nilivyoelezea kwenye maagizo ya ripoti nyengine na wao wamejitahidi sana kama tunavyojua wizara hii ni kubwa tunaweza kusema ni *Giant Ministry* katika Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.
Lakini pamoja hayo, wameweza kujitahidi kufuatilia yale maagizo yetu na kimsingi tunawashukuru na watendaji wake, kwa sababu mengi ambayo tumeyaeleza katika Ripoti ya mwaka 2012/2013 wameweza kuyatekeleza.

Vile vile nimpongeze zaidi Mhe. Waziri baada ya kuliingiza na ile Ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Manispaa. Kwa kweli tumeanza kuona mabadiliko au marekebisho yameanza kufanywa. Lakini bado tunamuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba ajitahidi kuhakikisha anakamilisha ile *reform* ya Baraza la Manispaa, kwani Mhe. Mwenyekiti Baraza la Manispaa likiyumba kidogo tu, basi mji wetu utaharibika.

Sasa kitu ambacho ninachokiomba ni kwamba aweze kukamilisha maelekezo yale ya Ripoti ya Kamati Teule na kwa kuwa maelekezo yale hata wao wenyewe walikiri.

UTARATIBU

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, huu tunaouanzisha leo ni utaratibu mpya kwetu, tumesikia maelezo ya Mawaziri juu ya utekelezaji. Kwa vyovyote vile nadhani ilikuwa ni busara Waheshimiwa Wajumbe tupewe nafasi angalau tuweze kuchangia kati ya yale ambayo yameelezwa na Mhe. Waziri.

Sasa Mhe. Mwenyekiti hivi sasa akifanya anaonekana anafanya majumuisho juu ya yale ambayo yameelezwa na Waheshimiwa Mawaziri. Kwa hivyo, sisi nafasi yetu kama Wajumbe wakati yeye hivi sasa anakwenda kufunga mjadala huu, sisi tunakuwa na nafasi gani kuweza kujadili yale ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Mawaziri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante sana ambapo umetoa *concern* yako hapa. Lakini inaonekana kwamba wakati tulipokuwa kwenye Kikao chetu cha *Briefing* huenda ulikuwa hupo au hukuelewa tulichokubaliana. Mhe. Mjumbe kwa faida ya wote tulikubaliana katika Kikao cha *briefing* kwamba watakuja hapa Mawaziri kwa ajili ya kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa mwaka 2011/2012 na wote watakapomaliza Mwenyekiti atatoa Taarifa ya Maagizo ya mwaka 2012/2013.

Halafu Waheshimiwa Wajumbe sasa watapata fursa ya kuchangia katika Wizara zile zote zinazohusika na kamati husika zinazosimamiwa na Kamati husika. Kwa hivyo, baada ya hapo mawaziri watapata fursa ya kuja kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo ambayo yanahitaji ufafanuzi na baadaye tutaacha ile ripoti ya Mwenyeki, ili ikafanyiwe kazi na iweze kuja kuwasilishwa baadaye na huo ndio muongozo ambao tuliokuwa tumekubaliana kwenye kikao cha *briefing*.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nadhani tulivyokubaliana ndivyo ulivyoeleza. Lakini tulikubaliana kwamba Mawaziri waeleze utekelezaji wa ripoti iliyopita na Mhe. Mwenyekiti aeleze ripoti yake mpya na baadaye tuingie kwenye mjadala na mwisho ndio tutakuja kwenye suala hilo. Kwa hivyo, hivi sasa yeye anaonekana anafunga mjadala huu, kitu ambacho sicho tulichokubaliana hicho. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, na mimi napenda kutoa maelezo mafupi kuhusu yale tuliyokubaliana kwa mujibu wa utaratibu huu ambao tumeamua kuanzisha kwa nia ya utekelezaji mzuri wa shughuli zetu za Baraza. Mhe. Mwenyekiti, maelezo yako yalikuwa sahihi na bado nafasi ya Waheshimiwa Wajumbe itakuwepo wachangie kuhusu utekelezaji wa mwaka uliopita na pia watakuwa na nafasi ya kuchangia kuhusu haya ambayo yameibuliwa na Kamati kwa mwaka huu 2012/2013.

Sasa anachokifanya Mhe. Mwenyekiti pale ni kuwasilisha Taarifa kwanza kwa muono wake kutokana na zile taarifa ambazo zinawasilishwa na wizara husika na baadaye atawasilisha hii taarifa ya mwaka 2013. Kwa hivyo, baada ya hapo kwa pamoja tutapata nafasi ya kuchangia, na tukimaliza kuchangia tena Mawaziri wenye hoja mbali mbali ambazo zitakazoibuliwa hapa, basi watatoa majibu na baada ya hapo Mwenyekiti ndio atakuja kufunga mjadala.

Kwa maana hiyo, Mwenyekiti hivi sasa si kama anafanya majumuisho, isipokuwa anatoa yale ambayo ameyaona yametekelezwa katika Wizara kwa mwaka uliokwisha. Vile vile atawasilisha ripoti yake kwa yale aliyoyakuta katika mwaka huu wa fedha na baada ya hapo tumekubaliana tutaanza michango ya jumla, na hivyo ndivyo ambavyo nimeelewa mimi Mhe. Mwenyekiti na ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Mwenyekiti, nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaendelea kumalizia.

Lakini Mhe. Mwenyekiti kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais huu utaratibu tumeuanzisha mwaka huu kwa kweli ni utaratibu mpya na jambo lolote unapo-*practice* lazima litaleta matatizo ya hapa na pale.

Kwa hivyo, nadhani sisi ni wajibu wetu kuangalia *modality* ipi ambayo itasaidia zaidi, kwa sababu hatupendi kuendelea kuacha viporo na ikawa kila siku tunazungumza na kurejea yale kwa yale. Kutokana na hali hiyo, ndio maana pale mwanzo nilisema kwamba nitawasilisha ripoti yangu katika maeneo mawili na eneo la mwanzo nitajibu yale maagizo ya Kamati ambayo Waheshimiwa Mawaziri wameyatekeleza katika kipindi cha mwaka 2011/2012.

Halafu baada ya hapo kwa kuwa Waheshimiwa Mawaziri ndio waliowasilisha, Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako unaweza ukawapa ruhusa Waheshimiwa Wawakilishi wakachangia kwamba agizo hili halikutekelezwa hivi na vile na halafu kama baadaye kama kutakuwa na *comments* zozote, basi Mawaziri watakuja kujibu na halafu wakishamaliza wao baadaye nitarudi tena nitakuja kusoma ripoti ya mwaka huu 2012/2013. Kwa hiyo, huu ndio muongozo nafikiri uliotoka katika Kamati ya Uongozi na ndio maana nikawa natekeleza hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hizi nilizozisoma hapa bado sijaanza kusoma ripoti mpya ya mwaka 2012/2013.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niongezee nguvu kidogo hoja iliyoanzishwa na Mhe. Omar Ali Shehe pamoja na kwamba umemruhusu tuendelee.

Lakini maelezo yake yanafanya rejea kwenye makubaliano katika Kamati ya Uongozi, yaani kwenye Kikao cha *briefing* kama ulivyofanya marejeo katika maelezo yako Mhe. Mwenyekiti. Tulizungumza kwa kina suala la kwamba kilichofanywa ndani ya Kamati ya Uongozi ilikuwa inaelekeza kutatokea kujirejea na hilo itakuwa ni kupoteza muda bure, kwamba Waziri akija anakuja kuelezea utekelezaji na halafu akija Mwenyekiti wa Kamati aanze kwanza kuzungumzia utekelezaji sasa maneno itakuwa ndio yale yale.

Sasa makubaliano ya mwisho katika Kikao cha *briefing* yalikuwa ni kwamba mawaziri ndio watakaotoa Ripoti ya Utekelezaji na Wenyeviti wa Kamati wakija wasizungumzie tena utekelezaji wa mwaka uliopita kwa sababu watakuwa wanafanya marejea na tayari kazi imeshafanywa na Waziri.

Kutokana na hali hiyo, basi Mwenyekiti azungumzie ripoti yake ya mwaka huu utendaji wake na akimaliza kuwasilisha ripoti, basi Waheshimiwa Wajumbe wajadili kama wanayo maswali watauliza.

Sasa katika majumuisho mwisho ndio wataanza Mawaziri na mwisho kabisa ndio atakuja Mwenyekiti wa Kamati ambaye ataweza kutoa maelezo na kama kujibu hoja au kutoa changamoto zake na sio tu kutokana na ripoti za mawaziri lakini ni kutokana na majadiliano ya Wajumbe pamoja na ripoti ya Kamati yake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tuweke sawa na hivyo ndivyo tulivyokubaliana kwamba Mwenyekiti akija hazungumzii tena utekelezaji, na yale yaliyozungumzwa na Waziri tusirejee kazi ile ile na kupoteza muda wa Baraza bure Mhe. Mwenyekiti, naomba tuzingatie makubaliano ya Kikao cha *briefing* Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ahsante sana. Nafikiri mwanzo nilipozungumza nilizungumza wazi na kila mtu alinifahamu kwamba alivyonukuu Mhe. Ismail Jussa Ladhu ndivyo nilivyoelekeza na ndio makubaliano yetu yalivyokuwa. Sasa baada ya kumaliza Mwenyekiti kutoa taarifa ya mwaka 2012/2013 tutaendelea na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuchangia.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana siku ya Kikao cha *briefing* nilikuwa kidogo nimedharurika sikuyasikia hayo yaliyozungumzwa na mimi nilikuwa nayo yale ambayo tuliyokubaliana kwenye Kamati ya Uongozi. Mhe. Mwenyekiti, kama ni hivyo na ndio maana nikasema kwamba jambo lolote mnalolianza lazima linakuwa linaleta changamoto.

Kwa hivyo, baada ya hayo yaliyojitokeza sasa naomba uniruhusu nitoe Muhtasari wa Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi za Kamati za Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2012/2013.

Mhe Spika, Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha 106 cha Kanuni za Baraza, Toleo la mwaka 2012. Kwa mujibu wa Kanuni ya 114 ya Kanuni za Baraza, kamati hii imepangiwa majukumu mbali mbali na miongoni mwa majukumu hayo ni haya yafuatayo:-

- Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.
- Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika.
- Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya serikali na kama matumizi hayo yalizingatia thamani halisi ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imepewa majukumu ya Kuzisimamia Ofisi zifuatazo:-

- Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
- Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.
- Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka naomba niwataje Wajumbe wa Kamati yangu kama hivi ifuatavyo:-

- Mhe. Hamza Hassan Juma - Mwenyekiti
- Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi - Makamo Mwenyekiti
- Mhe. Ali Salum Haji - Mjumbe
- Mhe. Mgeni Hassan Juma - Mjumbe
- Mhe. Mohammed Haji Khalid - Mjumbe
- Mhe Salma Mohammed Ali - Mjumbe
- Mhe Ussi Jecha Simai - Mjumbe
- Nd, Ramadhan Khamis Masoud - Katibu,
- Nd. Rahma Kombo Mgeni - Katibu.

Mhe Mwenyekiti, Kamati ilifuatilia Utekelezaji wa Bajeti, Miradi, Sera na Ukusanyaji wa Mapato katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na kubaini changamoto zifuatazo:-

- Uhaba wa wataalamu wa fani muhimu katika Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, Idara ya Sera, Mipango na Utafiti, Idara ya Mpiga Chapa Mkuuu wa Serikali na Idara nyenginezo.

- Uhaba wa usafiri na uchakavu wa magari kwa upande wa Unguja, Pemba na Dar es salaam.

- Uchakavu wa Mitambo ya Mpiga chapa Mkuu wa Serikali pamoja na Taasisi za Serikali kutolipa gharama za huduma wanazopatiwa na Kiwanda.

Maoni ya Kamati:

- Kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Pili inasubiri mchakato wa uajiri wa wataalamu kutoka serikalini, ni vyema mchakato huo ukaharakishwa, ili Idara za Ofisi hii zikapatiwa wataalamu hao ili kuleta ufanisi wa utendaji.

- Kuna umuhimu kwa Ofisi ya Makamu wa Pili kupatiwa usafiri wa kutosha katika Ofisi zake hususan zile zilizopo Pemba na Dar es salaam. Magari yaliyochakaa kupita kiasi ni busara yakapigwa mnada lakini baada ya kupatikana mapya.

- Kamati yangu inaishauri Wizara kwa kuwa ofisi hii ndio kioo cha kuonesha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, basi ni vyema kukiboresha Kitengo chake cha Habari, ili kuweza kuonesha na kuuelezea umma malengo yake ya muda mfupi na mrefu; na ni kitu gani serikali yetu inafanya kipi kimefanyika, kinachofanyika na kinachotarajiwa kufanyika.

Mhe. Mwenyekiti, sio hivyo tu, bali pia kuelezea umma ni mafanikio gani wananchi wanayapata kupitia miradi mbali mbali inayofanywa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Halikadhalika na ni changamoto gani zinazowakabili na kwa namna gani serikali inazishughulikia. Kwa hivi sasa kitengo hiki inaonesha hakifanyi kazi yake ipasavyo, kwa hiyo tunaomba alau Ofisi ya Makamu wa Pili inunue *camera*, ili kufuatilia na kuonesha matukio mbali mbali ya kitaifa, na miradi mbali mbali ya serikali,

Kamati inaitaka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuchukua taarifa na picha za miradi yote ya Wizara zote za SMZ na kuandaa Ripoti ya Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, ambayo itakayopelekwa kusomwa kwenye mkutano mkuu wa chama kinachotawala, ili iwe na mvuto kama inavyofanyika kwa wenzetu Tanzania Bara, ambapo taarifa yao karibu mara mbili inakuwa inavutia lakini ya kwetu inakosa mvuto wakati kuna mambo mengi yanafanyika lakini tunashindwa kuyaelezea ipasavyo.

Kwa hiyo, iko haja ya kuwapatia mafunzo Maafisa wa Habari, ili waweze kuwa na ubunifu wa kutayarisha ripoti zenye mantiki na mvuto unaostahili. Pia taarifa hizo ziingizwe kwenye (*web-site*) ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ili na dunia ishuhudie kinachofanyika kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Maafisa wa Habari hawa pia washirikishwe kwenye vikao vyote vya Wizara na pia kwenye safari za Makamu wa Rais, Waziri pamoja na Katibu Mkuu, ili kuwapa uelewa wa mambo yote ya Wizara na waweze kuripoti vizuri ipasavyo.

Kamati inaishauri wizara kuandaa (*job description*) kwa watumishi wake, kwani hivi sasa kuna baadhi ya wafanyakazi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wanafanya kazi zisizowahusu, kazi ambazo zingelipaswa kufanywa na watumishi wengine. Lakini kuna baadhi ya wafanyakazi wa Ofisi hii wanakuja kazini kila siku hadi saa tisa na nusu lakini hakuna kazi yeyote wanayopangiwa au wanayoifanya.

Hali hii ni kupoteza fedha za umma bure, kwani inavyotakiwa kila aliyeajiriwa katika sehemu ni lazima aifanye kazi aliyopangiwa. Kamati yangu inaishauri Wizara kuwapa motisha kwa kushiriki katika semina za mafunzo mbali mbali za nje na ndani watumishi wake, ili kuwajengea uwezo na kujiamini katika majukumu yao.

IDARA YA UPIGAJI CHAPA:

Kamati yangu inashauri Wizara kuharakisha Ununuzi wa Mitambo mipya, kwa ajili ya Kiwanda cha Uchapaji ili kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi. Lakini kuna umuhimu kwa Taasisi za Serikali kulipa madeni inayodaiwa na Kiwanda, ili kukiwezesha Kiwanda hicho kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuiongezea mapato ili kuweza kujitegemea.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaishauri serikali kuibadilisha Idara hii kuwa Shirika, ili kuweza kuwa na mipango mahsusi ya kazi na kujitegemea. Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu ilitembelea kiwanda cha uchapaji na kuzungumza na wafanyakazi wote pamoja na uongozi wa Idara ikiongozwa na Mkurugenzi, kamati yangu iligundua kuwa kulikuwa hakuna mashirikiano kati ya wafanyakazi na uongozi wa Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, hasa katika kushughulikia maslahi yao ikiwemo malimbikizo ya posho mbali mbali ambazo wafanyakazi hao walistahiki.

Lakini tunashukuru kuwa Mkurugenzi aliahidi kuwa atalimaliza si muda mrefu ujao. Kwa hiyo, tunamuomba Mhe. Waziri suala hili alisimamie, ili kuondoa manung'uniko ya wafanyakazi wetu. Pamoja na hayo tunapongeza jitihada zinazoendelea za kukihamisha kiwanda hicho na kukihamishia katika eneo la Maruhubi.

Mhe. Mwenyekiti, pia kamati yangu inaitaka serikali kutoa ruhusa ya kuajiri wataalamu wapya, kwani hivi sasa fundi mmoja anafanya kazi za aina zaidi ya tatu ambazo sio fani aliyosomea. Kwa hiyo, iko haja ya kuajiri wataalamu wengine, ili kuongeza ufanisi na utakaoweza kumudu kuendesha mitambo mipya na vile vile kuwapatia mafunzo ya ziada wale wataalamu waliopo, ili kuweza kuitumia mitambo hiyo mipya itakayokuja.

Vile vile Kamati yangu inasisitiza kuangaliwa upya posho za wafanyakazi hao hasa kutokana na mazingira ya eneo wanalolifanyia kazi na kemikali wanazotumia hapo kiwandani. Mhe. Mwenyekiti, kamati inaitaka Idara ya Upigaji Chapa kuwawekea utaratibu wa wafanyakazi kupimwa afya zao kila baada ya muda hasa kutokana na mazingira magumu ya kazi zao.

IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaishauri serikali kwa kuwa nchi yetu inategemea kuadhimisha na kusheherekea miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar ifikapo Januari 12 mwakani 2014. Kuna umuhimu mkubwa sherehe hizo zikaadhimishwa kwa ubora wa hali ya juu na wa kipekee hasa kutokana na kuyaenzi Mapinduzi yetu matukufu ya mwaka 1964, yaliyokuwa na lengo la kumkomboa mnyonge na kuleta maendeleo ya kasi na haraka hasa katika ulimwengu huu wa karne ya 21 ya Sayansi na Teknolojia.

Kamati yangu inaishauri serikali kupitia idara hii kuanza maandalizi hayo mapema na kuandaa halaiki ya aina yake na kuwaalika viongozi wakubwa Duniani akiwemo rafiki yetu kipenzi Rais wa China, ambapo nchi yake ndiyo iliyokuwa ya mwanzo kuyatambua Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaitaka Kamati hiyo ya Maadhimisho ya Sherehe za Kitaifa kuingiza kwenye ratiba ya sherehe hizo mechi ya mpira wa miguu na *net-ball* kati ya timu kabambe ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Wabunge wa Uganda mechi ambayo itakuwa kali na ya kusisimua ambayo itakumbusha enzi ya mashindano ya Gosej, ambapo Timu ya Taifa ya Zanzibar ilipokuwa na ushindani mkubwa na Timu ya Taifa ya Uganda.

Pia Kamati yangu inaikumbusha idara hii majukumu yake hasa ujenzi wa nyumba ya kumbukumbu ya viongozi waasisi wa Taifa letu, ili kuweka kielelezo cha mashujaa wetu wa taifa letu, kwani hakuna taifa lisilokua na historia, lakini inashangaza sana sasa ni nusu karne hatuna nyumba ya kumbukumbu ya kuwaenzi viongozi wetu waasisi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaishauri serikali kuweka kielelezo chochote aidha kujenga mnara hapo katika eneo la Michenzani au kitu kingine alau iwe kumbukumbu ya Mapinduzi yetu matukufu ya mwaka 1964, kwani vizazi vya sasa vinaweza kupoteza kumbukumbu ya kujua walikotoka na wapi waelekee. *(Makofi)*

IDARA YA MAAFA:

Suala la malipo ya fidia kwa wale waliofiwa na jamaa zao katika ajali ya *MV. Spice Islander* linahitaji kuchukuliwa jitihada ya kukamilishwa, kwani limekwishachukua muda mrefu tangu ajali hiyo ilipotokea. Pia Kamati yangu inashauri idara hii kuwa karibu na Halmashauri pamoja na Mabaraza ya miji, ili kutoa ushauri wa kitaalamu hasa katika kipindi hiki cha mvua za masika, ili kuepusha mafuriko na maambukizo ya maradhi ya matumbo na kipindupindu.

Vile vile Kamati yangu inaishauri wizara kuharakisha ujenzi wa jengo la idara hii, kuwa na ghala la kuwekea vifaa vyao vya kukabiliana na majanga mbali mbali yanapotokea. Kwa hivi sasa kutokana na mabadiliko ya tabia nchi lolote linaweza kutokezea Idara hii wasije wakahangaika.

TUME YA UCHAGUZI:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu imekutana na Tume ya Uchaguzi Zanzibar, na kupokea ripoti ya malengo yao waliyojiwekea. Kamati yangu imepongeza kwa kuwapatia nafasi za masomo watendaji wa Tume ya Uchaguzi, lakini bado tume hiyo haijafanya kazi ya kutoa elimu ya uraia kwa wananchi wetu kuhusu maandalizi ya Kura ya Maoni kuhusu Katiba mpya.

Lakini pia haijafanya maboresho ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura jambo ambalo ni muhimu hasa katika kuweka sawa majina ya wahusika, lakini pia kuingiza wapiga kura wapya waliotimia umri na kuwatoa wale waliopoteza sifa za kuwa wapiga kura, hii itaondoa s*intafaham* wakati utakapofika uchaguzi au Kura ya Maoni. Kwa hivyo, daftari ndilo litakaloweza kutoa haki kwa kila mwenye haki ya kupiga kura.

Mhe Mwenyekiti, kamati yangu inaitaka serikali kuitangaza Tume mpya ya uchaguzi ili kuweza kupanga ratiba ya kuanza kuliboresha Daftari la kudumu kwani muda mkubwa umeshapita tangu Tume iliyokuwepo kumaliza muda wake. Na hivi sasa shughuli nyingi za tume ziko nyuma ya ratiba jambo ambalo linaweza kuja kuleta vurugu wakati wa kura ya maoni ya Katiba mpya.

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI

Mhe Mwenyekiti, kamati yangu inaishauri serikali kuhakikisha utekelezaji wa taarifa za Kamati za Kudumu, na Kamati Teule za Baraza zifanyiwe kazi ili kupunguza kero katika jamii na kupelekea wananchi kuwa na imani na serikali yao kwani maelezo tunayoyatoa hapa Barazani mengi huwa tunatumwa na wananchi wetu waliotuchaguwa na utekelezwaji wa maagizo hayo ndio kuwatumikia wao.

Kwani kunaubadhirifu mwingi uliogundulika na kamati lakini hatuoni hatua za haraka kuchukuliwa, hii itapelekea wale wakosaji kujihisi wako sawa na wengine kuweza kufanya kama hivyo kwani watahisi kufanya ubadhirifu ni jambo la kawaida tu. Kamati yangu hata malengo ya serikali itakuwa ni ndoto tu ikiwa tutaendelea kuoneana mihali huku wachache kuitafuna nchi sisi tunaamini ikiwa serikali yetu itakuwa makini basi bado tunauwezo mkubwa wa kujitegemea kwa bajet ya matumizi ya kawaida kupitia mapato yetu ya ndani bila kutegemea wafadhili wa nje. Lakini kwa hali hii ya kufumbiana macho sio rahisi kufikia lengo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kuna malalamiko na migogoro mingi ya ardhi, kuna umuhimu mkubwa kwa waratibu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuifuatilia kwa karibu na kumshauri ipasavyo Makamu wa Pili wa Rais na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa lengo la kulitafutia ufumbuzi kwani miongoni mwa kadhia kubwa iliyopo hapa Zanzibar ni unyang'anywaji wa Ardhi, unyanyaswaji wananchi na wawekezaji hasa walioekeza katika maeneo ya pwani suala hilo hasa katika kuwazuia wananchi kuzitumia fukwe na kuwafungia njia za kuelekea pwani kwenye shughulizao za kila siku za kutafuta rizki..

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo kamati yangu inamuomba Makamo wa pili wa Rais akiwa yeye ndie kiongozi wa shughuli za siku zote za serikali awe mkali na kuchukua maamuzi magumu ili kulikomesha suala hili kwani wale wavamizi wamekuwa na kibri kwa kuona serikali haiwezi kuchukua hatua dhidi yao jambo ambalo wananchi hawaridhiki nalo. Tumeshuhudia mabarua mengi ya malalamiko ya wananchi wanayopeleka serikalini lakini yanayopatiwa ufumbuzi ni machache sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa migogoro mingi ya ardhi hupelekwa Mahkama ya ardhi Ili kutekeleza vyema suala zima la Utawala Bora na kuzifanya Taasisi tatu za Nchi kwa maana ya Mahkama, Chombo cha Kutunga Sheria na serikali kutekeleza kazi zao bila ya kuingiliana, ni vyema Mahkama ya Ardhi ikawekwa chini ya Mahkama Kuu badala ya utaratibu wa sasa, Mahkama hiyo kuwa chini ya wizara inayoshughulikia utoji na uhaulishaji wa ardhi na kwa kuwa wote wanawajibika kwa Waziri wa ardhi basi kuna shaka kubwa inayowapata wananchi hasa kwa kuona kesi nyingi huwa zinachukua muda mrefu kutolewa maamuzi na wakati mwengine watendaji wa wizara ndio wanaosababisha migogoro hiyo ndio maana kumekuwa na mlundikano mkubwa wa kesi ambazo hazifikii maamuzi kwani kuna baadhi ya kesi huchukua zaidi ya miaka saba bila ya kupatiwa ufumbuzi, kwa hiyo nadhani kwa yale ambayo hayajafika Mahkamani basi ofisi ya Makamo wa pili watusaidie kuyatatua ili matumaini yarudi kwa wananchi kwa serikali yao.

IDARA YA FARAGHA

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaiomba serikali kuu kuliangalia suala la ujenzi wa nyumba za Viongozi wetu wakuu wa Kitaifa kule Pemba, kwani sisi haturidhiki na jinsi wanvyoshughulikiwa wakiwepo kisiwa cha Pemba, hasa Makamo wa Kwanza na wa Pili wa Rais. Isitoshe hivyo tu bali pia hawana usafiri wa kutosha kwa kisiwa cha Pemba jambo ambalo hulazimika misafara yao kusitisha shughuli nyingi za kikazi wakati wanapokuwepo Pemba kwani magari mengi ya mawizara huazimwa kwa ajili ya kuwahudumia viongozi hao pamoja na misafara yao.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kamati yangu inaishauri serikali kujenga jingo jingine kule Dodoma ambalo litaendana na hadhi ya Makamo wa Rais, lakini pia na hapo Dar-es Salaam kujengwa jengo la nyumba ya Makamo wa Kwanza na Wa Pili hasa kutokana na muundo wa serikali yetu ulivyo hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu pia inashauri pia na hapa Zanzibar kuhamisha ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na kujengwa jengo jingine la kisasa litakalokuwa na huduma zote na eneo lenye faragha. Sio pale lilipo hivi sasa .

Kamati ilikutana na Uongozi wa Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais pamoja na Kamishna wa Polisi kuzungumzia suala la Ukamilishwaji wa Ujenzi wa Choo kwa Watumiaji wa dawa za kulevya, katika kiwanja cha Ndege cha Kisauni, Zanzibar pamoja na suala la ulinzi na usalama katika kiwanja hicho pamoja na maeneo mengine kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo Kamati yangu ilgundua tatizo la eneo la choo kilipo na mazingira yasiokuwa mazuri kiupekuaji na hasa kuzingatia baada ya hapo inabidi mtuhumiwa aondolewe hapo na kupelekwa kituo kingine cha Polisi kwa hatua zaidi.

Changamoto Zilizopo Katika Utekelezaji wa Mradi Huo

Kikao kilibaini yafuatayo katika ujenzi wa choo hicho pamoja na eneo la uwanja wa ndege na maeneo mengine ya mji kwa ujumla.

1. Katika eneo hilo hakuna sehemu iliyotayarishwa kwa ajili ya kuwafanyia uchunguzi watuhumiwa. Badala yake watuhumiwa hufanyiwa uchunguzi katika maeneo yaliyo nje na uwanja huo. Hali hii hupelekea uwezekano wa kupoteza ushahidi.

2. Kiwanja cha ndege hakina kituo cha Polisi chenye sifa angalau daraja la “C” kwa lengo la kukidhi suala la ulinzi na usalama katika eneo hilo. Serikali imelenga kuufanyia matengenezo makubwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume lakini suala la kuweka ulinzi na usalama katika kiwanja hicho limesahaulika. Polisi Zanzibar imekwishawasilisha mapendekezo yake serikalini lakini mpaka leo hii haijapata majibu.

3. Kitengo cha Madawa ya kulevya hufanya “Patrol” lakini hakina vitendea kazi. Kitengo hiki kilipoanzishwa miaka 15 iliyopita kilipatiwa na Wafadhili vitendea kazi kama vile pikipiki, gari na radio “ walk talk” ambavyo vyote kwa sasa vimekwishakufa.

4. Kitengo cha Madawa ya Kulevya pia hakina mafuta ya kutosha kwa ajili ya usafiri. Hali hii inachangia kitengo hicho kukusanya madawa katika kiwango kisichochotakiwa.

5. Idara ya Polisi ina kitengo kinachohusika na Ukamataji wa Dawa za kulevya. Hata hivyo, kitengo hiki hakina usafiri na kwa kipindi cha miaka mitatu Jeshi la Polisi halikuwa na lengo la kununua gari kwa vitengo vyake na vituo, ijapokuwa Jeshi hilo lilinunua gari katika kipindi cha Uchaguzi kwa kila Wilaya. Kwa upande mwengine Jeshi la Polisi Zanzibar lina vitendea kazi vilivyochakaa ambavyo hutumika kwa ajili ya ulinzi na usalama. Jeshi hilo tayari limeshalifikisha suala hilo katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais lakini bado hawajapatiwa majibu.

6. Katika masuala ya kesi bado kuna changamoto ya wale wanaokamatwa na dawa hizo, wengi wanaofikishwa Mahkamani huachiliwa huru.

7. Uhalifu kwa ujumla katika mji wa Zanzibar umepungua ijapokuwa katika maeneo ya Mboriborini, Chumbuni na Magogogni bado changamoto hiyo ipo.

8. Serikali hutoa maagizo kwamba Mihadhara yenye kuashiria uvunjifu wa amani isifanyike. Hata hivyo, maagizo hayo hutolewa bila ya kuwepo kwa sheria zinzoyapa nguvu maagizo hayo.

Kamati vile vile ilifanya ziara katika Nyumba za Polisi Ziwani na Mwera kujionea hali halisi ya nyumba hizo. Katika ziara hiyo, kamati ilibaini yafuatayo:-

i) Nyumba za askari Ziwani ni za miaka mingi sana, chakavu mno, zinavuja na hazina hadhi ya kuwa makaazi ya askari.

ii) Ijapokuwa Jeshi la Polisi limejenga nyumba mpya ya familia 12, nyumba hiyo inakabiliwa na ukosefu wa maji kutokana na miundo mbinu ya maji katika jengo hilo kujengwa vibaya.

iii) Nyumba kadhaa za askari kwa upande wa Mwera, Chwaka, Tunguu, Makunduchi na Pemba mapaa yao yamechakaa kiasi cha kutosha, ingawa kwa upande wa Mwera nyumba hizo zimeanza kufanyiwa ukarabati kwa kuezekwa lakini bado nyingi zimekuwa katika tatizo la kuvuja.

Maoni na Ushauri wa Kamati

1. Mhe. Mwenyekiti, kuna haja kwa serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mamalaka ya Uwanja wa Ndege wa Zanzibar kutayarisha eneo ndani ya kiwanja hicho kuweka eneo la kuwafanyia uchunguzi watuhumiwa wa dawa za kulevya wanaoingia na wanaotoka nchini. Hatua hii itasaidia kuepusha suala la kupoteza ushahidi wa uchunguzi wa dawa hizo

2. Mhe. Mwenyekiti, ni vyema kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanziabar kupitia Mamalaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kuweka Kituo cha Polisi chanye sifa cha angalau daraja la "C" ili kiweze kukidhi suala la ulinzi na usalama katika eneo hilo.

3. Mhe. Mwenyekiti, kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutenga Bajeti ya kutosha kwa ajili ya kukipatia vitendea kazi pamoja na mafuta Kitengo cha Madawa ya Kulevya. Hali hii itakiwezesha kitengo hiki kufanya kazi zake kwa ufanisi.

4. Mhe. Mwenyekiti, ni busara kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kurejesha utaratibu wa zamani wa kutoa mchango wake kwa Jeshi la Polisi, Zanzibar kwa kulipatia vitendea kazi ili nalo liweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

5. Mhe. Mwenyekiti, ni muhimu kwa serikali kuchukua hatua za kutoa maagizo ya kulinda amani kwa kutumia sheria. Kama sheria hizo hazipo basi kuna haja ya kutungwa. Hata hivyo, jambo la msingi ni kuwapatia wananchi elimu ya uraia na masuala ya kulinda amani katika jamii.

6. Kuna haja kwa SMZ kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa kushirikiana na jeshi la Polisi kulishughulikia suala la ukarabati wa nyumba za Polisi za Unguja na Pemba kwa kuziezeka mapaa mipya ili kuzihami zisiharibike kwani bado ni nzima.

Katika kufuatilia ukarabati wa nyumba hizo pamoja na maslahi ya askari Polisi, Kamati ilikutana na Uongozi wa Jeshi la Polisi- Tanzania na kufahamishwa kuwa Jeshi la Polisi lina mipango ifuatayo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, suala la matengenezo ya Nyumba za Polisi IGP alikubaliana na ushauri wa kamati yangu kuwa watajitahidi katika bajeti ya mwaka 2013/2014 na hali ikuruhusu nyumba zitafanyiwa matengenezo.

b) Kuhusu suala la farasi wa Zanzibar ambao wameshatengwa, Jeshi la Polisi lina mpango wa kulikamilisha Banda la Farasi liliopo Zanzibar.

c) Jeshi la Polisi limetuahidi kuanzisha mpango wa kuweka Police Trust Fund ili kuliwezesha Jeshi hilo kuepuka kufadhiliwa katika ujenzi wa vituo na nyumba za polisi na kuliepusha jeshi hilo kutumiwa na wajanja wachache kwa kisingizio kuwa eti wao ndio wafadhili wao, kwani jeshi hilo ni mali ya wananchi wote.

d) Pamoja na Polisi Jamii hapa Zanzibar imefanikiwa ijapokuwa kuna changamoto ya baadhi ya maeneo kutopata mashirikiano mazuri kutoka kwa viongozi wa Jimbo. Hivyo, kikao kimeona kuna umuhimu wa Viongozi hasa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kushirikiana na Polisi jamii katika majimbo yetu ili kuweza kuleta ufanisi katika ulinzi wan chi yetu.

e) Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu imeahidiwa na uongozi wa Jeshi la Polisi kuwa limepanga kuboresha vitendea kazi na mafuta ili Polisi Zanzibar iweze kufanyakazi kwa ufanisi hususan

inapotokea matukio ya dharura. Aidha, jeshi hilo limeeendelea kuongeza idadi ya askari katika Bajeti inayoendelea.

f) Vile vile kamati yangu imeahidiwa kuwa Jeshi la Polisi lina mpango wa kuwa mashine ya DNA ili kuharakisha kesi zinazohitaji uchunguzi wa mashine hiyo. Aidha, jeshi hilo lina mpango wa kufungua Dawati la Masuala ya Unyanyasi kwa lengo la kupunguza matatizo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kikao hicho, Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa pia ilikuwa na maoni na mapendekezo ziada yafuatayo:-

1. Kuna haja kwa Idara ya Upelelezi Zanzibar kupatiwa usafiri ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

2. Kwa kuwa nyumba za askari za Ziwani na Mwera ni kongwe zinahitaji kufanyiwa matengenezo na zaidi kwanza iangaliwe huduma ya dharura yaani ziezekwe ili kuzihami.

3. Nyumba za Tunguu nazo zinahitaji kuezekwa lakini pia kuna haja katika eneo la Tunguu pakajengwa Jengo la Makao Makuu katika Mkoa wa Kusini, Unguja ili kuimarisha ulinzi na usalama katika Mkoa huo.

4. Mhe. Mwenyekiti, kuna haja ya kukiimarisha kituo cha Chwaka kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama katika maeneo hayo ya kitalii.

5. Mgao wa mafuta kwa ajili ya usafiri unahitaji kuongezwa ili kuiwezesha Polisi Zanzibar kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

6. Kitengo cha Anti- drugs kinahihitaji kuimarishwa kwa kupatiwa usafiri, simu pamoja na radio za mawasiliano ili kiweze kupambana ipasavyo na suala la dawa za kulevya.

7. Mbali na kuanzishwa kwa dawati la masuala ya unyanyasi, Askari wanahitaji kupatiwa Elimu kuhusu Masuala ya Kinamama, Watoto na Unyanyasi wa Kijinsia ili kupunguza hali inayojichomoza katika vituo vya polisi kwa baadhi ya wananchi kunyanyaswa kijinsia. Ili kupunguza unyanyasaji wa kijinsia ni hali ambayo imejitokeza katika vituo mbali mbali vya polisi.

Katika kikao hicho, Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa na Uongozi wa Jeshi la Polisi- Tanzania.

Mhe Mwenyekiti, Kamati yangu ilipata nafasi ya kutembelea JKT na jeshi hilo linaendelea na kazi zake vizuri hasa kuwapokea vijana wetu amba wanatoka Zanzibar. Kitu ambacho kinachokiomba Kamati yangu ni kwamba uongozi wa JKU kuweza kushirikiana na uongozi wa JKT ili kujifunza mambo mengi ambayo JKT wamepiga hatua kubwa katika maendeleo kwa JKT. Maendeleo yale basi wenzetu JKU waweze kuyarithi kwa hapa Zanzibar.

Kamati vile vile ilipata fursa ya kutembelea Ofisi ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) Zanzibar na kufahaimshwa Majukumu ya Ofisi hiyo ambayo ni pamoja na kuweka Mfumo wa Utambuzi wa Usajili wa Watu, Wageni Wakaazi na Wakimbizi wenye umri wa mika 18 na kuendelea waishio nchini.
Kamati ilifahamishwa kuwa Mfumo huo una faida kadhaa na miongoni mwa hizo ni hizi zifuatazo:-

a) Kusaidia katika zoezi la Upigaji Kura ya Maoni pamoja na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015.

b) Kusaidia serikali kuongeza wigo wa ukusanyaji wa Kodi na kusaidia Kuongeza Pato la Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mafanikio hayo, Ofisi hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

1. Baadhi ya wananachi kukosekana taarifa zao kwa masheha na kupelekea usumbufu katika utekelezaji wa zoezi la uandikishaji.

2. Baadhi ya wageni hulikimbia zoezi la uandikishaji kutokana na kumalizika muda wao wa kukaa nchini kihalali

Maoni na Ushauri wa Kamati

i) Kuna haja kwa Masheha katika Shehia zao kuwa makini na kuwafuatilia wakaazi na wageni wanaoingia na kutoka katika maeneo yao.

ii) Baada ya kutolewa vitambulisho kwa wananchi, NIDA kwa kushirikiana na Polisi na Masheha inahitajika kufuatilia katika Shehia ili kubaini wenye vitambulisho na wasiokuwa navyo. Aidha, zoezi hilo litasaidia kuwatambua wanaoishi nchini kinyume na Sheria za nchi.

Changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa kazi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba

1. Ofisi hii haina Nyumba yenye hadhi kwa ajili ya makaazi ya Makamu wa Pili wa Rais hasa kwa kule Pemba.

2. Ofisi ya Makamu wa Pili, Pemba haina usafiri wa kutosha.

3. Katika masuala ya bajeti hakuna mfumo wa aina moja wa Kiidara kati ya Idara za serikali zilizopo Unguja na zile za Pemba. Baadhi ya Idara za Serikali zilizopo katika Ofisi za Pemba zinakuwa na bajeti zao na mfano mzuri ni zile Idara zilizopo katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Pemba. Idara za Serikali katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba ni mfano wa Idara zilizopo Pemba amabazo hazina bajeti na badala yake huzitegemea kupitia Kurugenzi za Ofisi zilizokuwepo Unguja. Katika suala la matumizi wakati Ofisi hizo kwa upande wao hazina bajeti zenye kukidhi haja.

4. Idara ya Maafa, Pemba bado haina ghala yake kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vya dharura na badala yake imeazima ghala katika Uwanja wa Michezo wa Gombani huku ikisubiri kupatiwa ghala yake ya kudumu. Idara hii pia haipatiwi vifaa mpaka yatokee maafa. Hali hii inapelekea usumbufu wa majukumu kwa Idara hasa pale yanapotokea maafa.

5. Ofisi ya Tume ya Uchaguzi, Pemba haina jengo lake na badala yake imekodi jengo ambalo hivi karibuni wamejitokeza warithi wa jengo hilo na wameanza kulidai.

6. Taasisi zinazohusika na utoaji wa Elimu ya Uraia, zinashindwa kutoa elimu hiyo kwa jamii kutokana na ukosefu wa fedha.

7. Miradi ya TASAF inayohusu ufugaji, kutokana na kuwepo kwa idadi kubwa ya watu katika kila kikundi na kuwepo kwa kutoelewana kwa wanavikundi, kumepelekea maendeleo yake kuwa madogo ukilinganisha na miradi ya ujenzi na maji ambayo imeonekana kupiga hatua za kimaendeleo.

8. Katika utekelezaji wa TASAF III kumeelezwa kuwa familia maskini zitapatiwa fedha kwa ajili ya ununuzi wa sare kwa watoto wa familia hizo. Hata hivyo, wananchi katika utekelezaji wa TASAF III watatakiwa wachangie 75%, suala ambalo ni gumu kiutekelezaji kutokana na hali duni za kiuchumi za wanananchi.

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Wete na Uongozi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba ulitembelea Mtambwe Kusini kufuatilia suala la Sensa ya Watu na Makaazi iliyofanyika mwaka 2012

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ililifuatilia suala hilo baada ya kuwepo taarifa kwamba katika eneo la Mtambwe zoezi hilo halikwenda vizuri. Kwa kuwa zoezi hilo lilizishirikisha taasisi tofautiza za serikali huku Makamu wa Pili wa Rais akiwa ni Makamu Mwenyekiti wa Taifa katika kamati iliyosimamia suala hilo, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa iliona ni vyema ikalifuatilia suala hilo kufahamu sababu za zoezi hilo kupata changamoto lakini pia kutafuta njia ili suala kama hilo lisije likajichomoza tena.

Wananchi walieleza Kamati pamoja na ujumbe iliofuatana nao sababu zilizopelekea zoezi hilo kutotekelezeka vyema. Sababu hizo ni hizi zifuatazo:-

a) Wananchi wa Mtambwe Kusini, kimsingi, waligoma kujiandikisha katika zoezi la sensa kutokana na ukosefu wa maendeleo katika kijiji chao na vijiji vyenginevyo vya Mtambwe.

b) Wananchi kutopatiwa Vitambulisho vya Mzanzibari ingawa huwasilisha vyeti vya kuzaliwa ili wapatiwe vyeti hivyo.

c) Wananchi kutopatiwa vyeti vya kuzaliwa ijapukuwa waliomba kupatiwa vyeti hivyo katika taasisi husika kwa kipindi kirefu.

d) Wananchi kutopatiwa mikopo ya AK na JK

e) Kuwepo kwa migogoro ya Ardhi isiyopatiwa ufumbuzi

f) Viongozi wa Jimbo kutokuwa na mashirikiano ya karibu na wananchi wao.

g) Wananchi kutoshirikishwa katika kazi za Miradi inayotekelezwa katika Jimbo la Mtambwe. Mfano mzuri wananchi hawakushirikishwa katika ajira ya muda katika ujenzi wa barabara iliyotengenezwa na Kampuni ya Izraeli.

h) Wananchi wengi hawakujiandikisha katika zoezi la sensa kutokana na mkumbo wa Dini. Katika suala la Dini, ilielezwa kuwa tatizo lilianzia Tanzania Bara baada ya kutolewa Takwimu ya sense ya dini ambazo zilizowakasirisha Waislamu.

Maoni na Ushauri wa Kamati

1. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa eneo kwa ajili ya Makaazi ya Makamu wa Pili wa Rais limeshapatikana kuna umuhimu mkubwa wa kuchukuliwa hatua na serikali kupitia Wizara ya Fedha kuweza kujenga jingo hilo.
2. Kuna umuhimu mkubwa kwa serikali kuipatia Ofisi ya Makamu wa Pili usafiri wenye hadhi na wa uhakika kwa ajili ajili ya Makamu wa Pili wa Rais huko Pemba.

3. Ufinyu wa Bajeti na Uchangiaji wa Fedha za Bajeti katika ununuzi wa meli umechangia kupunguza huduma za uendeshaji katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba na taasisi nyenginezo zinazosimamiwa na Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa. Hata hivyo, kuna haja kwa serikali kutenga bajeti itakayoiwezesha Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kufanya shuguli zake kwa ufanisi, hasa kutokana na hadi yake kitaifa.

4. Mhe. Mwenyekiti, ni vyema kwa serikali kuweka mfumo wa aina moja wa kibajeti kwa Idara za Taasisi za Serikali zilizopo Unguja na Pemba, kwa maana ya kuwa Idara zilizopo Pemba nazo ziwe na kasma zao kama inavyoonekena katika Idara za Ofisi ya Wizara ya Afya, Pemba. Utekelezaji wa mfumo huu utaleta ufanisi katika utekelezaji wa kazi lakini pia utawapunguzia mzigo Maofisa Wadhamini, kwani wakati mwingine wakurugenzi hufanya maamuzi ya kiutendaji moja kwa moja kutoka Unguja bila kumjuulisha afisa mdhamini Pemba, kitu ambacho kinachopelekea kama dharau kwa afisa mdhamini ambaye yeye ndie mkuu wa vitengo vyote vilivyoko Pemba.

5. Idara ya Maafa Pemba inahitaji kupatiwa ghala yake kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vyake. Vile vile, Idara hii inahitaji kupatiwa vifaa kabla ya maafa kutokea.

6. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Tume ya Uchaguzi, Pemba imeshapatiwa kiwanja, kuna haja kwa Serikali kuiwezesha Tume kuanza ujenzi wa Ofisi yake.

7. Taasisi zinazohusika na utoaji wa Elimu ya Uraia, mfano Tume ya Uchaguzi, Polisi pamoja na Polisi Jamii zinahitaji kuwezeshwa na serikali ili ziweze kutoa Elimu ya Uraia kwa wananchi.

8. Miradi ya TASAF inayohusu ufugaji ni vyema ikawashirikisha wanavikundi wachache watakaowezeshwa vizuri ili waweze kutekeleza miradi hiyo kwa ufanisi.

9. Kamati yangu inasiitika kwa kuwatelekeza wananchi walioamua kufuga kuku ambapo pia baadhi yao wamepewa pesa na serikali kupitia mradi wa TASAF, kwani imeruhusu kampuni ya fulani kuingiza kuku waliokwisha kuchinjwa na kuangusha bei ya kuku wa hapa Zanzibar, kitu ambacho kimewakosesha ajira na soko la kuuzia kukuwao hasa kwa kuzingatia kuna wafugaji wengi hapa Zanzibar na kuwaacha wakihangaika bila ya kujua hatma ya maisha yao.

10. Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaitaka serikali kupiga marufuku uingizwaji wa kuku hai au walikwisha kuchinjwa, ili kulinda ajira kwa wananchi wetu kama walivyofanya wenzetu T/Bara.

11. Kamati yangu inapongeza serikali kupitia TASAF III kwa kuweza kuwasaidia fedha kwa ajili ya ununuzi wa sare kwa watoto wa familia hizo. Hata hivyo, kamati inaiomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Serikali kwa ujumla kulifikiria tena suala la wananchi katika TASAF III kuchangia 75% katika utkelezaji wa miradi kwani wengi wao hawana uwezo kiuchumi na iweke angalau 50% uwe ndio mchango wa wananchi na asilimia 50% ichangiwe na TASAF.

12. Kuhusu vyeti vya kuzaliwa kwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Wete aliwahi kutoa agizo kuwa mwananchi mwenye tatizo katika kudai cheti cha kuzaliwa aonane nae, ni vyema Wananchi wakaitumia fursa hiyo kwa lengo la kulifuatilia ufumbuzi suala hilo. Lakini Mhe. Mwenyeki, tunashukuru Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwamba suala hilo tayari na yeye ameamua kulivalia njuga. Tunampongeza sana Mhe. Waziri.

13. Vile vile kuna umuhimu mkubwa kwa Viongozi wa Jimbo la Mtambwe kushirikiana na wananchi katika kuviletea maendeleo vijiji vya Jimbo hilo.

14. Taasisi za Serikali zinazoshirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo katika Majimbo mbali mbali, hasa ujenzi wa Barabara zinapaswa kuzingatia umuhimu wa kuwashirikisha na kuwapatia ajira za muda wananchi waliokuwemo katika maeneo inayotekelezwa miradi hiyo kwa lengo la kustawisha maisha ya wananchi hao lakini pia kupunguza malalamiko kwa wananchi.

15. Pia kamati yangu inashauri ni vyema kwa wale wasiokuwa na vyeti vya kuzaliwa na wanasifa ya kupatiwa vyeti hivyo, wakafuata taratibu za kupatiwa vyeti hivyo, likiwemo suala la kula viapo Mahkamani ili waweze kuendelea na mchakato wa kupatiwa Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

16. Suala la mikopo kwa wananchi lina umuhimu wake katika ustawi wa wananchi hao na Taifa kwa ujumla. Hivyo ni vyema mikopo itolewe bila ya kubagua maeneo

17. Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala sugu la migogoro ya Ardhi limechangiwa na baadhi ya Viongozi wakiwemo Masheha. Hivyo, kuna haja kwa viongozi hao kwa kushirikiana na wananchi kuyatatua matataizo hayo, ili wananchi kerejesha imani kwa viongozi wao.

AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilifuatilia Utekelezaji wa Bajeti, Miradi, Sera na Ukusanyaji wa Mapato katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Unguja na kubaini changamoto mbali mbali zikiwemo hizi zifuatazo:-

1. Wananchi bado wanavuna mali asili zisizorejesheka bila ya kufuata Sheria na Utaratibu wa Kimazingira.

2. Bidhaa chakavu kama vile magodoro, nguo na vifaa vya umeme visivyokuwa na viwango bado zinaendelea kuingizwa kwa kasi nchini bila ya utaratibu.

3. Hakuna Utaratibu wa Ufuatiliaji wa Athari za Kimazingira kabla ya kuanza Utekelezaji wa Miradi mbali mbali hasa mikubwa kwa hapa nchini kwetu.

4. Uingizwaji na Utumiaji wa dawa za kulevya bado upo na unaendelea kwa kasi nchini.

5. Mabadiliko ya Tabia nchi yanaendelea kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii.

6. Udhalilishaji wa watu wenye ulemavu bado unaendelea katika jamii.

7. Utata uliopo baina ya wananchi wa Shehia ya kuhusu eneo wanalotaka kulitumia kwa ajili ya mradi wa uhifadhi wa mazingira, eneo ambalo limetolewa kwa mwekezaji kinyume na utaratibu wa kisheria katika eneo la kilimani.

8. Ufukiaji wa shimo lililochimbwa na Kampuni ya Mecco wakati wa ujenzi wa Barabara ya huko Bumbwini.

9. Kuhusu ujenzi wa *Rehabilitation centre* suala limekuwa ni la mda mrefu jambo ambalo linawakosesha vijana wanaocha kutumia madawa ya kulevya kupata pahala pa kurejesha hali na afya zao.

Kamati ilikutana na Uongozi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Pemba na kuna mambo mbali mbali ambayo yaliyojitokeza katika mkutano huo ni haya yafuatayo:-

1. Ofisi inakabiliwa na ufinyu wa bajeti lakini pia uchangiaji wa meli umeongeza tatizo hilo. Mfano Ofisi ilitenga Shs 25,000,000/= kwa ajili ya ununuzi wa gari. Hata hivyo, kuwepo kwa mchango wa meli kumepelekea bajeti hiyo kupungua kutoka kiwango hicho hadi Shs 3,000,000/=. Bajeti ya Mafuta katika Ofisi hiyo imepungua na kufikia 20%. Hali ambayo imeathiri utendaji wa ofisi, likiwemo suala la Ufuatiliaji wa Uharibifu wa Mazingira ambapo kwa upande wa Pemba kumejitokeza tatizo kubwa la Bahari kuivamia maeneo yanayolimwa hasa mpunga na kusababisha uhaba wa maeneo ya kilimo.

2. Ofisi pia inakabiliwa na uhaba wa usafiri. Suala hilo pamoja na ufinyu wa bajeti imepelekea shughuli za uendeshaji pamoja na ufuatiliaji wa uharibifu wa mazingira kuwa mgumu.

3. Sheria ya Mazingira haitoi fursa kwa Idara ya Mazingira kudai fidia baada ya kuzuia ujenzi unaofanywa na muwekezaji aliyekwenda kinyume na sheria. Hali hii imeipelekea Idara ya Mazingira, Pemba baada ya kuzuia ujenzi wa Hoteli ya Muyuni Makangale, na maeneo mengine kushindwa kudai fidia ya aina yeyote baada ya hoteli hiyo kuanza ujenzi bila ya Kufanyiwa Tathmini ya Mazingira.

4. Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inamshauri waziri wa Ardhi na Nishati alifute eneo hilo alopewa muekezaji hapo Kilimani na wapewe wananchi wa Shehia ya Kilimani ili waliendeleze kwani tayari ziko pesa zao kupitia Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa ajili ya kuendeleza mradi huo wa kuhifadhi mazingira katika eneo la Kilimani.

5. Kamati yangu inaishauri Idara ya mazingira kuendelea kushirikiana na wizara ya Miundombinu kuitaka Kampuni ya Mecco ili kulimaliza kulifukia shimo hilo lililopo njia ya kuenedea Bumbwini, ambalo kampuni hiyo ililichimba wakati wa ujenzi wa njia hiyo.

6. Kamati imefarajishwa kwa kufahamishwa kuwa Kurugenzi kuanzia bajeti ya mwaka 2012/2013 zinafanya kazi kibajeti kwa Unguja na Pemba.

7. Uharibifu wa Mazingira bado unaendelea na ni jambo la kusikitisha baadhi ya masheha wanachangia uharibifu huo. Kamati ilishuhudia hayo ilipofanya ziara Rumbwende Kangani kuona uharibifu wa mazingira wa uchimbaji mchanga unaofanywa na wananchi wanaotumia gari za ng'ombe huku sheha akihusika katika kukusanya kodi ada ya uchimbaji bila ya kushauriana na idara ya mazingira.

TUME YA UKIMWI

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaipongeza tume ya Ukimwi kutokana na kazi kubwa wanayoifanya kupambana na kudhibiti maambukizo mapya ya maradhi ya ukimwi pia elimu wanayoitoa kwa jamii inasaidia sana kujikinga na

maambukizi mapya ya maradhi ya ukimwi. Kamati yangu inazipongeza NGO'S zote zinazotoa elimu ya mapambambano dhidi ya maradhi ya ukimwi kwani bila woa basi hali ingelikuwa mbaya, kwani kazi wanazozifanya hasa kuwasaidia wagonjwa walioko majumbani basi hii ni kazi kubwa sana na inastahiki kuwapongeza na tunawaomba kuongeza bidii.
Pamoja na kazi yote ya mapambano haya inayofanywa lakini tujue hivi sasa hali sio nzuri sana kwani baadhi ya wahisani waliokuwa wawasaidia taasisi hizo aidha wameanza kupunguza misaada hiyo na wengine wamekatisha kabisa kwa hiyo tunaishauri Serikali yetu kuendelea kutenga fungu kubwa zaidi katika kila bajeti ya kila mwaka kwa kuweza kusaidia mapambano ya maambukizi mapya dhidi ya gonjwa hatari la ukimwi na hili litafanikiwa tu pale itakapoweza kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kila itapobidi.

Idara ya Watu Wenye Ulemavu

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaipongeza Idara hii kwa kazi kubwa inayoifanya hasa kuwatambua na kutetea haki zao, lakini pia kusaidiana na asasi za kiraia kusaidia kuwapatia huduma pamoja na mafunzo mbali mbali ili kujijua na kujiunga pamoja na kutetea haki zao, kupitia jitihada zao hizo Serikali imesikia kilio chao na kwaka unaomalizia Serikali imeweza kuongeza fungu la Bajeti yao ili kununulia vifaa vya kutumia kwa ajili ya walemavu iliwemo fimbo kwa ajili ya wasioona, lakini bado changamoto inabaki kuitekeleza sera ya watu wenye ulemavu kuwapa kipaumbele hasa katika masuala ya ajira.

Jumuia ya wasioona iliishauri wizara ya Elimu kuwatafutia machine maalum ya kuchapishia vitabu vya kusomea wanafunzi wasioona lakini hadi leo hakuna hatua zozote zilizochukuliwa.

Pia jumuia hiyo iliiomba kamati yangu kusaidia kuifanyia matengenezo barabara ipitayo hapo ofisini kwao katika mtaa wa Kikwajuni wireless kwa kuweka kifusi na lami kwani kwa kuwa wao hawaoni hupata taabu pale wanapopita kuelekea ofisini kwao kutokana na madimbwi makubwa ya maji hasa mvua zinaponyesha.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Ni busara kwa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Pemba ikaongezwa ili kuiwezesha ofisi hiyo kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Aidha, kuna umuhimu mkubwa kwamba inapotokea dharura ya msingi ambapo itapelekea kukatwa kwa bajeti, kushirikisha wadau kama vile Baraza la Wawakilishi lililopitisha bajeti hiyo pamoja na watendaji wa Serikali ambao nao pia huathirika.

a) Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inamshauri waziri wa Ardhi na Nishati alifute eneo hilo na awakabidhi wananchi wa Shehia ya Kilimani ili waliendeleze kwani tayari ziko pesa zao kupitia afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kwa ajili ya mradi huo.

b) Kamati yangu inaishauri Idara ya mazingira kuendelea kushirikiana na Kampuni ya Mecco ili kulimaliza kulifukia shimo hilo lililopo njia ya kuenedea Bumbwini.

c) Kutokana na umuhimu wa utekelezaji wa kazi katika Ofisi hii, likiwemo suala la ufuatiliaji wa uharibifu wa mazingira, Serikali inahitajika kuchukua jitihada za makusudi kwa kuipatia Idara ya Mazingira Pemba usafiri wa kutosha na wa uhakika. Vyenginevyo uhaba wa usafiri na mafuta unapelekea ongezeko la uharibifu wa mazingira pamoja na kuongezeka umaskini katika jamii.

d) Marekebisho ya Sheria ya Mazingira, ambayo kwa muda mrefu iliahidiwa kuwa itawasilishwa Barazani, inahitajika kuwasilishwa Barazani katika mwaka huuu 2013 ili kuiwezesha Idara ya Mazingira kufanya shughuli zake lakini vile vile kukusanya kodi iliyokosekana.

e) Kuna haja kwa Viongozi wa Jimbo Mtambile na Naibu Sheha kulitembelea eneo la Rumbwende Kangani kwa lengo la kulifanyia tathmini. Aidha, ni vyema kwa viongozi hao kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira, na ya Misitu kufikiria kutafuta eneo mbadala kwa ajili ya kuvuna rasilimali hiyo

f) Polisi Jamii katika eneo hilo kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira na Idara ya Misitu inahitajika kutoa Elimu kwa wanananchi kuhusu Athari za Uharibifu wa Mazingira.

g) Serikali kuendelea kuongeza fungu kwenye bajet ya Idara ya watu wenye ulemavu kwa mwaka ujao 2013/14 ili kuweza kuwanunulia vifaa vya kusomea hasa watoto wasioona pamoja na wasiosikia, ikwemo *computer* madaftari na machine za lugha ya alama n.k.

h) Serikali kupitia wizara ya utumishi wa Umma kutekeleza ahadi aliyoitoa Waziri hapa Barazani kwa kuwatengea nafasi maalum za upendeleo watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kujitegemea.

i) Serikali kuifanyia matengenezo maalum Skuli ya Kisiwandui kwa kuijaza kifusi eneo la assemble ambalo hujaa maji mengi wakati wa mvua jambo ambalo linawapa shida watoto wadogo wenye ulemavu wanaosoma hapo wakati Shule hiyo inapokea watoto wadogo sana wenye ulemavu kitu ambacho mvua zikinyesha ni hatari kwa maisha yao.

j) Serikali kujitahidi kuharakisha ujenzi wa Rehabilitation centre ili kuwahudumia vijana walioacha utumiaji wa madawa ya kulevya ingawa kuna *Sobber House* nyingi Unguja na Pemba lakini wengi wa vijana hao hukosa fedha za kujiunga katika sober hizo.

OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Mwenyekiti pamoja na shukuruani ambazo nilizozitoa Kamati ya Ofisi ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ilikutana na viongozi wa Baraza la Manispaa Zanzibar ili kupata kuelewa mambo mbali mbali yakiwemo hatua zilizofikiwa katika Mpango wa Ujenzi wa "*Shopping Malls*" Darajani, Ujenzi wa Ofisi katika eneo iliyopo Diplomatic Supermarket, Kiembesamaki, maendeleo na changamoto katika suala la kuyaendeleza masoko kama vile Darajani na Saateni, maendeleo ya Bustani za Forodhani, Jamhuri garden, Michenzani pamoja na Mradi wa ZUSK na mengineyo

Kamati ilifahamishwa kama ifuatavyo:

a) Kimsingi Serikali imelikubalia Baraza la Manispaa kujenga *Shopping Malls* Darajani ili kuimarisha mapato ya Baraza hilo na kuweka mazingira mazuri ya eneo hilo. Mpango huo pia utawashirikisha wafanyabiashara wa makontena waliopo katika eneo hilo. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iliagizwa na Serikali kukutana na wadaua kama vile Idara ya Mazingira, Mji Mkongwe na wengineo ikiwa ni sehemu ya kufanikisha mchakato huo. Suala hili ambalo tayari limekwishafikishwa serikalini na bado linasubiri majawabu.

b) Kuhusu suala la kujenga Ofisi katika eneo iliyopo *Diplomatic Supermarket* Kiembesamaki, Baraza la Manispaa limo katika mchakato wa kuwasilisha mpango wake wa ujenzi kama lilivyoagizwa na Serikali.

c) Baraza la Manispaa kwa upande wa Soko la Kuku ambalo limo ndani ya Mji Mkongwe, Baraza bado linaendelea kushauriana na Mji Mkongwe ili hatua za ujenzi zianze. Baraza pia limeshatiliana mkataba na wafanyabiashara kwa ajili wa ujenzi wa soko hilo la kuku.

Lakini vile vile limo katika hatua ya kuendelea kuwahamasisha wafanyabiashara kuhamia Soko la Saateni

- Kukifanya kituo cha Dala Dala cha Saateni kiwe kinashusha na kupakia abiria kwa lengo la kuongeza idadi ya wateja.
- Kushirikiana na uongozi wa Dala dala kuwahamasisha wateja kufika eneo hilo
- Kuimarisha mitaro ya maji, kuweka kituo cha Ulinzi na Usalama, kujenga ukuta kwa ajili ya usalama.

d) Lakini vile vile Bustani za Michenzani zinazoendelea kuimarishwa bustani ya Jamhuri.

e) Kuhusu kuwepo kwa changamoto kwa wafanyabiashara katika eneo la Darajani Baraza wametuahidi kwa kushirikiana na taasisi nyenginezo linaandaa mpango wa kuondosha msongomano huo. Kamati yangu inashauri suala hili liharakishwe.

f) Ingawa Baraza la Manispaa walituahidi kuwa katika mwezi huu wa Aprili 2013 lina mpango wa kupata gari mpya za kuzolea taka, kwani bado limekabiliwa na changamoto nyingi lakini hadi leo Mhe. Mwenyekiti, gari hizo bado hazijapatika. .

g) Kuhusu Mradi wa ZUSP, kwa ujumla unaendelea kutekelezwa. Vifaa kwa upande wa Pemba vimekwishapatikana, na kwa upande wa Unguja vinatarajiwa kupatikana mwezi huu wa Aprili 2013. Mbali na Mradi wa ZUSP, walitueleza kuwa Baraza la Manispaa linatarajia kupata msaada wa Wachina wataoweza kutia taa za barabarani katika Manispaa ya Zanzibar.

h) Kuhusu Uboreshaji wa Utendaji katika Baraza la Manispaa. Ofisi ya Baraza hilo imeanza kuchukua hatua ya kutekeleza maagizo yaliyotolewa na Ripoti ya Kamati Teule ya Baraza la Wawakilishi kama alivyoelezea Mhe. Waziri.

i) Bajeti ya Matumizi ya Baraza ipo juu ukilinganisha na uwezo wao kimapato. Aidha, Baraza halipatiwi bajeti yote inayoiomba kutoka Serikalini. Baraza pia halijaachiwa "*Retention"* kama lilivyoahidiwa na Serikali baada ya kupunguziwa baadhi ya vyanzo vyake vya mapato. Ingawa Baraza hilo limeshawasilisha mapendekezo yake serikalini kulikumbushia suala hilo lakini bado hakuna hatua iliyochukuliwa.

Maoni na Ushauri wa Kamati

a) Mhe. Mwenyekiti, Serikali ni vyema ikachukua jitihada ya kuharakisha mchakato wa ujenzi wa *Shoping Malls* Darajani kwa lengo la kuliwezesha Baraza la Manispaa kuongeza mapato lakini pia kulipa haiba nzuri zaidi eneo hilo. Pia kuwekea mazingira bora na kuwaondosha wafanya biashara wadogo wadogo eneo hilo kwani huwasumbua wanafunzi wanaosoma hapo na kuwakosesha raha katika masomo yao.

b) Kuhusu uendeshaji na uimarishaji wa Bustani ya Forodhani, kamati inaona kuwa kuna mvutano wa kimaslahi kati ya Mji Mkongwe na Baraza la Manispaa. Hivyo kuna haja kwa taasisi mbili hizi kukutanishwa ili kutafuta muafaka wa suala hilo, vyenginevyo, Bustani iliyoimarishwa kwa gharama kubwa kwa msaada wa *Aga Khan Foundation* haitodumu kwa muda mrefu. Kamati yangu inamshauri Waziri wa Ardhi pamoja na Waziri Nchi, Afisi ya Rais MBLM kuwakutanisha viongozi wa ile Bodi ya Mji Mkongwe pamoja na Baraza la Manispaa ili kuweza kulipatia ufumbuzi suala hilo.

c) Vile vile kuna umuhimu mkubwa Serikali kulitafutia Baraza la Manispaa eneo muafaka kwa ajili ya kuzihifadhi taka na kutunza mazingira ya Mji wa Zanzibar. Aidha, Baraza la Manispaa linapaswa kuchukua hatua za kuzihifadhi vizuri taka za Darajani, ambazo zimekuwa zikitoa harufu mbaya sana na kuharibu mazingira katika eneo hilo.

d) Serikali inapaswa kulisaidia Baraza la Manispaa kwa kuliwezesha kifedha kwani pia kulipangia mipango mizuri ili liweze kufanyakazi zake kwa ufanisi, vyenginevyo kila siku litakuwa lawamani na kusemwa vibaya. Suala la Baraza kuwezeshwa kifedha na kupangiwa mipango mizuri si jambo geni kwani baadhi ya Mabaraza ya Miji katika nchi mbali mbali zikiwemo zile za Afrika yanafanya kazi vizuri kutokana na Serikali kuu hizo kuziwezesha vyema mabaraza hayo, kuyapangia mipango mizuri na kutoingiliwa katika maamuzi katika mambo yaliyomo ndani ya uwezo wa mabaraza hayo.

e) Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inaitaka Serikali kupitia Baraza la Manispaa kuharakisha mradi wa ZUSP ili kuiboresha mitaro ya maji machafu kwani, mradi huu umeshachukuwa muda mrefu na kuna hatari ya bei ya vitu kupanda na mradi ukaja kukwama njiani. Kwa hiyo tunaomba mradi huo uharakishwe ili kuokoa fedha za wananchi.

Kamati vile vile ilitembelea Chuo cha Mafunzo Ubago na kujionea Chuo hicho ambacho kinakabiliwa na changamoto nyingi zifuatazo:-

1. Chuo kina wanafunzi wachache (19) ambao huwajibika kufanya kazi kubwa kutokana na kuzidiwa na ukubwa wa eneo hilo. Hali hiyo hupelekea askari kulazimika kushiriki katika kazi na kubaki "field" kwa muda mrefu.

2. Ijapokuwa wanafunzi hupata milo mitatu (3) kwa siku, hawana vitanda vya kulalia na badala yake wanalala chini. Mhe. Mwenyekiti ninapozungumza chini nakusudia wanalala kwenye magodoro lakini hayako katika vitanda. Hali hii inadhoofisha afya zao kwani magodoro wenyewe yameshachakaa lakini vile vile kuwa ni mepesi.

3. Wanafunzi hawana viatu ambavyo vinavyohitajika kwa shughuli za kilimo na hasa ikizingatiwa kuna baadhi ya maeneo ya kilimo ni ya maweni na yanahatarisha usalama wao.

4. Chuo hicho hakina usafiri kwa wafanyakazi na wanachuo. Aidha, Chuo hicho ambacho kinachukua jitihada kubwa katika uzalishaj wa mazao mbali mbali hakina zana za kisasa za kilimo zinazohitajika kwa ajili ya uzalishaji zaidi mfano kama trekta.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Kutokana na umuhimu wake na mazingira yaliyopo, katika Chuo hicho chuo kinahitaji kuimarishwa kwa maeneo yake kujengewa ukuta (*fence*), kumaliziwa ujenzi wa mabweni yake, kupatiwa vitanda, usafiri,askari pamoja na wanachuo lakini vile vile kupatiwa viatu kwa wananchuo pamoja na matrekta.
Kwa ujumla kamati ina imani kuwa kuimarishwa wa Chuo hicho, kitapunguza msongomano wa wanafunzi katika vyuo vyengine lakini pia kuongeza ufanisi wa kazi na zaidi katika suala la uzalishaji katika kilimo.

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa pamoja na Mkuu wa Wilaya ya kati na Viongozi wa Serikali ilitembelea Chwaka, Mkoa wa Kusini Unguja kufuatilia suala la Sensa ya Watu na Makaazi iliyofanyika Agosti 2012.

Kamati ililifuatilia suala hilo baada ya kuwepo taarifa kwamba katika eneo la Chwaka zoezi hilo halikwenda vizuri. Kwa kuwa zoezi hilo lilizishirikisha taasisi tofautiza za Serikali huku Makamu wa Pili wa Rais akiwa ni Makamu Mwenyekiti wa Taifa wa Kamati hiyo ya sensa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa iliona iko haja ya kulifuatilia suala hilo kufahamu sababu zilizopelekea tatizo hilo.

Kamati ilijifunza kwamba ijapokuwa Viongozi wa Kisiasa na Vyama tofauti pamoja na Wakuu wa Wilaya walishiriki kuhamasisha wananchi kujiandikisha zoezi la Sensa halikwenda vizuri kutokana na sababu zifuatazo:-

1. Wananchi wengi hawakujiandikisha kwa sababu walifahamishwa na Kikundi cha Dini kuwa atakayejiandikisha atakuwa amekwenda kinyume na Maadili ya Dini ya Kiislamu. Wakati huo kulikuwa na kaya mbali mbali ambazo wananchi wake walisusia zoezi hilo. Baadhi ya kaya hizo ni hizi zifuatazo:-

    a) Unguja Ukuu kaya 99
    b) Uzi Ng'ambwa kaya 99
    c) Kaye Kaebona kaya 1
    d) Kitumba (Shehia ya Kidimni) kaya 19
    e) Uzi kaya 90

2. Baadhi ya wanawake waliambiwa kuwa wakijiandikisha zitakuwa ndio talaka zao
3. Wananchi wa Chwaka wamekata tamaa baada ya vijana wao kutopatiwa ajira za Vikosi vya SMZ. Mfumo wa sasa kwamba vijana wajiunge na JKU kwa ajili ya kupata ajira ya vikosi unapelekea vijana wa Wilaya hiyo kukosa nafasi za ajira. Suala hilo limeshawahi kutokea kuwa kati ya vijana 11 waliojiunga na JKU ni kijana mmoja tu ndiye aliyepata ajira ya JWTZ.
4. Kuwepo kwa malalamiko ya Watu wa Shehia ya Chwaka ngalawa na nyavu zao zilitiwa moto na Serikali kutokana na kufanya uvuvi haramu hii ni sababu nyengine iliyochangia suala hilo. Hata hivyo, kutokana na jitihada za Makamu wa Pili wa Rais na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tatizo hili sasa limetatuka.
5. Baadhi ya wananchi walidiriki kuyakata mabomba ya maji ya mwituni, jambo ambalo limepelekea kuwakosesha maji wananchi wengi ni sababu nyengine iliyochangia wananchi kususia zoezi la uandikishaji wa sensa. Hata hivyo, kamati ilifahamishwa kuwa Mhe Makamu wa Jamhuri ya Muungano aliahidi kusaidia ununzi wa mabomba mapya katika eneo hilo. Lakini Mhe. Mwenyekiti sasa hivi katika eneo hilo suala la maji imekuwa sio tatizo tena. Serikali ya Mapinduzi imeshalitatua.

Maoni na Ushauri wa Kamati

1. Kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali kuwaelimisha wananchi Sheria pamoja na Elimu ya Uraia ili waelewe haki zao na wasikubali kusindikizwa na watu wengine ambao wana malengo yao kwa jambo hili muhimu kwa kuwapotosha. Kwa upoteshaji huu unaweza kuendelea wakati wa chaguzi na sensa zijazo. Lakini pia wananchi hao kutii sheria bila kushuritishwa.
2. Kuna haja ya kuandaliwa Mfumo au utaratibu utakayoiwezesha JKU kuhakikisha kuwa inawapatia ajira Vikosi mbali mbali vijana kutoka Wilaya tofauti ikiwemo Wilaya ya Kati, Unguja likiwemo Jimbo la Chwaka.

Kamati kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Magharibi, Mkurugenzi wa Tawala za Mikoa, Mkurugenzi wa Mipango Miji walitembelea Mwanakwerekwe kusikiliza malalamiko ya wananchi kuhusu eneo la wazi lililojengwa kinyume na Sheria na Utaratibu.

Yaliyojitokeza katika kikao hicho:-

a) Kwa mujibu wa maelezo ya Idara ya Mipango Miji, eneo hilo lilikuwa ni la wazi lakini lilitolewa kihalali kwa Marehemu Sheikh Khatib Mlanzi ili ajenge Chuo. Hata hivyo wakaazi wa eneo hilo walieleza Kamati kuwa jamabo la kushangaza huku Idara ya Upimaji ikishuhudia pamejengwa "Slab" kubwa iliyopelekea wakaazi hao kutokuwa na eneo la kufanya shughuli zao za kijamii kama vile harusi na misiba lakini pia umepelekea baadhi ya wakaazi kutoweza kupita katika eneo hilo.

b) Kamati ilifahamishwa na Idara ya Mipango Miji kuwa kazi ya Idara hiyo kisheria ni kuhusika na kutoa vibali tu na kufuatilia na kusimamishwa kwa ujenzi lakini hawana mamlaka ya kubomoa kile kilichojengwa kinyume cha sheria.

c) Idara ya Upimaji iliifahamisha kamati kuwa Idara hiyo baada ya ujenzi huo, ililipima eneo hilo na kugundua kuwa ujenzi huo umekwenda kinyume na vipimo vya eneo na Idara ilichukua hatua ya kusimamisha ujenzi huo na kuwataka wakaazi wa eneo hilo kutoa taarifa katika Idara hiyo kama ujenzi huo utaendelea.

d) Kwa ujumla wakaazi wa eneo hilo wanataka umiliki wa kiwanja hicho ufutwe, eneo hilo libaki kuwa la wazi kama ilivyokuwa katika ramani ya mwanzo ili kuepusha usumbufu na kuweka amani katika eneo hilo.

e) Kamati ilifahamishwa kuwa matatizo yanaanzia Idara ya Ardhi kwani wao ndio watoaji wa Ardhi hiyo na hutokeza kutoa maeneo bila ya kuzingatia ramani ilivyo.

Kamati inaona kuwa kutokana na hali halisi iliyojitokeza ya mjenzi kutofuata sheria lakini pia kwenda kinyume na lengo la ujenzi lililokusudiwa na kupelekea usumbufu kwa wananchi.

- Kuna haja ya msingi umiliki wa kiwanja hicho kufutiwa na eneo hilo likaendelea kuwa la wazi kama ramani ya mwanzo ilivyoonyesha kwa faida ya wananchi wanaoishi katika eneo hilo.
- Wamiliki wa kiwanja hicho ni vyema wakapewa eneo mbadala. Hivyo, ni vyema kwa Idara ya Upimaji, Idara ya Ardhi, Idara ya Mipango Miji na Idara ya Usajili wa Ardhi zikashirikiana ili kulifanyia kazi suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti Kamati kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Kati pamoja na maofisa mbali wa Wilaya na Mkoa walitembelea Bonde la Matora Bambi kusikiliza malalamiko ya wananchi ambao walielezea kamati kuwa kuna mpango wa Bonde lao kuchukuliwa ili apewe muwekezaji. Walieleza kuwa hawako tayari bonde hilo kulitoa linalozalisha mazao ya chakula ambayo hulima na kujitegemea na familia zao mfano kama viazi, mboga mboga, tungule na matango.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu bonde hilo ilipata maelezo kwamba:

1. Bonde hilo, walirithi kutoka kwa wazee wao tangu enzi za Rais wa kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Karume, ndio ajira yao ya enzi.
2. Lakini vile vile kuchukuliwa kwa bonde hilo kutazipelekea familia zaidi ya mia tatu kukosa ajira wakati hakuna mikakati yoyote inayoandaliwa kuwapatia ajira mbadala wale walioukwa wakijishughulisha na kilimo.
3. Pia waliileza Serikali iwaangalie wananchi wake kwanza na baadae ndio kuangalia wawekezaji na aina ya uwekezaji wenyewe na faida itakayopatikana.

Maoni na Ushauri wa Kamati

1. Kamati yangu inashauri Serikali kuachana na mpango wake wa kutaka kumpa muekezaji eneo hilo kwa ajili ya kufuga ng'ombe wa maziwa katika eneo hilo na kuangalia kumpatia maeneo mengine huyo muekezaji na eneo hilo kuwaachia wananchi Bambi kuendelea kulima na kufuga wao wenyewe ili kuendelea kujiajiri wao wenyewe na kuendesha familia zao, lakini pia kuwapa imani wananchi hao kuona kuwa Serikali yao inawajali na kuwathamini kwani hivi sasa wanahisi kama Serikali yao inawatelekeza, na kuna dalili za kila aina kuwa wananchi hao wameanza kukosa imani na Serikali yao kwa jambo hilo.

Kamati ilikutana na Diwani wa Gamba pamoja na mlalamikaji kutoka Moga kwa kuharibiwa mazao na Mkuu wa Wilaya na Diwani huyo.

Baada ya maelezo ya pande mbili, kamati ilibaini kuwa suala hilo lilihusisha mambo ya kisiasa. Kwa hivyo, kamati ilimrejeshea Mkuu wa Wilaya, Diwani na mlalamikaji kulimaliza wenyewe suala hilo. .

Kamati vile vile ilikutana na Mkuu wa Wilaya ya Magharibi, Mkurugenzi Tawala za Mikoa, Maofisa kutoka kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Diwani wa Dimani, Sheha na Naibu Sheha, maofisa wengine wa Serikali pamoja na mlalamikaji wa Shamba la Fumba ndugu Juma Ali Juma na walalamikiwa ndugu Abdulmalik Shoka Hassanali na ndugu Ramadhan Khamis Msuri ambao walichukua hatua ya kuliuza eneo hilo kwa Ndugu Toufiq S. Turkey.

Lengo la Kamati ni kusuhisha mgogoro huo kupitia taasisi za Serikali na hususan Ofsi ya Mkuu wa Wilaya.

Yaliyojitokeza katika kikao hicho ni haya yafuatayo:-

1. Mlalamikaji alieleza kwa niaba ya ndugu zake kuwa shamba la marehemu baba yao, wao wakiwa warithi, limeuzwa. Mauziano hayo yalifanywa mbele ya Sheha wa Shehia ya Fumba.
2. Walalamikiwa na waliouziwa eneo hilo waliwasilisha mbele ya kikao nakala ya waraka ambao ulikuwa na utata wa uhalali wake. Kopi hiyo ya waraka haikukamilika na haikuonesha nani mmiliki wa eneo hilo. Kwa ujumla waraka huo pia haukuwa na majina.
3. Maofisa kutoka Kamisheni kutokana na utata huo ilieleza kuwa haina waraka huo katika kumbukumbu zaa lakini pia walieleza kuwa Kamisheni ya Wakfu hutoa warka wa urithi baada ya taratibu kukamilika lakini waraka huo ulionyesha kuwa ni wa kubuni na wala hauhusiani na shamba hilo.

Maoni ya Kamati

1. Suala hilo kamati imemuachia Mkuu wa wilaya ya Magharibi Unguja kulishughulikia kwani Sheha wa Fumba ndie aliyehusika na suala hilo na kumsimamia kuweza kulipatia ufumbuzi suala hilo.
2. Kamati yangu inawataka Masheha kuwa makini wakati wanapotoa baraka ya uuzwaji wa mashamba kwani hivi sasa hapa Zanzibar kumekuwa na unyang'anyi dhulma, na ubabaishaji mkubwa katika mauziano ya maeneo ikwemo ardhi pamoja na mashamba jambo ambalo linaweza kupelekea uvunjifu wa amani katika maeneo ya jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilikutana na Uongozi wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Pemba kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa bajeti, miradi, sera na ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha miezi mitatu (3).

Katika ufuatiliaji huo kamati ilibaini yafuatayo:-

1. Halamashauri na Mabaraza ya Miji kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira na taasisi nynginezo za Serikali zimefanikiwa kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki. Hata hivyo, Kamati inazipongeza taasisi hizo za Serikali kwa kuweza kufanikisha zoezi hilo. Hata hivyo, Halmashauri, Pemba bado zinakabiliwa na uhaba wa wafanyakazi katika fani ya sheria na ukusanyaji kodi. Mfano Micheweni kunahitajika wafanyakazi 5 ambao kuweza kuziba pengo hilo.

2. Lakini Ofisi pia inakabiliwa na ufinyu wa bajeti lakini pia uchangiaji wa bajeti katika suala la ununuzi wa meli limeongeza tatizo katika bajeti hiyo.

3. Katika kuwapatia wazee fedha zao za pencheni kupitia Mikoani, Maofisa wa Mikoa huwafuatilia wazee hao majumbani kwa ajili ya kuwalipa pencheni hizo. Hata hivyo, maofisa hao wanalitekeleza zoezi hilo katika mazingira magumu kutokana na ukosefu wa usafiri.

4. Fedha za wazee hao bado zinalipwa na Serikali kwa kupitia O/C. hali hii hupunguza kiwango cha fedha za matumizi kwa taasisi husika.

5. Viongozi wa Kisiasa mbali mbali pamoja na Masheikh walitoa elimu kwa wananchi kuhusu zoezi la Sensa na kupelekea maeneo mengi kufanikisha zoezi hilo kwa asilimia kubwa. Hata hivyo, kuna baadhi ya maeneo zoezi hilo halikwenda vyema kutoka na sababu ambazo kama tulivyokwisha kuzielelza katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

6. Kuna mwananchi karibu na eneo la Uwanja wa Mpira wa Gombani waliruhusiwa kujenga msikiti. Hata hivyo, mfanya biashara ya mbao na kuelezwa kuwa hana leseni wala halipi kodi kwa halmashauri husika. Halamshauri ya Chake ilimuandikia barua Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kuhusu kadhia hiyo lakini majibu mpaka leo bado suala hilo halijapatiwa ufumbuzi kwa hivyo tunaomba suala hilo lishughulikiwe.
7. Baadhi ya wananachi kuwa na vyeti visivyo halali vya kuzaliwa amabavyo walipatiwa kwa ajili ya usajili wa vitambulisho vya Mzanzibari. Ofisi ya Usajili na Vitambulisho, Pemba ilibaini kuwepo kwa vyeti feki vya kuzaliwa 52. Aidha, baadhi ya Masheha huwapa barua kwa ajili ya kwenda kuchukua Vitambulisho vya Mzanzibari watu wasiokuwa na sifa, na kuwakosesha vitambulisho wananchi ambao wenye sifa.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Kamati yangu inahisi kuwa kuna haja kwa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuchukua jitihada za kuzipatia Halmashauri za Pemba watumishi wa kada za sheria na ukusanyaji mapato ili ziweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuongeza mapato na ufanisi katika Halmashauri hizo.

Maofisa wa Mikoa wanahitaji kupatiwa usafiri na mafuta ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi likiwemo suala la kuwapelekea wazee fedha zao za pencheni, lakini vile vile kuna haja kwa Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kutafuta utaratibu wa kuziingiza fedha hizo katika kifungu cha Matumizi Mengineyo (*Other Charges*) kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi na kupunguza malalamiko kwa taasisi za serikali.

Wizara ya Habari, Utamaduni, Michezo na Utalii inapaswa kufuata taratibu za kiofisi, kulifuatilia suala la mwananchi aliyejenga mbele ya Kiwanja wa Gombani eneo ambalo uhalali wake katika kufanya biasahara hiyo, lakini pia Wizara hiyo inawajibika kuijibu kwa maandishi Halmashauri ya Wilaya ya Chake kuhusu suala la ufuatiliaji wa kadhia hiyo.

Lakini vile vile kuna mwelekeo mkubwa kwamba kupatikana kwa vyeti visivyo halali vya kuzaliwa kunatokana na baadhi ya watendaji wa Taasisi za Serikali kuangalia maslahi binafsi. Hali hii inamfanya mwananchi apate cheti katika njia yoyote ile ili apate kitambulisho cha Uzanzibari. Kamati inaona kuwa suala hili ni la maslahi binafsi katika utendaji wa shuguli za serikali na halikubaliki. Hivyo, kuna umuhimu mkubwa wananchi kueleweshwa utaratibu utakaowawezesha wananchi kuweza kupatiwa vyeti kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, Masheha pia wanapaswa kutekeleza kazi zao kwa kufuata Sheria na taratibu zilizopo ili kuhakikisha kuwa wale wenye sifa ya kupatiwa barua kwa ajili ya kutafuta Vitambulisho vya Mzanzibari, wanapatiwa barua hizo.

Kamati yangu vile vile ilikutana na Watendaji wa Idara Maalum na kutembelea Vikosi mbali mbali vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuona maenedeleo na changamoto inavyovikabili vikosi hivyo.

Chuo cha Mafunzo, Pemba. Chuo hiki kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:

a) Ukosefu wa zana na wataalamu wa kilimo na madaktari wa mifugo
b) Ufinyu wa bajeti na uchakavu wa majengo
c) Kuwepo kwa mrundikano wa watuhumiwa ingawa kwa sasa katika kipindi cha miezi minne kiwango hicho kimepungua kutoka 125 hadi 89.
d) Bado hakuna Chuo cha Mafunzo cha Watoto. Watoto bado wanachangayika na watu wazima na kupelekea watoto hao kukulia katika mazingira magumu

Maoni na Ushauri wa Kamati

Chuo cha Mafunzo kichukue jitihada ya kuajiri wataalamu wa kilimo na mifugo. Aidha, Chuo hiki katika suala la mpito kinahitajika kuwapatia mafunzo ya aina hiyo askari wake ili waweze kutoa huduma hiyo kwa ufanisi.

Kwa kuwa Chuo cha Mafunzo, Pemba kimeahidiwa na Makao Makuu Unguja kupatiwa wanasheria wawili, ni vyema mchakato huo ukaharakishwa kwa lengo la kuwasaidia watuhumiwa na wananchuo kupata huduma za kisheria.

Kuna umuhimu mkubwa kwa serikali kutengenisha Chuo cha Mafunzo kwa watu wazima, na lile la watoto kwa lengo la kuwawezesha watoto kuishi kwa amani katika vyuo hivyo vya
mafunzo.

Kamati inakipongeza Chuo hiki kwa kuwakumbusha mahakimu kupitia upya hukumu za watoto ambao hapo kabla hupewa vifungo vikubwa.
Chuo cha mafunzo kuwapatia wanasheria wafungwa ili kuwasaidia kufuatilia rufaa zao ambazo huchukua muda mrefu kusikilizwa, lakini vile vile kuwasaidia wale rumande waliokaa muda mrefu bila ya kesi zao kusikilizwa.

Jeshi la Kujenga Uchumi – Pemba

Maeneo ya kwa Pweza na Msaani ambayo hapo kabla yalikuwa ni mabonde yaliyokuwa na maji ya kutosheleza na kupelekea kuwa na uzalishaji mzuri wa mpunga na mazao mengineyo hivi sasa yamekuwa ni majangwa ijapokuwa JKU inachukua jitihada za kulima mazao mbali mbali.

Kamati imefarajishwa na Jeshi hilo kuwa Jeshi la Polisi siku ya tarehe 23/09/2012 litafika JKU Pemba kuorodhesha vijana wanaotarajiwa kujiunga na Jeshi hilo. JKU ilieleza Kamati kuwa vijana huajiriwa katiak Vikosi vya Ulinzi na Usalama kuzingatia Mikoa.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Kujengwa kwa mashine katika kisima kilichopo kwa pweza na hali ya kisima hicho kudhibitiwa na *ZAWA* kumepelekea Bonde hilo kukauka. Suala la kilimo cha kutegemea mvua nalo limepitwa na wakati. Hivyo kuna haja kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kukutana ili kuisaidia JKU kupata visima kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji katika eneo hilo, vyenginevyo uzalishaji katika maeneo hayo utaendelea kuwa mdogo na usioridhisha.

Serikali inahitaji kuingiza mkono wake kwa ajili ya kuiendeleza JKU, vyenginevyo lile lililokusudiwa katika uanzishwaji wa JKU litakuwa halifikiwi.

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi- Pemba

Kamati ilikutana na Uongozi wa kikosi hiki na kubaini yafuatayo:-

Kikosi cha Zimamoto na Uokozi hutoa mafunzo na vifaa vya zimamoto kwa wenye kujenga majengo ya hoteli. Hata hivyo, chamngamoto iloyopo kwa upande wa Pemba, Zimamoto haishishirikishwi katika ujenzi wa hoteli hizo.

Kikosi hiki hakina vifaa vinavyohitajika kwa kazi zake. Mfano kikosi kinahitaji kupatiwa “protective suits”, magari ya kuzima moto, redio calls na dawa kwa ajili ya maji.

Jengo la Kikosi kwa upande wa Uwanja wa Ndege Pemba, linavuja mno pale mvua zinaponyesha, na kikosi hakiwajibiki kulifanyia matengenezo jengo hilo.

Bado wananchi katika maeneo mengi hujenga bila ya kufuata ‘Planning” za Mipango Miji. Hali hii hupelekea Magari ya Zimamoto kusumbuka kupita katika maeneo hayo wakati wa kufuatilia uzimaji moto.

Maoni na Ushauri wa Kamati

Kuna haja kwa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kukutana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, *ZIPA* na Idara ya Mazingira kukisaidia kikosi hiki ili kiweze kushiriki katika ujenzi wa mahoteli, lakini vile vile nakuwashajihisha wananchi kujenga kwa kufuata “*planning*” ili yanapotokea maafa magari ya zimamoto yaweze kupita.

Kikosi hiki kinahitaji kupatiwa vifaa ili viweze kufanya kazi zake kwa ufanisi

Mamlaka ya Uwanja wa Ndege inapaswa kulifanyia matengenezo jengo la Uwanja wa Ndege, ili kuondosha usumbufu kwa kikosi hiki kuvujiwa na mvua.

Kikosi cha Valantia

Kamati imebaini yafuatayo:-

Kikosi kimeshapewa eneo lake la Micheweni na kukamilisha malipo lakini bado hakijapatiwa hatimiliki. Hata hivyo, jambo la kufurahisha wameshapatiwa magodoro ya kutosha na daktari ameshapatiwa chumba chake.

Choo cha wanawake bado hakijajengwa kutokana na ufinyu wa bajeti.

Eneo la Ndugu Kitu ingawa limepimwa nalo bado halijapatiwa hatimiliki. Katika eneo hili, Kamati imekuwa na mashaka kwa kutopatiwa hatimiliki kwa muda mrefu sasa. Jamabo la kushangaza eneo la Micheweni limeshapimwa na kulipiwa. Kamati inaona katika eneo hili kuna maslahi ya watu binafsi. Hivyo, ilimuagiza Afisa Mdhamini Pemba kulifuatilia suala hilo.

Maoni ya Kamati

1. Kikosi kijenge Makao Makuu yake huko Pemba na kufuatilia hati miliki za maeneo yao.

2. Kuongezwa uingizwaji wa fedha Pemba kwani mgao unaopelekwa Pemba ni mdogo mno haulingani na mahitaji ya kazi. Lakini pia kumaliza madeni ya muda mrefu ambayo kikosi kimekopa kwa wafanya biashara binafsi.

3. Kukamilishwa ujenzi wa choo cha wanawake ili kuweka stara kwa askari wetu.

Malalamiko ya Wananchi Dhidi ya Wawekezaji

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu ilipokea malamiko karibu sita kutoka kwa wananchi, kuhusu dhulma, unyanyasaji wanaofanyiwa na wawekezaji, lakini hapa nimekusudia zaidi malalamiko mawili ambayo nitaliomba Baraza lako tukufu kuiagiza Kamati ya Fedha na Uchumi kwenda kuyachunguza na kuyashughulikia kikamilifu mara tu baada ya kumaliza kikao hichi cha Baraza ili watuletee rupoti katika kikao kijacho, na malalamiko yenyewe ni haya yafuatayo:

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu dhulma waliofanyiwa wananchi wa Kijiji cha Michamvi dhidi ya muekezaji mzalendo mwenye Hoteli ya kitalii inayomilkiwa na MAGEMBE CHEYO, iitwayo (*UTALII BEACH RESORT)* iliyoko

Michamvi Kae, ambapo kwa mujibu wa sheria za ZIPA mwekezaji yeyote kabla ya kupewa kibali cha uwekezaji anatakiwa kuwa ameshalipa fidia kwa wanachu ambao waliokuwepo kwenye ardhi au eneo hilo, lakini kwa kibri na jeuri aliyokuwa nayo mwekezaji huyo aliikata miti ya mazao ya wananchi hao bila ya ridhaa yao, lakini baada ya wananchi hao kwenda kushtaki kwa Mkuu wa Wilaya ya Kusini alikubali kuwalipa wananchi hao shilingi milioni kumi na sita kwa maandishi mbele ya Mkuu wa Wilaya hiyo, lakini hadi leo hii bado hajatekeleza ahadi hiyo.

Lakini kamati yangu pia baada ya kupata malalamiko ya wananchi hao ilimuita Ndugu Magembe Cheyo, Mkuu wa Wilaya ya Kusini Unguja,Wananchi walalamikaji pamoja na mtendaji kutoka ZIPA, katika kikao hicho Ndugu Magembe Cheyo alikiri kuwa kweli amelitumia eneo la wananchi na kukata miti kwa ajili ya uwekezaji wa Hoteli yake hiyo na alikiri kuwa walikubaliana mbele ya Mkuu wa Wilaya hiyo kuwa atawalipa fidia ya shilingi za Tanzania 16 milioni na aliahidi mbele ya Kamati yangu kuwa angeliweza kuzilipa tarehe 25 mwezi November, 2012. Lakini kama kawaida yake aliidanganya Kamati yangu hadi leo bado hajawalipa wananchi hao deni hilo sasa ni zaidi ya miaka mitatu.

Lalamiko la pili ni kuhusu mwekezaji anaemiliki Hoteli ya *CRISTAL HOTEL* iliyoko Paje. Mhe. Mwenyekiti, yeye huyu wananchi wamemlalamikia kwa makosa mengi yasiyopungua sita, kati ya hayo matatu yako mahakamani hatuwezi kuyazungumzia hapa lakini yaliyobaki tunaweza kuyazungumzia.

Kuhusu unyanyasaji unaofanywa na muwekezaji huyo kuwazuia wananchi wasitumie fukwe iliyopo mbele ya Hoteli yake hadi kufikia kuwafukuzisha mbwa wake pale ambapo wanapopita eneo hilo, ambapo kwa mujibu wa sheria za Ardhi na Mazingira eneo la yaishiapo maji ya Bahari basi ni mita thalathini ni za Serikali kila mtu anayo haki ya kuzitumia.

Kuvamia maeneo ya wananchi waliopakana nao na kujenga ndani ya maeneo hayo bila ya ridhaa yao.

Kujenga vibanda vya makuti na kuwalaza watalii jambo ambalo ni kinyume na sheria za ZIPA.

MAONI YA KAMATI

Kamati yangu inashauri Baraza lako tukufu liitake ZIPA kuhakikisha inasimamia sheria zao ili wananchi wetu wasinyanyaswe na wawekezaji ndani ya nchi yao, kwa hiyo imtake muekezaji wa Hoteli wa Utalii Beach Resort ndugu Magembe Cheyo kuwalipa mara moja wananchi hao wa michamvi malipo yao wanayodai kwa muekezaji huyo.

Kamati yangu inaliomba Baraza lako kuiagiza Kamati ya Fedha na Uchumi kufuatilia uhalali wa uwekezaji Hoteli ya Cristal ya Paje, kujua kuwa umefuata masharti ya uwekezaji wa ZIPA, lakini pia kutokana na ukorofi wa muwekezaji huyo kufuatilia malipo ya kodi zote za Hoteli, lakini pia kujua wale watalii wanaolala kwenye vibanda kwenye Hoteli hiyo wanasajiliwa na kama wanalipia kodi inyostahili. Pia kupata maelezo ya wananchi wa eneo la Paje ili kuwasikiliza ni unyanyasaji wa aina gani wanaoupata kutoka kwa muwekezaji huyo wa *CRISTAL HOTEL* huko Paje Unguja na kuleta ripoti hiyo Barazani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo sasa nilikuwa nina maoni yangu machache binafsi. Mhe. Mwenyekiti, kutokana na marekebisho ya ripoti tunazosoma sasa hivi, ripoti zinakuwa ni ndefu sana, kwa kawaida huwa tunasoma ripoti ya kila wizara, lakini sasa hivi inabidi tusome ripoti za wizara tatu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kazi hii ni kubwa na ninaomba sana hasa katika maagizo ambayo tunayaagiza, tatizo kubwa linalojitokeza sasa hivi kwamba wananchi wengi wanaoishi katika ukanda wa pwani wanakuwa wanapata manyanyaso makubwa sana kwa wawekezaji wetu. Kwa hivyo, kitu ambacho nakiomba Mhe. Mwenyekiti, hasa Masheha na Wakuu wa Wilaya kuweza kusikiliza vilio vya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, matatizo mengine yanakuwa sio makubwa kufika pahala yakafika hapa Barazani, lakini kutokana na uzembe na kutokuwa makini na usimamizi wa viongozi waliokabidhiwa majukumu yao kuanzia Masheha pamoja na Wakuu wa Wilaya matatizo haya yanakuwa makubwa na wananchi wanateseka. Haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, leo mwekezaji anafika pahala anawekeza katika eneo anachukua ardhi ya wananchi anashindwa kuwalipa haki zao wakati yeye anaendelea kuzalisha ya ile ardhi ya wananchi hao. Sisi viongozi tupo tunalipwa na serikali kwa ajili ya kuwatumikia wao, lakini vile vile hapa Barazani wanatuleta wao kwa ajili ya kuwatumikia wao.

Sasa nilikuwa naomba hasa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuagiza Waheshimiwa Masheha, Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kushughulikia hizi kero za wananchi. Haya mambo mengine sio ya kuletwa hapa Barazani na nadhani katika ziara ya Mhe. Rais hivi karibuni katika Mkoa wa Kusini alielezea hili, kwamba wananchi wasikilizwe. Sasa leo Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia ndani ya serikali kuna barua nyingi za malalamiko ya wananchi lakini wananchi wanashindwa kupata jawabu. Haiwezekani malalamiko ya wananchi yachukue miaka mitatu au mine bila ya kuweza kupatiwa ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nataka niseme nawashukuru nyote kwa kuweza kunisikiliza, lakini vile vile niwashukuru Wajumbe wangu wa Kamati kwa kuweza kuniruhusu kuja kusoma ripoti tatu kwa pamoja na ninaomba sasa kwa ruhusa yako Wajumbe waendelee kuchangia ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenuyekiti, na mimi kuweza kunipa nafasi asubuhi hii ya leo na nikushukuru sana pamoja na Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi na mimi naomba leo wanistahamilie kama Mwenyekiti wa Kamati aliyemaliza kusoma Saitoti na mimi niweze kuchukua muda kupindukia wake yeye. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kiashirio cha kupigwa makofi basi Wajumbe wamenikubalia.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Mawaziri kila waziri atashughulika na sekta yake wakati Mjumbe anachangia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naanza na kupongeza sana ripoti ya Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti kwa maelekezo yake mazuri sana yenye hisia kali na mimi niweze kumuunga mkono sentensi aliyoimalizia hasa ya uwekezaji. Mimi ni mmoja katika mdau wa kukasirika jinsi ambavyo wanavyotufanyia hawa wawekezaji wengine kwa nia iliyokuwa si nzuri kwa wananchi wetu. Pamoja na serikali kutoa agizo hilo la kuleta wawekezaji ili kupata maendeleo kwa wananchi na hasa kutia kodi na wananchi kupata ajira, lakini kinyume chake imekuwa ni janga wanalotufanyia kwa wananchi wetu au ni fimbo ya kutupigia katika ardhi zetu kwa wananchi wetu waliokuwa watiifu.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa na nina mfano hai mimi kwa wananchi wangu wa Kiwengwa wana uwanja wao mzuri wa mpira wa miguu walikuwa wana nia safi ya kutaka kumkabidhi mwekezaji, lakini kinyume chake imekuwa ni sawa sawa na kuchukua sukari ukaitia baharini namna wanavyofanywa. Mwekezaji amezidi kujikosha lakini hakujikosha kwa mujibu wa utaratibu kwa sababu yale anayotaka yeye wananchi wangu sasa wamekataa kata kata, wamesema hawakubali tena kumpa mwekezaji uwanja huo wanatafuta mtu ambaye sasa hivi watakubaliana naye kwa mujibu wa sheria. Kwa maana hiyo, wamefuta na ile hati aliyopewa kinyume na utaratibu au kinyemela na watu wenye tama kwa sababu kuna watu ambao wana tamaa walikwenda kule wakakunja pesa pamoja na kiongozi mmoja hapa, lakini nampa siku saba na yeye ajieleze si hivyo nitakuja kumtangaza hadharani moja kwa moja. Hati hiyo naomba ifutwe mara moja warejeshewe wenyewe wananchi, sasa niende kwenye mchango wenyewe pengine huko nitakuta mengione.

Mhe. Mwenyekiti, naanza na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa kuweza kuchangia na hasa katika ripoti ya Mhe. Waziri, nimeona hapa ripoti yake ni fupi lakini maagizo ya kamati iliyopita yalikuwa ni kidogo sana. Kwa kweli hii inahudhunisha sana kwa sababu kamati inapofanya kazi kwa uangalifu na serikali inaipa fedha kamati ili kutafuta hizi kero za wananchi ili serikali iweze kutekeleza kwa wakati inakuwa yanalimbikizana mpaka mwisho yanakuwa mengi serikali inashindwa kuyatekeleza.

Kwa mfano, mimi nilizungumzia sana masuala ya nyumba na uzio wa Bomani, nilisema kwamba askari wanaokaa mle niseme kuwa wametupwa, kwa sababu askari anavyotakiwa awe katika nyumba nzuri za kupendeza pale ndio tutasema amehifanyiwa. Nyumba zile tangu enzi za Said Khalifa mpaka leo hii wakati wa ukoloni mimi sina nia ya kuzaliwa, nimezaliwa mpaka nimefika hapa kwenye Baraza hili bado nyumba zile zipo.

Mhe. Mwenyekiti, nyumba zile hazistahili tena kukaa askari kwa sababu ni hatari na tunawatarisha askari wetu wakati wowote nyumba zile kukatika na kuwapotezea maisha. Mimi hushangaa Mhe. Mwenyekiti, tunaambiwa ile ni polisi katika Serikali yetu ya Muungano nao wamo, lakini inakuwaje wawe vile, utakuta nyumba za wenzetu Chang'ombe wenzetu wana nyumba nzuri sana vereje sisi askari wetu wanakuwa nyumba zao mbovu, hapa mimi hujiuliza. Lakini nilichogundua labda sisi wenyewe hatufuatilii ukweli tuseme hivyo, kwa sababu tungelikuwa tunafuatilia haki za askari wetu wa Zanzibar isingefika hali hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha *escort* zote za Marais wetu mbovu, tunaambiwa tuzifanyie *renew*, *recondition*, haa kwa nini? Ni kitu cha kusikitisha. Leo ukiona *escort* ya Rais, Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais zote hazifai.

Siku moja nikwambie Mhe. Mwenyekiti hiyo sio siri ukweli niuseme, tulikuwa na Mhe. Ali katika Kamati yetu Mwenyezi Mungu amjaalie Mzee wetu yule aendelee kumpa fikra nzuri. Mhe. Ali alisema kwa nini Zanzibar katika migao yenu ya gari mnatupa kidogo hasa katika mambo ya *escort* tulikakamaa na mimi mjumbe wake nilikuwemo kwenye kamati ile ya Katiba na Sheria alinipigia *pass* na mimi kwa kuwa mtu wenyewe *sharp* nikaituliza ngoma chini nikanga'ang'ani nikasema haiwezekani, tulikakamaa. Lakini anapigiwa simu Mzee Ali anaambiwa Mzee tayari *escort* tumeshapeleka tatu Zanzibar tukagundua kumbe sisi wenyewe tuna udhaifu wa kufuatilia mambo yetu. Mwenyewe yupo hapa hanisuti kwa sababu nasema vitu kwa *evidence* sisemi uongo, wakati ule alikuwa waziri ambaye alikosa jimbo kule Mwanza jina lake limenitoka, alikazana siku ile akamwambia IGP haraka sana bwana.

Sasa mimi nafikiri mambo mengine jamani tunapokuleteeni mawaziri wetu muwe *serious* na hili suala, sasa na mimi nitakuwa *serious* katika hili na hasa katika bajeti. Naanza kutoa indhari mapema kama sijaona utekelezaji wa nyumba za Bombani, njia zake mbovu Mhe. Makamu wa Pili fanya ziara tunakwenda kudondosha vijumba viwili vitatu tumekwenda kuoneshwa kuwa vimejengwa vya vigorofa vinatusaidia nini kidogo vile, fanya ziara uone kama gari yako itapita pale *benz*, njia chafu kabisa zina mashimo, hazifai kuweka askari wetu pale.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, kamati ilisema kuwa hawa Polisi Jamii serikali iwasaidie na mimi nilisema, Polisi Jamii ni moja katika kuinua, kusaidia polisi, kuondoa uhalifu, lakini Polisi Jamii tumewadharau hata serikali haijatoa kusema kwamba tunatenga fungu maalum kuwasaidia Wallahi Mwenyezi Mungu awajaalie kuwa na roho za imani vile vile wale Polisi Jamii vyenginevyo vyote tutaendelea kuwa na wahalifu wa hapa na pale. Umepungua uhalifu wa hapa na pale kama alivyoisoma ripoti mwenyewe Saitoti pale kuwa umepungua kutokana na kushirikishwa Polisi Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, na hilo naliomba pia, kwenye bajeti hii nitakuwa mkali sana kama sikuona fungu la Polisi Jamii angalau kuweza kuwasaidia. Mhe. Waziri naomba tuwasaidiane polisi jamii jamani tumeweka mfano mzuri pamoja na kuwa polisi wetu hawana zana. Kwa mfano, naweza kusema kuwa juzi nilikwenda katika kesi moja mwananchi wangu alikamatwa Kiboje. Kituo kizuri sana kusema kweli, lakini hakina nyezo gari hakina, lakini kituo kizuri sana tena cha kisasa hapana hata nyumba za kulala angalau hao askari wala gari ya dharura kama akitokea askari kuumwa au kutokea mhalifu kufuatilia tukio hakuna. Jamani hili suala tuwaambie wenzetu upande wa pili na wao watufikirie jamani watupe vitu vya kuokoa wananchi wetu na kufika katika majanga haraka sana. Hilo nasema na kilio chake kimesikika.

Nikienda katika ukurasa mwengine wanne kama nilivyoeleza suala la vituo vyetu na Mwenyezi Mungu atujaalie hivyo hivyo tuendelee kupata na vifaa ambavyo vitawasaidia polisi wetu. Lakini pia polisi hawa wanalalamika wanasema pesa za kufiwa kwenye *salary slips* zao hawazioni kutiwa mle na ukizitaka pesa hizo kwanza aulishie ndio uweze kuzipata. Mimi ningeomba sana Mheshimiwa anayehusika na wizara hii waende wakakae na wenzao hebu waondoleeni hili suala lisifanywe lazima, kama ni lazima basi lifuate utaratibu kwa mujibu wa sheria ziingizwe katika *salary* zao mtu aone pesa zake. Mfano mzuri lakini hatimaye hawanufaiki, kunafaika kwake kunakwenda *slow* kabisa. Mimi naomba sana hili suala nililisema muda uliopita lakini sikuona humu kuwa utekelezaji wake umefikia pahala pazuri vile inavyotakiwa. Vile vile katika uhamisho bado fedha zao zinachelewa kufika, wakienda kule wanakuwa wanapata tabu sana kwa ajili ya utekelezaji.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, nishukuru sana kwa jitihada zao wanazozifanya na hasa katika masuala ya utekelezaji wa hapa na pale, lakini kuna mambo ambayo nataka niyazungumzie kidogo.

Nataka nije katika suala la agizo la wanakamati, inakuwaje agizo la kamati inatowa masuala ya mipaka ya kufungua njia halafu sisi serikali tunakuwa tuna-*delay* kwenda kutatua suala lile. Hili ni suala ambalo linasikitisha sana. Wananchi wetu Mhe. Mwenyekiti, wanapata tabu sana, mwenyekiti alisema kuwa kule kwetu Kiwengwa wanapitishwa baharini katika maji ambayo hustahiki hata wewe mwenyewe binadamu mwenye akili zako kuweza kupita, inakuwaje leo hali kama hiyo. Mimi naomba sana Waheshimiwa Mawaziri hebu kuweni *active* kabisa katika kuamua hizi kamati jamani, haziendi kufanya kazi bure tu, zinakwenda kufanya kazi kwa mujibu wa taratibu za sheria na kanuni zetu na tunalipwa pesa nyingi.

Mimi nakwambieni jamani hizi pesa nyengine tuziogope wengine tunataka kwenda Makka basi tuziogope kuzichukua pesa za kufanyia kazi halafu tusitekeleze, ni suala ambalo linasikitisha sana hili. Kwa sababu kamati inapewa pesa nyingi na inafanya kazi kwa uadilifu lakini wanaleta *presentation* yao inashindwa kufanyiwa kazi. Mawaziri hili lazima tulione jamani, tumekuwa vipi sijui. Labda niseme ingekuwa naweza kuwa Rais, hebu wafanye masihara siku moja tu, Wallahi Mhe. Mwenyekiti, sisemi kwa Mungu wangu lakini siku moja tu na mimi niwe waziri ama watanifukuza au wataniachia milele niwepo, ni *simple* kabisa, inakuwaje wewe waziri unaletewa mashtaka unashindwa kufafanua jambo. Wallahi nakwambia Mhe. Mwenyekiti, siapi kwa Mungu wangu lakini mwezimmoja tu aone nitavyomfanyia kazi. Sasa atajua kumbe kweli mawaziri wangu mimi nikiwachagua wengine wanalala usingizi wanaona raha kupanda kwenye ma- *benz* wananchi huku wanadhalilika, haiwezekani linaniuma sana suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea humu mna mambo mazuri sana kamati imetoa. Kamati imeona jinsi gani vijana wetu askari wanavyokatwa pesa, lakini mpaka leo bado pesa za michezo wanakatwa, pesa za likizo hawapewi. Mimi nilisema Mhe. Rais hebu aweke wizara maalum ili kuondoa haya matatizo halafu anipe mimi Wizara ya Vikosi, lazima wizara hii ipewe bajeti yake maalum ya WAziri wa Vikosi Maalum Zanzibar, tutaondoa matatizo ya askari wetu, itakuwa kila siku askari wetu wanadhalilika tu mishahara midogo na wanafanya kazi nzuri kupita hao Askari wa Muungano, wanajitahidi wanacheza gwaride vizuri lakini pesa zao pengine wanapewa kidogo za posho hili lazima tuwasemee.

Mhe. Mwenyekiti, wanakatwa pesa za michezo kwa sababu gani, pesa ya chakula wanakatwa sijui kama mpaka leo wanaendelea kukatwa, lakini hapa utaambiwa hawakatwi ukienda nje utaambiwa wanakatwa. Mimi naona hili suala kila siku tunalisema hapo kwa hapo kwa nini, wajumbe wangu wangu nakwambieni hebu tuweni na msimamo mara hii, tuwaambie mawaziri waliokuwa hawawajibiki watupishe tukae wenyewe tufanye kazi, msione tabu tumekuja kwa ajili ya wananchi hapa hatukuja kuvaa suti, tumekuja kutetea maslahi ya wananchi watakwenda kutusuta mbele ya safari hiyo lazima tuseme.

Kwa hivyo mimi naomba, kuna maagizo ambayo ni muhimu sana, lakini tunaletewa ripoti na hii ni hasara tukipiga *total* vitabu vyote hivi tunawea tukawalipa wafanyakazi wetu hapa Zanzibar pesa chungunzima kwa vitabu hivi tu. Lakini kutokana na hali halisi utakuta bure tu kwa sababu makaratasi haya yanawajibika kufanya kazi lakini hakuna kinachofanywa.

Mhe. Mwenyekiti: Tujitahidi hayo mawasiliano yanawaumiza wale watu wa ndani, kama kuna simu iko wazi ifungwe kwa sababu wale watu wa mitambo wanaumia masikio. Tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea tena agizo walivyosema wenzetu hawa ni je kwenye suala la *diplomatic*. Mimi nilisema sana hapa na Mhe. Waziri akanambia kuwa basi ulikosekana utaratibu hebu na aje anambie tena sasa utaratibu uliokosekana ni upi, huko nyuma ulitueleza vizuri kuwa utaratibu umekosekana lakini mpaka leo bado marekebisho hakuna tunaacha tu vile vile. Nasema na hili Mhe. Waziri anipe jibu rasmi na anambie kuwa mikataba tayari iko kwenye meza wanapewa watu wa Manispaa kwa kufanya shughuli zao kwa huyo mwekezaji wanaemtaka, hivyo ndivyo tunavyotaka. Lakini bado tu, bado tu, mpaka lini?

Suala la *Shopping Mall*, *Shopping Mall* anavyosema Mhe. Mwenyekiti, tulikwenda Zambia, mmetupeleka Zambia kwenda kutafuta maendeleo tuyalete kwenye Baraza tuwasaidie wananchi. Wenzetu kule wanafanya kazi *24 hours* lakini inategemea tabaka kuna wengine wanafunga mapema wenye maduka, wenye madisko, wenye kuuza nini wanaendelea na *time* zao, wanatia fedha *24 hours.* Lakini sisi sijui kikwazo kiko wapi hiki ni kitu ambacho kinanisikitisha na ndio maana nikawa nasema nataka mambo mengi sio kwa kutaka kwa uchungu wa roho.

Kwa sababu leo mimi nikisema kuwa nipewe Uenyekiti wa Miradi ya Kitaifa kwa nini nilaze nina sababu ya kulaza, kuna kampuni ngapi zishakuja hapa kutaka kuleta maendeleo tunalala, wananchi wetu wanagaragara ajira hakuna, ajira zenyewe zinatozwa kwa pesa watu wananyang'anywa pesa zao hawana ajira wanayopata, hili lazima litusikitishe. Ajira zenyewe hazipo kabisa na zikiwepo watu wanatoa pesa na ajira wakitoa hizo pesa watu hawapewi, tunasema ajira zitazotoka sasa hivi wapewe wale watoto walionyang'anywa pesa, lazima wapewe hakuna vyengine vyovyote lazima tuseme iko siku nitataja, nasema na hiyo watu wajisalimishe mapema iko siku nitataja hadharani hapa wala sitomuogopa mtu kwa sababu nimekamata msahafu. Msahafu nauogopa lakini iko siku nitasema, niletewe kimemo unambie Mheshimiwa ndio mimi niliyefanya mambo yale nitakuwa sisemi, lakini

vyengine vyovyote mimi nitasema ala, wamepata tabu wananchi wamenipigia kura mimi bwana, wamekaa masaa yote kunitafuta mimi halafu mimi leo nisiwasemee, nitawasemea kwa mujibu wa utaratibu ulivyo.

Mhe. Mwenyekiti, pale tuliposema Darajani basi ni lazima yaheshimike maelezo ya kamati tunataka na sisi tuone Zanzibar inabadilika, tuna mambao mengi ya kusikitisha. Kuna watu walitaka eneo lile la Bwawani waigeuze waifanye kama *half London* na watu waweze kupata ajira mpaka leo linasua sua. Pengine tuna tabia moja nataka niwaambie serikali niachiwe niseme, tunatafuta watu wabovu wabovu kwa kuwa mtu apate *income* yake hatutafuti watu waliokuwa *strong* wa kutuletea maendeleo, hili ndio tatizo letu. Pengine eneo la Bwawani lile kapewa mtu pale pote ambaye hata fedha hana wala hajaiona fedha leo mnataka kumpa pale afanye maendeleo. Mimi naona ni sawa sawa na Uwanja wa Ndege anaotaka kupewa mtu ambaye hana maslahi nao, hana uwezo nao hili nalo hatulikubali tunasema. Mamlaka iliyochagua mtu ndiye huyo atakaepewa kazi mwengine hatutaki.

Wawakilishi lazima tuwe imara bwana kwa sababu kuna mambo mengine sisi ndio tutakaojenga nchi. Sisi *back bencher* ndio tunaojenga nchi kupitia kwa mawaziri wetu na mawaziri wetu sio kama wote wako *weakness* hata siku moja, wengi wako *strong* lakini kuna baadhi ya mawaziri lazima tuseme wanapoteza muda katika kuleta maendeleo ya wananchi, wajibu wao wa kuwajibika unakuwa ni mdogo sana.

Kwa hiyo mimi nasema kuwa hii *Shopping Mall* kabisa Darajani tupewe sababu gani mpaka leo inadorora. Kwa sababu liliwekwa *slogan* pale zuri watu wote tukasema *yes*, maendeleo yatakuja sasa hivi, lakini hatuyaoni. Sasa kuna mambo pengine kwa kuwa mtu hajapata 10% anayakwamisha hee, tutafika wapi. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kuwa tuheshimike katika kutoa ripoti zetu hizi za kamati.

Nataka nimalizie sasa hivi kama ulivyosema nimalizie basi nimalizie katika vikosi vyetu vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa KMKM. Mhe. Mwenyekiti, wanajitahidi sana kikosi hiki kulinda magendo hasa karafuu, lakini asilimia yake kama tunavyosema kuwa iangaliwe kwa kina iweze kuwa katika hali ya juu sana. Kwa sababu huo ndio uti wetu wa mgongo tumesema kuwa hii karafuu ni moja katika bidhaa kuu ya serikali.

Lakini humu katika ripoti ya Mhe. Mwenyekiti wangu sikuona lile swali alilosema bado linazungumzika, linazungumzia mpaka lini, tumeanza lini kufanya sisi operesheni hiyo tukijiuliza, tuna muda gani mpaka leo hii bado mnasema linazungumzika ni kitu cha kuamua tu jamani tunasema kwa 100% tu hapo kwani kuna tatizo gani tukisema 100% tuwape, mimi sioni tatizo. Kwa sababu wanafanya kazi ya ujasiri, hatari na wengine pengine wana silaha wale wanaokwenda kuvusha, pengine mle mna kijana wake, damu yake na anakwenda kumtia ndani, lakini leo tunasema *percentage* bado inazungumzika.
Mhe. Waziri naomba sana hili suala tuone jinsi gani linavyoendelea vyengine vyovyote hatusiti kusema waziri ajiuzulu hata siku moja kwa sababu tunataka ufanisi uonekane.

Suala la mwisho Mhe. Mwenyekiti tulisema *salary slip*, nalo hili mpaka leo hakuna utengenezaji wake uko wapi. Tunaambiwa tufungue kidogo kidogo yanazungumzika.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kuiunga kwangu mkono ni Ripoti ya Mwenyekiti wangu wa Kamati tena kwa asilimia mia moja. Lakini indhari yangu mimi na hasa kupitia wananchi wangu wa Jimbo la Kitope wamenambia mara hii nisiwe kucheka cheka upuuzi niweko *serious* katika masuala ya kuamua. Nimesema kuwa jopo litoke Mhe. Waziri twende zetu Bara, hebu chukua mmoja vijana katika sisi twende Bara kule tukadai haki yetu ya Polisi ifanyike pale, usione tabu Mheshimiwa mimi niko *free* hebu twende zetu. Tumeonesha mfano na Mhe. Ali Mzee Ali masihara kumbe si masihara tumefanya kazi, nichukue siku moja au Mhe. Ali Mzee au ile kamati iliyokuwa ya Mhe. Haji Omar Kheir wakati ule hebu waulize tulifanya kazi gani sisi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri usione tabu nichukue mimi kijana wako wala sichukui *brief case* nikawatisha nakwenda *simple* tu, tukifika tu, tunafungua vitabu vyetu vya sheria sisi tuna mgao gani kwa asilimia ngapi tunarudi nayo huku tunawapa askaro wetu wala usipate tabu kwa nini uone tabu.

Mimi hivi ninavyosema wala msinipe posho siku mnaponipeleka Bara nambieni mapema nitajitayarisha posho langu mimi mwenyewe nitachukua, lakini najua kwenda kuwatetea askari wangu wa Zanzibar mafao yao yafike kwa wakati. Hilo la msingi nasema, uniambatanishe kama Mhe. Jazira au Saitoti au nani lakini utavyoamua wewe mwenyewe nani niende nae. Naomba sana hili suala litekelezeke twendezetu Bara tutakusaidieni, nyinyi kama mmeshazoeleka mana pengine mshazoeleka ulikuwa waziri, lakini mimi sijawa waziri ananijua nani mimi ndio

kwanza watanijua leo kwa kuwa nasema, lakini nikifika kule watasema *yes* kaingia kidume hapa sasa toa vitu vya watu.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe kwa kumalizia kutoa mchango wako kwa hamasa kubwa sana. Waheshimiwa Wajumbe kwa asubuhi hii tumemalizia na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na tutakaporejea jioni tutampa nafasi Mhe. Ussi Jecha Haji na baadae Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Naomba tuje mapema ili tuweze kuendelea. Katika orodha yangu nina watu kama tisa hivi lakini ndio tutaanza nao.

La pili kabla hatujaahirisha kuna tangazo hapa, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Wanawake wanatangaziwa kuwa yale mafunzo yao yanaendelea. Kwa hivyo, tukimaliza hapa wao waende kwa mujibu wa utaratibu wao. Baada ya maelezo hayo naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni ahsante.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe idadi ya wanaotaka kuchangia inaendelea kuwa kubwa na kazi yetu leo tunatakiwa tumalize. Kwa hivyo naomba basi tugawane hizi dakika kila mjumbe atumie dakika 15 ili tuweze kuchangia wote na tuweke *points* zetu ili kila mtu asiweze kurejeareja maeneo yale kwa yale.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi hii jioni ya leo kuchangia ripoti ya Kamati ya Kusimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Lakini kabla ya hayo kwanza naomba nisahihishe jina langu ni Ussi Jecha Simai. Pili Mhe. Mwenyekiti, naomba muongozo wako kwa mujibu wa kanuni ya 58 (6) kinazungumzia kwamba kila mjumbe anayejadili hoja ataruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 20 wakati wa vikao mkutano wa kawaida na dakika 30 kwa wakati wa mikutano ya bajeti lakini Spika akiona inafaa anaweza kumuongezea muda msemaji dakika si zaidi ya 10. Sasa Mhe. Mwenyekiti, naona kanuni hii imetupa nguvu zaidi ya kuongeza muda kuliko kupunguza. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mjumbe kwa *concern* yako ambayo inazingatia kanuni kama ambavyo umeelekeza, kilichopo ni kwamba kwa mujibu wa taratibu zetu tulizokuwa tumekubaliana kila kamati na wizara zake tutajadiliana kwa muda wa siku moja.

Sasa ukiangalia wachangiaji ambao wameomba kuchangia mpaka sasa hivi tunao wengi na kila mmoja anataka nafasi ya kuweza kuchangia. Labda tufikie pahala tuamue, tuwape watu muda wao wa kawaida wachangie watakaobahatika tukifika pahala tusitishe hapo na tumuombe Mhe. Waziri afanye majumuisho au tupunguze muda katika kuchangia ili tuweze kuchangia wengi, kila mmoja mwenye *concern* zake ziweze kueleweka na zifahamika ili tuweze kufanya shughuli yetu iende kwa ufanisi zaidi.
Sasa hayo ni maamuzi yenu Waheshimiwa Wajumbe.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, makubaliano yetu yamo ndani ya kanuni hizi, na mara nyingi tumetahadharishana kwamba isipokuwa kwamba kuna ulazima sana tusiwe na tabia ya kuichezea chezea kanuni kila wakati. (*Makofi*).

Sasa Mhe. Mwenyekiti, Mjumbe kasoma na mimi naomba niisome hiyo hiyo Kanuni ya 58 (6) ambayo inasema "Kila mjumbe anayejadili hoja anaruhusiwa kusema kwa muda usiozidi dakika 20 wakati wa mikutano ya kawaida na dakika 30 kwa mikutano ya bajeti lakini Spika akiona inafaa anaweza kumuongezea msemaji dakika si zaidi dakika 10".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hatujakuwa na makubaliano kwamba kamati ichukue siku moja hata katika *briefing*. Tulijaribu kuelekezana kwamba tutizame muda utakavyoruhusu. Kinyume chake tumetumia muda mchache zaidi katika kujadili miswada kuliko vile ambavyo imekubaliwa mwanzo, kwa sababu kila mswada ulitengewa siku moja na nusu angalau lakini kuna miswada ilichukua nusu siku tu ikamaliza shughuli zake. (*Makofi*).

Na awali Baraza hili ilipangwa tulipewa taarifa kwamba litaendelea hadi tarehe 22. Sasa hata utaratibu tuliopewa na Afisi ya Katibu ya kutupangia shughuli mbali mbali zitakavyokwenda, tumepewa lakini tukaambiwa usiuendekeze sana, uendelee kufuatilia mijadala itakavyokwenda kwa sababu mpangilio wa ratiba unaweza ukabadilika kulingana na shughuli za Baraza zitakavyokwenda.

Nimalizie utaratibu Mhe. Mwenyekiti, katika vikao vinne vinavyofanyika kwa mwaka katika Baraza, kikao ambacho Baraza linafanya kazi yake hasa ni kikao hiki cha pili cha kila mwaka. Kwa sababu kikao hiki ndicho kinachofanya shughuli za kifungu cha 5(a) cha Katiba ya Zanzibar, kwamba Baraza hili kazi yake ni kusimamia shughuli za umma wakati huu unapopima utendaji wa serikali kupitia ripoti za kamati na mijadala yetu. (*Makofi*).

Kwa hivyo tunakuomba Mhe. Mwenyekiti, tufuate kanuni ndio makubaliano yetu umruhusu mjumbe asipungue dakika 20 na kama inafaa umuongezee dakika 10 zilizokuwa zimeruhusiwa kwenye kanuni. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakubaliana na hoja za wajumbe lakini kwa mujibu wa ratiba yetu tuliyojipangia kwamba tutachukua siku moja katika kila kamati kujadili. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, busara unazo umeshauliza wajumbe, jee tutumie muda mfupi kwa kuwapa wengi au tutumie muda mrefu kwa kuwapa idadi ndogo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini kwa kwenda kwa mujibu wa utaratibu wetu wa ratiba basi tukitumia muda mrefu kwa wajumbe basi tutatumia idadi ya wajumbe ndogo, mimi naamini wajumbe watakaopata nafasi ya kuchangia watakuwa watakuwa wamekidhi haja ya kutosheleza serikali kuelewa nini wajumbe wanataka.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiria maelezo ya Mhe. Waziri yamefahamika vizuri. Naomba tuendelee Mhe. Ussi.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja naona tuendelee katika hoja iliopo mbele yetu.

Mimi kwanza nitaanza na Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, waswahili wanasema “mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni”. Kwa hivyo na mimi leo kwanza awali kwa mara yangu ya kwanza nadhani naianza kuipongeza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri ambayo inaridhisha sana.

Kumbukumbu zangu tangu tulipoanza kuisimamia ofisi hii kila siku tunakuwa na malumbano makubwa sana na Mhe. Waziri pamoja na watendaji juu ya mitazamo tofauti ya utekelezaji wa kazi. Lakini kwa mara hii, mara ya kwanza maagizo kama 40 haya yamefikia asilimia 90 ya utekelezaji wake. Kwa hivyo ninawapongeza wote walioshiriki katika kuandaa ripoti hii lakini pia kuitekeleza vyema ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza ninapongeza hili agizo tuliipa wizara hii ya kuwapatia usafiri watumishi ambao wanapeleka yale mafao ya wazee vijijini kwetu. Hili limetekelezwa na tunashukuru sana kwa hilo, wazee wetu hapa wamepunguziwa usumbufu kwa kiasi kikubwa kwa kuifuata ile shilingi elfu tano katika maeneo mbali ambapo elfu tano hiyo wangeliweza kuitumia kwa nauli tu badala yake wakarudi vijijini hawana chochote.
Kwa hivyo tunashukuru na tunapongeza sana ila tunaiomba serikali kwa sasa muda umefika kuibadilisha posho hii ya shilingi elfu tano kwa wazee wetu, kwa sababu maisha yamepanda na hali ya fedha imeshuka kwa kiasi kikubwa.
Mhe. Mwenyekiti, la pili ningelizungumzia agizo ambalo tulilitoa kule Pemba kwa Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) kwamba itolewe asilimia fulani wapewe wao katika ukamataji wa magendo ya karafuu ili waweze kufanya shughuli zao, kwa sababu fedha hii tunaona kwamba zinaishia kwa Wakuu wa Mikoa ambapo kazi kubwa tunafanya na idara hii ya KMKM ambapo wao hawanufaiki na chochote na fedha hizi.

La tatu Mhe. Mwenyekiti, ni suala la *salary slip* kwa wafanyakazi hasa watumishi wa idara maalum. Muda mrefu hivi sasa wafanyakazi hawa wamekuwa wakilalamika juu ya kutokutambua mishahara yao. Kwa hivyo tukaona ni

vyema sasa wakati umefika kuwepo kwa uwazi kabisa kwa kuziweka hizi salary za siku zao ili waweze kujua mishahara yao pamoja na mambo mengine yanayohusiana na mafao yao wenyewe.

La nne, niipongeze hatua iliyochukuliwa na serikali ya kuipatia hati miliki Ikulu. Tangu mapinduzi miaka 49 hivi sasa Ikulu ile pale ambayo Marais wote wanakaa ilikuwa haina hati miliki. Hili ni jambo moja baya sana ambalo serikali ilikuwa ikilifanya kwa muda mrefu sana. Lakini pia pamoja na kupatikana na hati miliki hii kuna majengo mengine ya Ikulu ndogo ndogo ambazo zipo mikoani kwetu nazo tunasisitiza haraka zipatiwe masuala ya hati miliki, kwani itafika siku moja tuje tuambiwe Ikulu hii ya mtu au anamiliki mtu fulani. Jambo hilo linaweza likatutia aibu sana katika serikali yetu.

Jengine niipongeze wizara kwa kujitahidi kuwapatia wananchi vitambulisho vya Ukaazi. Tumeona juhudi za Mhe. Waziri kwa kushirikiana na watendaji wake wa Idara ya Vitambulisho pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi hasa wa Pemba kwa kufuatana nao na kwenda kutatua kadhia hii.

Mhe. Mwenyekiti, mambo mengine ambayo kwa ujumla nitazungumzia kwenye wizara hii ni matatizo ya fedha za likizo kwa watumishi wetu wa Idara Maalum au maaskari wetu wa Idara Maalum. Tumeona kwamba maaskari wanafika miezi sita baada ya kwenda likizo fedha yao ya likizo hawajapewa, fedha yenyewe hiyo utaratibu wa serikali ni shilingi laki moja kwa miaka mitatu.

Lakini pia hii inaonekana kama haipatikani. Kwa hivyo tunawazidishia ugumu wa maisha maaskari wetu hawa ambao ni tegemeo kubwa katika kutusaidia kutunza amani ya nchi. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ninakuomba sana kwamba hili lifanyiwe haraka maaskari hawa wapatiwe hizi fedha zao likizo.
Mhe. Mwenyekiti, jengine tukija katika Idara Maalum kuna tatizo kubwa sana. Tatizo lenyewe hili la mikataba. Kuna makamanda wengi sana ambao muda wao wa kustaafu umefika, wanaongezewa miaka miwili, wanaongezewa na miwili tena, sijui utaratibu huu upo kisheria. Kwa hivyo kama upo kisheria utaratibu huu tunamuomba Mhe. Waziri aipelekee serikali suala hili sio zuri kwa sasa.

Kwa sababu moja kubwa. Kwanza inanyima nafasi za ajira kwa vijana wetu, tunao vijana wengi ambao wana uwezo mzuri lakini pia linapelekea kuwanyima askari wengine kupanda vyeo. Mfano KMKM wakuu wa zone wengi wamestaafu wamerejeshwa tena na tena. Kwa hivyo hili ni tatizo na ni kero kubwa kwa Idara zetu Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, ninakuja kwenye posho la mazingira magumu. Kama tunazungumzia mazingira magumu basi moja ni kazi ya ulinzi ambayo inafanywa na vijana wetu hawa wa Idara Maalum hakuna posho. Kwa mfano Chuo cha Mafunzo wao wana-*deal* au wanashughulikia watu ambao wametiwa hatiani kwa makosa mbali mbali na makosa mengine makubwa kabisa. Kwa hivyo watu hawa sasa yoyote wanaweza wakahatarisha maisha ya maaskari wetu. Tunawashukuru sana kuna wakati wanakimbia na wanawakamata. Kwa hivyo hili tuliangalie sana tuwaingizie posho la mazingira magumu wafanyakazi hawa, kwa sababu tukiangalia kwanza askari wenye mishahara midogo mno mishahara ambayo jeshi la Polisi inawalipa maaskari wake kama ni posho tu kwa mwezi, sisi ndio tumefanya mshahara lakini hakuna kitu chengine chochote ambacho kinawapatia watu hawa kwa ajili ya kuwapa motisha kwa kufanya kazi zao kwa ufanisi mkubwa. Hili ni tatizo kubwa. Kwa hivyo lazima serikali ijilazimishe kushughulikia idara hizi ili isije ikasababisha maafa huko mbele.

Watu hawa tumewakabidhi silaha au bunduki, lakini wao wenyewe hatuwajali. Hawa ni binadamu kama binadamu mwengine mwengine, kuna siku wanaweza wakasema tumechoka wakaanza kusababisha maafa katika nchi hii badala yake tukaanza kuja kulaumiana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kupitia serikali naomba sana tuangalie maaskari wetu hawa. Nchi zote duniani zinawajali maaskari wake kwa sababu wana mchango mkubwa sana katika uwekaji wa amani.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo jengine katika Idara hizi Maalum ni suala la kuwapandisha vyeo maaskari. Hili tumekuwa tukilizungumza mara kwa mara. Tunashuhudia kuna maaskari wa KMKM wapo kwa zaidi ya miaka kumi sasa bado hawajapandishwa vyeo na kwa mujibu wa sheria zinazoongozwa idara hizi basi inatakiwa miaka mitatu mtu apendekezwe kupandishwa cheo ikisa hakuna tatizo, na tumeona wengine hawana tatizo lolote lakini pia Zimamoto wapo watu kama hawa, Chuo cha Mafunzo wapo watu kama hawa ambao kupandishwa kwao vyeo ni tatizo. Ni sababu gani ya msingi inayopelekea tatizo bado kuendelea katika Idara Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, jengine katika Idara Maalum namuomba sana Mhe. Waziri fedha za bajeti za Idara Maalum kwa kule Pemba, hili ni kwa idara zote ziliopo kule Pemba naomba sana kwamba ziingiziwe fedha zao moja kwa moja zisipelekwe makao makuu hapa, halafu wao badala yake waje waombe hapa, kule kuna taasisi ambazo zinajitegemea, kuna wakuu ambao wanajitegemea katika kule.

Mhe. Mwenyekiti, tukiachana na Idara Maalum niangalie kidogo suala la masuala ya uwekezaji, hapa tunalizungumzia hili kwa sababu Ofisi ya Rais ndio yenye watu katika mikoa na wilaya. Kumetokezea tatizo kubwa sana kule Paje kwamba kuna wawekezaji hivi sasa wamejivalisha sura za Firauni za kuwasumbua sana wananchi wetu, wao ndio wenye nchi hii hao wananchi, wawekezaji ni wageni wanatoka kwao wanakuja huku wanawadhalilisha wananchi.

Kitendo cha kuwajengea ukuta wananchi wetu wasifike pwani wakapata ile fursa ya nchi yao ya kutumia bahari nzuri Mwenyezi Mungu aliowajaalia, wakapata kutafuta riski kule katika bahari, kitendo hiki sisi haturidhiki nacho. Tunakuomba sana Mhe. Waziri hili likaondolewe mara moja, waachiwe wananchi watumie ufukwe lakini pia njia ile nayo ipatikane ili wapate kufanya shughuli zao.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, hapa zaidi tutakuja kuzungumza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kidogo tutaligusiagusia. Pale Paje kuna kituo kimehifadhiwa nyumba za kulala askari zimefadhiliwa na huyu mwekezaji wa Paje katika Hoteli ya Cristal. Huyu amekuwa kikwazo kikubwa sana. Wananchi wa Paje kwa sasa wanapoteza imani kwa Jeshi la Polisi kuona kwamba kila wanalolifanya wao halichukuliwi na jeshi hili kwa sababu limefadhiliwa kujengewa nyumba na mwekezaji huyu. Jambo hili ni hatari wananchi wanaona sasa kwamba askari labda wamenunuliwa na watu wenye uwezo. Kwa hivyo suala hili si suala la kulifumbia macho ni lazima serikali iliangalie kwa umakini mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kuhusu Tawala za Mikoa, tunaomba ikiwa kuna sheria ambayo inaelekeza moja kwa moja kwamba Mkuu wa Mkoa atakapokuwa pengine hayupo au hawawezi kufanya kazi zake kukaimiwa na Mkuu wa Mkoa mwengine, hili suala hili ni gumu kwa sasa. Tunashuhudia mara kadhaa, tunawaona Wakuu wa Mikoa wengine wanakuwa ni wagonjwa, inakuwa hawapo, kazi zao wanapewa Wakuu wa Mikoa wengine, wakati Wakuu wa Mikoa hawa wanaopewa kukaimu nafasi hizi wao wenyewe uwezo pengine wa kiafanya unakuwa mgumu, hivyo tunawaongezea matatizo zaidi. Kwa hivyo tungeliwapa nafasi bora kwamba Maafisa Tawala wa Mikoa wakafanya hizi kazi za Wakuu wa Mikoa.

Mhe. Mwenyekiti, tukiacha wizara hii nitaangalia Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji sio mambo mengi ambayo kamati yangu iliwapa katika utekelezaji. Lakini miongoni mwa mambo hayo kuna jambo moja kubwa sana la msingi, nalo ni hii Tume ya Uchaguzi juu ya kutoa elimu ya uraia.

Hakuna siri Zanzibar ukitaka kujua udhaifu wa Wazanzibari na mimi miongoni mwao wakati wa uchaguzi unapofika, imani za watu wote zinapotea kabisa. Kila mtu akili yake anaelekeza katika siasa. Wananchi wetu hawana elimu ya kutosha ya uraia. Elimu ya uraia ndio inayomjenga mtu kuwa katika mustakabali mzuri, kujijua wajibu wake nini, haki zake yeye zipi. Kwa hivyo hili Mhe. Mwenyekiti, si jambo la kulifumbia macho, tutakapotoa elimu ya uraia katika nchi yetu hii, tutaweka mustakabali mzuri wa amani, watu wajua wajibu wao nini katika nchi hii. Lakini sheria mbali mbali zinazomeshwa katika elimu ya uraia.

Kwa hivyo Tume ya Uchaguzi kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais suala hili lazima ilifanyia haraka watu wapate elimu ya uraia kabla ya kufika mwaka 2014, tukiingia mwaka 2015 hata hiyo elimu kama itatolewa wananchi wetu hawawezi wakaipokea na kuifanyia kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Umebakiwa na dakika 5.

Mhe. Ussi Simai Jecha: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea mbele kuna tatizo kubwa tulilikuta kule katika Afisi ya Mpiga Chapa wa Serikali. Moja ni posho la mazingira magumu watu hawa hawapewi lakini pesa za likizo ni tatizo sana kwa wafanyakazi hawa.

Tulikwenda na mkurugenzi alikuwepo pole na yeye mwenyewe alikiri kutokuwepo kwa mambo haya. Kwa hivyo tunaomba sana katika idara moja muhimu sana ambayo hii inachapisha siri za serikali muhimu, lakini kama hawa

hatutowajenga katika mazingira mazuri kuna siku tutakuja kulaumiana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hili Wizara ya Nchi (OR) Makamu wa Pili walifanyie umuhimu mkubwa sana.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka haraka ni suala la Mahakama ya Ardhi kwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndiye mwenye dhamana ya serikali karibu zote. Tunaomba sana Mahakama ya Ardhi nayo ipelekwe katika Mahakama Kuu. Sababu kuu moja ya msingi ni kwamba kile ni chombo cha utoaji haki lakini kipo katika muhimu wa serikali. Hapa kidogo pana mashaka makubwa lakini pia udhibiti na usimamizi wa Mahakama hii utakuwa mzuri zaidi ambapo utapelekwa katika Mahakama Kuu kama tulivyoipeleka Mahakama ya Biashara katika kwenye kitengo cha Mahakama Kuu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia haraka haraka suala la nyumba za askari Polisi. Mhe. Mwenyekiti, Jeshi la Polisi ambalo linafanya kazi Zanzibar, linafanya kazi katika Serikali ya Mapinduzi kwa kuwalinda, kuwashughulikia raia wa Zanzibar.

Sasa tutakapokaa siku zote kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ije ishughulikie Jeshi la Polisi huku ambapo ina mikoa zaidi ya ishirini na ngapi kule, hili inakuwa ni tatizo kwa sababu Zanzibar kuna serikali, askari hawa wanalinda viongozi, wananchi, wanakamata wahalifu. Lakini sisi tunaoshughulikiwa kazi hii tunaona kama hatuna wajibu wa kuwashughulikia hawa.

Kwa hivyo tunachoomba nyumba zile pale za askari ni mbovu na tumekwenda juzi katika kamati yetu hii tukazungumza na Mkuu wa Jeshi la Polisi, moja kwa moja alikubali mambo yote ambayo tulimuomba kwamba aje afanye huku kwa sababu ni wajibu wake kuyafanya haya.

Kinachotutia mashaka kwamba mara nyengine tunalaumu masuala ya muungano, hawataki kutushughulikia lakini inaonekana wazi kabisa Serikali yetu ya Mapinduzi haina utamaduni wa kufuatilia masuala ya muungano kule Bara.

Mfano mzuri tumeona Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Mzee nasikia alikwenda Bara siku moja tu kuomba gari ya Polisi, siku hiyo hiyo alipewa gari ya Polisi. Sisi tulipokwenda mambo yote kama mambo saba tulipokwenda kule, yote Mkuu wa Jeshi la Polisi alikubali kuyatekeleza. Sasa basi tunaiomba serikali iende ikafuatilia zile ahadi tulizozichukua kule kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi ili tutayatatua matatizo ya askari wetu hawa.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Muumba wetu Mwenyezi Mungu Mtukufu kuendelea kuturuzuku uhai na uzima tukawa tunaendelea na shughuli zetu katika Baraza hili.

Nikushukuru na wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa tatu katika ripoti hizi za utekelezaji wa ofisi tatu za viongozi na vile vile ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Niruhusu Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze wote mawaziri watatu waliowasilisha ripoti kwa niaba ya ofisi hizi na vile vile mwenyekiti wa kamati ambaye aliwasilisha ripoti yake kwa urefu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na ofisi kubwa kuliko zote, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Bazara la Mapinduzi. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais kwa kuendelea kwake kuiongoza nchi yetu ya Zanzibar, chini ya muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa katika hali ya amani na utulivu. Tunamuahidi ushirikiano wetu na tunamtakia kila la kheri katika kuendelea na kazi yake hiyo ambayo ameianza mwezi Novemba, 2010.
Mhe. Mwenyekiti, ni utaratibu mzuri tuliojiwekea kupitia kanuni zetu baada ya marekebisho tuliyofanya mwaka jana kwamba sasa sio tu tupokee ripoti za kamati, halafu kuna mjadala wa mawaziri watoe majibu ya hoja zilizochangiwa lakini tumeanzisha utaratibu kwamba mawaziri wawe wanatupa ripoti ya utekelezaji wa ripoti ya mwaka uliopita kwamba isiingie tu kapuni kuwa imekwisha tena inakuja nyengine, ile ya zamani imesauhaulika. Tuwe na utaratibu wa kufanya ule wajibu wetu katika chombo hiki wa kuisimamia serikali kuona kiasi gani imetekeleza.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tumemsikiliza Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ninataka nimpongeze kwa maeneo yote ambayo kafanikisha maagizo ya Baraza hili. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kamati

itawasilisha ripoti hapa lakini ikishawasilisha hapa inakuwa sio ripoti ya kamati tena, ni ripoti ya Baraza baada ya Baraza kuipokea na kuikubali.

Lakini niseme pamoja na maeneo ambayo yameonekana utekelezaji wake umeripotiwa vizuri na kwa sababu ya kuokoa muda sitaki kuyazungumza hayo, kwa sababu wajibu wetu ni kukumbusha pale ambapo haturidhiki ili utekelezaji uwe wa kasi zaidi ili huduma za wananchi ziweze kupatikana. Mimi kidogo nimevunjika moyo na lugha ya jumla jumla iliopo humu katika vifungu vingi kwenye hii jadweli ambayo imeambatanishwa katika ripoti hii ya utekelezaji wa Ofisi ya Rais.

Na naomba nitoe mfano Mhe. Mwenyekiti, la kwanza hili halikuzungumzwa kijumla lakini sikuridhika na ile kasi yenyewe. Ni kifungu Na. 2 kinazungumzia ufuatiliaji wa uraia wa watu ili kuhakikisha kwamba vitambulisho hivyo vinatolewa na kutumiwa na wale wenye sifa kama sheria inavyoelekeza.
Sasa katika utekelezaji ninasema ufuatiliaji umefanyika na jumla ya kesi 14 zimepelekwa Idara ya Uhamiaji kwa ajili ya upelelezi na kuthibitisha uraia wa wahusika. Nilikuwa najiuliza Mhe. Mwenyekiti, kwamba hivi kwa mwaka mzima kuanzia Machi/Aprili mwaka jana mpaka Aprili hii, utendaji wa idara hii umeweza kuwanasa watu 14 tu kwa sababu tunawajua watu kwa maelfu ambao wapo mitaani si Wazanzibari na inajulikana hasa ni maeneo gani. Kwa sababu kuna mfano katika sekta ya utalii ndipo unakuta watu wengi sana si Wazanzibari wana vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi wakivitumia kupata haki ambazo si zao ni haki za Wazanzibari.

Sasa najiuliza kwa mwaka mzima tumeridhika kwamba tumepata watu 14 ndio kesi ambayo tunakusudia au tunasema kwamba tuna-*prosecute*, hilo ni moja. Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, katika hayo niliyosema maelezo yake hayaniridhishi ni kwa mfano kifungu nambari 9. Afisi ya Mkuu wa Mkoa Kaskazini Pemba imefanya utaratibu wa kuhakikisha kuwa wazee wanapelekewa pesa za misaada zinazotolewa na serikali ili kuondosha usumbufu na gharama wanazozipata wazee hao katika kufuatilia fedha hizo afisini. Utekelezaji nasema mkoa umeandaa ratiba ya malipo ya pesa za wazee wasiojiweza kwa mujibu wa sheria zao na kwamba maafisa wa Ustawi wa Jamii wameandalisa usafiri maalum kuzifikisha fedha hizo kwa walengwa. Sasa najiuliza kwa mwaka mzima utaratibu kwamba kuna mkoa umeandaa ratiba ya malipo. Mimi nilidhani kwamba tungeambiwa utekelezaji wake kwamba sasa usumbufu huu umeondoka na wazee idadi kadhaa fedha zao wanapelekewa kule walipo, lakini maelezo kama haya yanakosekana Mhe. Mwenyekiti.

Tuchukue kifungu cha 12 Mhe. Mwenyekiti, kinasema;

Kifungu cha 12

> “Kikosi cha KMKM kipatiwe asilimia zaidi ya ofisi za mikoa, mgao unaotokana na shughuli za ukamataji wa karafuu ili ikiwezeshe kikosi hiki kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi”.

Utekelezaji Mhe. Waziri anatuambia utaratibu unaendelea kwa kufanya mazungumzo na mikoa. Najiuliza kwa mwaka mzima bado utaratibu wa mazungumzo tu ndio utekelezaji wenyewe huo Mhe. Mwenyekiti huo.

Lakini njoo katika kifungu cha 15

> “Kuimarishwa kwa shamba la JKU Msaani na Kwa Pweza kwa kupatiwa zana na kuchimbwa visima”.

Utekelezaji. JKU imewaandikia barua ZAWA ili kujua gharama za uchimbaji wa visima hivyo. Yaani kwa mwaka mzima Waziri anatuambia wizara yake imesimamia kuandika barua tu JKU kwa mwaka mzima juu ya utekelezaji wa suala hili, sio kwamba hatimaye tumefanikisha suala hili limetanzuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, niondoke hapo niende katika kifungu nambari 21.

> “Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itachukua hatua za kurekebisha suala la kuwapa uhamisho wa kutoka Pemba kwenda Unguja, au kutoka Unguja kwenda Pemba askari wa Vikosi vya SMZ bila ya kuwapa fedha za nauli za usafirishaji mizigo”.

Utekelezaji unasema. Hatua zimeanza kuchukuliwa. Haya Mhe. Mwenyekiti, ni maelezo ya ubabaishaji kupita kiasi. Ukiona mtu anakuambia hatua zimeanza kuchukuliwa, basi hana majibu. Sasa hakuambii hatua zimechukuliwa, anakuambia zimeanza kuchukuliwa, maana yake wewe hujui ukamate wapi kuhoji utekelezaji huu umefanikiwa au haujafanikiwa. Mhe. Mwenyekiti, mambo kama haya yanavunja moyo sana.

Kifungu cha 22 kupitia mradi wa ZUSP. Pia jengo la Ofisi ya Baraza la Mji Wete litatengenezwa upya kwa gharama ya dola za Kimarekani zipatazo 40.

Utekelezaji. Mshauri Mwelekezi anatarajiwa kufika Pemba na kufanya uchambuzi yakinifu kuhusiana na kazi hiyo, lakini kwa mwaka mzima hajafika anatarajiwa kufika Pemba Mhe. Mwenyekiti. Mradi huu wa ZUSP Mhe. Mwenyekiti, tangu serikali hii imeingia unaimbwa nyimbo leo umeshafika nusu ya kipindi cha serikali hii, bado hatujaona chochote ni hadithi hizi hizi tu, Mshauri Mwelekezi *tender* zimetangazwa, zabuni zinaendelea, hakuna kinachoendelea Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 23 kulifanyia kazi suala la kutoa mishahara pamoja na *salary slip* kwa Askari wa Vikosi vya SMZ. Hivi hili lina uzito wa kiasi gani, kwamba mtu akilipwa mshahara apewe na *salary slip* yake, ili ajue anachopata na anapata kwa misingi ipi. Utekelezaji tunaambiwa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inalifanyia kazi suala la *salary slip*, maana yake halijatekelezwa inalifanyia kazi, hatujui litakamilika lini Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kuonesha kwamba hii ripoti imeandaliwa kwa haraka tu, chukua hata kifungu cha 24 kwenye utekelezaji kunazungumziwa Mtanzania Mkaazi. Mimi nilikuwa najiuliza Mtanzania Mkaazi ndio yupi huyu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, njoo kifungu cha 25, kuhusu usajili wa askari wa vikosi vya SMZ katika mfuko wa hifadhi ya jamii Zanzibar, ZSSF.

Utekelezaji unasema. Kamati ya wanasheria idara maalum ya SMZ wameanza kulifanyia kazi kisheria suala hili. Maelezo ndio haya haya. Mhe. Mwenyekiti, nisiendelee kuupoteza muda wangu bure na Wajumbe wa Baraza lako. Ukienda kwenye kifungu cha 26 ni hivyo hivyo utaratibu wa mazungumzo unaendelea. Ukitizama kifungu cha 28 ni hivyo hivyo na hata ukienda kifungu cha 31 ni hivyo hivyo mazungumzo tu na Mkandara. Ukija katika kifungu cha 33 serikali inachukua hatua ya kuangalia sheria, mwaka mzima bado serikali inachukua hatua ya kuangalia sheria tu, haijaangalia bado. Kifungu cha 35 ni hivyo hivyo na Kifungu cha 36 ni hivyo hivyo hatua zimeanza kuchukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuonesha mfano wa mwisho huu naomba niusome. Kifungu cha 39 kinasema;

> "Kufuatilia fedha". Maana hapa kuna maneno ya Mhe. Saleh Nassor Juma, pana madukhuli kidogo. Kifungu hiki kinasema, "Kufuatilia fedha TShs. Milioni 4 zilizotumika ikiwa ni sehemu ya kwanza ya malipo ya ununuzi wa gari na kujulisha Kamati kila hatua iliyofikia ili kujua hatima ya fedha hizo".

Utekekezaji unasema. Muhusika amepewa *account* namba kwa hatua za kurejesha fedha hizo na ameahidi kufanya hivyo. Mwaka mzima hajarejesha, lakini kaahidi kufanya hivyo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, haya yanaendelea kifungu cha 40 hivyo hivyo na kifungu cha 41 pia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hakika ripoti hii kama kawaida ripoti ya Mhe. Waziri huyu, kwa hakika zinadhalilisha, kuiangusha na kuishushia hadhi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, ni watendaji hawa hawa wanaomfikisha Rais kufika pahala kutangaza katika vyombo vya habari, kwamba tatizo la wanyama wanaotembea katika miji limemalizika, kumbe bado mpaka tunakumbana na ng'ombe na punda katika miji yetu kwa sababu ya kumdanganya Mhe. Rais na huku ni kuidhalilisha Ofisi kubwa. Kwa sababu Ofisi ya Rais Mhe. Mwenyekiti, katika nchi yoyote ni *symbol* ya nchi au ni *symbol* ya utawala. Leo utekelezaji ndio kama huo.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli najiuliza kwamba ikiwa haya bado mazungumzo yanaendelea, hatua zimeanza, tunashughulikia na haya aliyokuja nayo Mhe. Hamza Hassan mwaka huu yataendelea hivi hivi na mwakani yatakuja tena hivi hivi. Sasa mimi nilikuwa nataka kumuuliza rafiki yangu Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Hivi kwa ule uwezo tunaojua sisi wa Kisaitoti wa viwango na kasi, kaikubali ripoti hii na kwamba Wajumbe wake karidhika kuwa huu ndio utekelezaji ambao amekuja kuupongeza hapa, wa serikali kwa mwaka mzima kwa ofisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana pale asubuhi tulimsaidia, tukamwambia hebu usiingie huko, endelea kuwasilisha ripoti yako ya mwaka huu, hii tuachie wenyewe tupate kuendelea na kazi.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea kumwambia Mhe. Rais kwamba asipozingatia vizuri, kuna hatari ya serikali hii kuingia madarakani ikaondoka baada ya miaka mitano, ikiwa hakuna kitu cha msingi chake chenyewe cha kuonesha. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, yako mambo yamerithiwa kutoka serikali iliyopita, yanaendelea na utekelezaji tutajisifu, lakini kwamba limeanzishwa na Serikali ya Awamu ya Saba na likafikia utekelezaji, tutafika pahala tutakuja kusema hakuna kitu, na kwa sababu inayotekeleza utaambiwa ilani ya Chama cha Mapinduzi, sisi tutakuja kusema ilani ya Chama cha Mapinduzi imeshindwa kazi, tutakuja kusema hivyo Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, hatutaki tufike huko. Tunataka Rais awasimamie Mawaziri.

Leo Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nanunua magazeti ya leo, nilipotoka hapa kwenye kikao cha asubuhi, ilikuwa inaonekana kwamba wenzetu wa upande wa Tanganyika wamesema wanaanzisha utaratibu wa kuwatathmini Mawaziri utendaji wao, Waziri Mkuu jana alisema Bungeni. Nadhani tunahitaji utaratibu kama huo kwa Zanzibar wa kuwatathmini Mawaziri wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ili nisiumalize muda wangu wakati bado ndio kwanza namaliza Ofisi ya Rais, naomba niende katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano za ziada.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba uangalie saa yako vizuri. Isiwe kwamba kiti kikawa kinailinda serikali. Tupe haki yetu na ionekane unatenda uadilifu Mhe. Mwenyekiti hapo ulipo.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Kwanza nilikuwa naangalia hapa kwamba katika ripoti ya mwaka jana yalikuwepo maeneo ambayo yalitakiwa yafanyiwe kazi. Moja lilikuwa ni mahoteli yale kukiuka sheria za mazingira. Sasa katika utekelezaji inaonekana ripoti yake zaidi imejikita katika kusema kwamba majukumu haya mengi hayako kwake, kwa sababu usimamizi wa sheria uko katika ofisi nyengine. Sasa hili nilikuwa naomba kwamba Mhe. Waziri na kwa sababu serikali inawajibika kwa pamoja katika Baraza hili, basi ije ituambie na kwa sababu hapa tunazungumzia utekelezaji wa serikali, huko kwengine ambapo wana dhamana ya utekelezaji wa sheria hizi, kikwazo ni nini katika kutekeleza masuala hayo.

Kwa mfano Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa agizo nambari 4. Kufanya marekebisho ya sheria ya mazingira, inasema vikao vya marekebisho ya sheria hiyo viliwahusisha wataalamu wa mazingira, ofisi ya Tume ya marekebisho ya sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, zimefanyika maeneo yanayostahiki kufanywa marekebisho yameorodheshwa na rasimu ya kwanza mpya inayozingatia marekebisho iliyopendekezwa katika vikao hivyo inatayarishwa.

Sasa hili limezungumzwa. Mwaka jana lilikuwemo na katika ripoti ya mwaka huu limo tena, mpaka Mhe. Mwenyekiti wa Kamati mara hii anasema kwamba anaomba litekelezwe mwaka huu, kwa sababu keshachoka na hizi ahadi. Tuambiwe hili litakamilika lini.

Jengine ni kwa mfano kifungu cha 5 Mhe. Mwenyekiti, suala la kufukia shimo la Bumbwini, ambapo MECO ndio wanaohusika. Humu imeripotiwa kwamba wahusika ni Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kwa hivyo, nasema serikali ijibu kwa pamoja, tuambiwe utekelezaji huu umefikia wapi Mhe. Mwenyekiti, na serikali kwa pamoja inavyowajibika hapa Barazani.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, suala la dawa za kulevya. Ningemuomba Waziri atakapokuja kutupa majumuisho mwisho atusaidie. Juzi kumetoka ripoti katika vyombo vya kimataifa yaani magazeti ya kimataifa ambayo yameonesha suala la dawa za kulevya, karibu nusu tani zilizokamatwa katika bahari ambayo imeandikwa karibu na maeneo ya Zanzibar. Sasa nataka kujua je, ilikuwa katika mipaka ya Zanzibar, na kama ilikuwa katika mipaka ya Zanzibar, hivi vyombo vyetu vimekosa ujuzi, uwezo na utaalamu mpaka imefika kwamba ni vyombo vya kimataifa vilivyofuatilia unga ule au dawa zile za kulevya mpaka kufika katika bahari ya Zanzibar, vyombo vyetu vyenyewe havijui taratibu hizi. Naomba kupewa maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Ninayo mambo mengi, lakini kwa sababu ya kuokoa muda naomba nizungumzie machache. Kwanza pamezungumzwa hapa suala zima la *Website* ya serikali ambayo inatakiwa ifanye kazi na ionekane kwamba utendaji wa serikali mtu akitaka kufuatilia maelezo aweze kuona pale. Hili limekuwa ni tatizo kubwa sana la *Website* za taasisi nyingi za serikali kuwa hazifanyi kazi wala hazitoi taarifa kwa mujibu wa wakati wake unavyopaswa.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka nilizungumzie haraka haraka ni suala la Polisi Jamii. Polisi jamii imesaidia, lakini vile vile kuna tatizo kubwa sana la malalamiko ya wananchi, kwa sababu vijana hawa wanaachiwa tu hawana muongozo, na hata wale askari dhamana waliambiwa watafuatana nao, mara nyengine wanakuwa hawapo. Matokeo yake Mhe. Mwenyekiti, hawa inakuwa ni vigumu sana kufuatilia sheria, kwa sababu hawakusomea sheria. Kwa hivyo, wanakuwa wanachukua sheria mikononi mwao wenyewe na wanafanya vitendo vinavyowadhalilisha wananchi. Hayo ni malalamiko makubwa sana Mhe. Mwenyekiti, naiomba Ofisi ya Makamu wa Pili, kwa sababu wao ndio waratibu wa suala hili walifuatilie.

Suala la mwisho katika Ofisi ya Makamu wa Pili Mhe. Mwenyekiti, ni suala sugu la Muungano. Mhe. Mwenyekiti, nimeisikiliza ripoti ya utekelezaji ya Ofisi ya Makamu wa Pili ina kurasa mbili, maagizo moja, mbili, tatu na nne. Hii hapa, je hii ndio *seriousness* ya serikali. Mhe. Rashid Seif Suleiman alivyokuwa huku *back bencher* alikuwa anapenda kusema *be serious!* Na sisi tunaiambia serikali *be serious*! Huu ndio utekelezaji wa Ofisi inayosimamia uratibu wa shughuli zote za serikali na utekelezaji wake Mhe. Mwenyekiti.

Nilikuwa naitazama ripoti ya mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, maeneo yaliyotajwa. Inaonekana haraka haraka tu, tumekwenda katika majumuisho kule mwisho yamezungumziwa mambo manne. Lakini ripoti ya Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa huo mwaka uliopita ina maeneo mengi sana. Sasa kwa sababu ya muda Mhe. Mwenyekiti, sitaki kuyasoma.

Lakini nataka kwenda katika ukurasa wa 189 wa ripoti ya mwaka jana, na ukurasa wa 190 unazungumzia mambo ya Muungano. Mhe. Mwenyekiti, hizi hadithi za kwamba kila siku mazungumzo yanaendelea tumechoka nazo.

Mhe. Mwenyekiti, juzi hapa ndugu yangu Mhe. Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Muyuni aliuliza swali tarehe 5/04/2013 na Hansard ninayo hapa. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili akaorodhesha kama kawaida yake, mambo yanayoshughulikiwa, yaliyokuwa mbioni kushughulikiwa na yaliyokuwa yamekaliwa kitako, kwa lugha tofauti nimeizungumza mimi, lakini maana yake ni ile ile.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tunajiuliza kwamba mpaka lini tutaendelea na suala hili, tulitaka hapa kila kikao tupewe taarifa ya mazungumzo yanayohusu suala la mafuta yamefikia wapi, hatuletewi taarifa hizo Mhe. Mwenyekiti, tunangojewa katika hotuba za kuakhirisha tunaletewa maelezo ya kijumla jumla kwa sababu hatuwezi kujadili tena Baraza linaakhirishwa. Lakini tunajiuliza hivi mpaka lini tutaendelea kusubiri Mhe. Mwenyekiti.

Lakini kama hayo hayamaliziki matatizo mengine yanaongezeka. Juzi Wajumbe wamezungumza hapa Mhe. Mwenyekiti. Leo hata Zanzibar kuheshimiwa kama mshirika, mbia mkuu wa Muungano katika masuala ya ushirikiano wa kimataifa hayaheshimiwi tena. Viongozi wa kigeni wanaokuja wote wanaishia Tanganyia na wanaambiwa wamefika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, huko nyuma tunataka kuorodhesha alikuja Rais George Bush hakufika Zanzibar hapa, alikuja Mama Hilary Clinton hakufika Zanzibar hapa, alikuja Rais Abdalla Gull wa Turkey hakufika Zanzibar hapa. Lakini hivi karibuni kaja Rais Mwai Kibaki Rais mstaafu wa Kenya kaja kuaga, Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano basi msituletee Xi Jinping basi hata huyo anashindwa kuja hapa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hapa nina gazeti la Raia Mwema la jana, mwandishi sio Mzanzibari huyu, Joseph Mihangwa ameandika katika ukurasa wa 15 kwamba bila ya Zanzibar Tanzania isingejua China. Mhe. Mwenyekiti, leo anakuja Rais wa Jamhuri ya Watu wa China anashindwa kufikishwa Zanzibar. Hapa alikuja Choela alifika Zanzibar kwanza mwaka 1965 na tamko lake mashuhuri kutamka kwamba *Africa is for revolution,* kaja kuitamkia ndani ya Zanzibar. Wanapouliza Bungeni kule, tunaambiwa kwamba ati wao wenyewe ndio wanaamua wapi waende. Tunadanganywa watu wazima Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, programu za ziara kiongozi yeyote akitembelea, zinapangwa baina ya wizara mbili, wizara ya nchi anayetoka anayekuja kutembea na wizara ya mambo ya nje ya nchi mwenyeji. Vipi tunaweza kusahauliwa kiasi hiki Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, tunakotoka Zanzibar msingi wa Muungano ulikuwa ni huu hapa, na leo nimewachukulia picha nitakupa zawadi moja na wengine niwape kwa kupitia Makamu wa Pili wa Rais waone huko tunakotoka Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, hii inaonesha Rais wa Jamhuri ya Muungano Mwalimu Nyerere na Makamu wake ambaye ni Rais wa Zanzibar, wamefuatana mguu kwa mguu wanakagua kwa pamoja gwaride la heshima la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hivi ndivyo ilivyokusudiwa. Muungano wa heshima, haki na usawa hii hapa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati nitakupa yako moja zawadi hii. Leo Zanzibar inafanywa kama vile wilaya tu au mkoa mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari wamechoka na ushahidi wa wazi kwamba Wazanzibari wamechoka kama serikali hii haitaki kufungua macho yake ikatizama ikaona, wajifunze jana Mhe. Mwenyekiti. Jana palikuwa na tukio kubwa sana la nchi hii kupokea umeme. Mwaka 2009 tulipokea umeme Pemba, waone uwanja ulivyojaa kwa hamasa, kwa sababu wananchi walikuwa hawakemei serikali ile ilikuwa inawakilisha matakwa yao. Jana tumekwenda kuwachukua watoto wa skuli tukawajaza uwanjani, kuficha aibu kwamba wananchi hawataki hata kusikia suala lile kwa sababu hawaoni kama serikali inatumia maslahi yao hasa katika suala la Muungano.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namalizia maneno yangu kwa kuiambia serikali, kwamba suala hili tulitaka mambo haya yapate ufumbuzi kupitia suala la Katiba. Tukaitaka serikali ichukue msimamo. Ikasema haiwezi kuchukua msimamo kwa sababu itakuwa inaingilia maoni ya wananchi. Wananchi wameshatoa maoni yao. Sasa kabla hatujaenda katika hatua za mabaraza ya Bunge la Katiba toka kusikia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar muda iliyopewa dhamana na wananchi wa Zanzibar kusimamia maslahi yao. Nini mtazamo wake kuhusu hatima na mustakbali wa Zanzibar katika suala hili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nasema tusipoziba ufa tutakuja kujenga ukuta. Jana ni ujumbe tosha kwa Wazanzibar na tukifanya mchezo tutakuja kutokezea huko mbele tusije tukalaumiana. Mwanasiasa yeyote Mhe. Mwenyekiti, ngome yake ni wananchi anaowaongoza, ukipoteza imani ya wananchi Mhe. Mwenyekiti, basi umekwisha.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, nangoja maelezo ya serikali kujibu hoja zangu, halafu tutajua kama tuipokee ripoti au tuirejeshe ripoti ya utekelezaji wa serikali. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru jioni ya leo kuweza kupata nafasi ya kuweza kuchangia maelezo ya Kamati tatu. Lakini kabla ya kuchangia Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii adhimu kabisa kumpongeza Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu haikufanya makosa pale ilipotumia kanuni ya 107 kifungu cha 5(i) kuweza kumchagua Mhe. Hamza Hassan Juma kuwa Mwenyekiti wa Kamati. Pamoja na kwamba tumeelekea ukingoni, kufuatana na kanuni hiyo hiyo katika ukurasa wa 78 kifungu cha 107(4).

Mhe. Mwenyekiti, vifungu hivi viko kwa mujibu wa sheria na tumeletewa kwa mujibu wa sheria. Kile ambacho tulikitumia kumpa Mhe. Hamza Hassan kuwa Mwenyekiti basi hakikumalizikia hapo, kati ya Wenyeviti wenzake kutokana na heshima kubwa walimvisha kiatu cha kuwa Mwenyekiti wa Wenyeviti wote.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi zangu hizo kwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kipindi ambacho ametuongoza cha miaka miwili na nusu kama nilivyosema tunaelekea ukingoni, kufuatana na kifungu cha 107(4), sasa naomba niingie katika mchango.
Mhe. Mwenyekiti, nishukuru kwa dhati kwa kupata fursa hii. Lakini na mimi nisiwe mchache wa fadhila nimshukuru Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa namna ambavyo ameweza kusimamia kazi zake katika kipindi hiki.

Mhe. Mwenyekiti, mazuri mengi Mhe. Waziri ameyafanya, lakini panapo mazuri na mabaya hayakosi. Ni wajibu wetu kuelezea zile kasoro zilizopo ili tumsaidie aweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nilizungumzie Baraza la Manispaa. Mara nyingi tunapenda kulitupia lawama Baraza la Manispaa, kila anayekuja hapa mji mchafu, hali mbaya, *draining* hazifanyi kazi. Niseme tu, tukiangalia upande mmoja Mhe. Mwenyekiti, basi tuangalie na upande wa pili.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa lilikuwa likikusanya kodi za aina mbali mabali katika kipindi cha nyuma. Lakini kwa bahati mbaya baadhi ya kodi zile zimechukuliwa na Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya

Maendeleo kupelekwa ZRB. Katika kuchukua kodi zile palikuwa na makubaliano ya kufanya *retation* kwa zile kodi ambazo zimechukuliwa. Lakini la kusikitisha kwamba hilo Mhe. Mwenyekiti, halijafanyika. Tatizo hilo lilipelekea kuipa hali ngumu Baraza la Manispaa kutokana na kwamba mahitaji yanayohitajika ni mengi, uwezo wa kifedha ni mdogo. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri kuharakisha sera kuileta haraka.

Mhe. Mwenyekiti, kama wengi walivyozungumza tunakuwa tunajenga imani, ustahamilivu, lakini mambo yanachelewa mno na mambo Mhe. Mwenyekiti, yanapochelewa basi hali ya nchi inakuwa hatari.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kutokana na hali hiyo ya kuzidiwa na uwezo Baraza la Manispaa pamoja na kwamba Baraza hili la Manispaa linakabiliwa na ufinyu wa magari, lakini kiutaratibu Mhe. Mwenyekiti, huko tunakotoka Baraza la Manispaa lilikuwa likitumia gari za mawasiliano katika kufanya operesheni za mara kwa mara. Lakini kinachoonekana hivi sasa ni kwamba Baraza la Manispaa halina fedha za kuweza kupata mafuta ya kufanya hiyo operesheni.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba hili suala nimuombe Mhe. Waziri kuliangalia kwa kina na kuweza kulifanyia kazi kwa haraka, vyenginevyo nchi yetu inaweza kukumbwa na maradhi wakati wowote, hali mitaani ni nzito sana.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo Baraza la Manispaa, nimuombe Mhe. Waziri aziangalie sheria za manispaa. Kwa kweli kuna masuala ya mgongano ambayo yanaipa tabu sana Baraza la Manispaa katika masuala mazima ya kisheria. Hili nalo linaipelekea Baraza la Manispaa kutofanya kazi zake kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, moja ya kadhia ambayo Baraza la Manispaa linapata ni suala zima la miundombinu ya maji na hususan nyakati za mvua. Sasa kila mtu analitupia lawama Baraza la Manispaa, kwamba maji hayaendi, michanga imejaa barabarani wakati mtengeneza barabara sio manispaa ni UUB. Sasa mimi nafikiri kuna haja ya kuangalia sheria zetu, ili yale mamlaka yanayostahiki kupewa Baraza la Manispaa basi nafikiri tuwape mamlaka kamili ili tukifikia pahala kwa mzigo wa lawama, basi tuwape lawama ambazo zinastahiki. Lakini tusije kuwapa lawama ambazo hazistahiki kwa kuwabebesha mizigo ya watu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, kadhia hii pia iko katika kitengo cha ardhi, katika masuala mazima ya utoaji vibali migongano inakuwepo, mipango miji ya ardhi wao wanakuwa na sehemu yao, lakini mipango miji ya manispaa wana sehemu yao, lakini hatimaye taasisi moja inayochukua maamuzi na taasisi nyengine inashindwa kufanya maamuzi. Nalo hili linapelekea katika masuala ya kisheria kwenye eneo zima la Mamlaka ya Mji Mkongwe, istifhamu kubwa, kila mmoja anajiona *father* kwa upande wake, Mji Mkongwe ana sheria zake na Manispaa ana sheria zake. Lakini wote inafikia pahala sheria zao zinagongana na kila mtu akamtia mwenziwe lawama katika hali halisi ya maeneo yetu ya Mji Mkongwe. Kadhia hii imejitokeza katika suala zima la Bustani yetu ya Forodhani, bustani nzuri imejengwa na ndugu zetu wa Aghakhan, lakini kutokana na mtiririko wa kuwa na Mamlaka ya Mji Mkongwe, basi pale imeundwa bodi kupitia taasisi mbili. Lakini bodi wao kazi hawafanyi, wao kazi yao kuangalia kinachoingia na kutafuta mapato jinsi ya kuyafanyia kazi. Lakini mzigo wote wa usafi na uendeshaji wa biashara wameachiwa ndugu zetu wa manispaa. Hili tatizo ni kubwa na kwa kweli halina taswira nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie katika taasisi ya manispaa kwa kutaja jambo ambalo mimi linanipa tabu sana, jambo ambalo mimi limenikimbiza kule nikaja hapa. Ni imani yangu wengi watajitayarisha kuja hapa 2015 kutokana na kazi hii hapa.

Mhe. Mwenyekiti, tumewavalisha watu kilemba cha uheshimiwa madiwani, lakini heshima yenyewe Mhe. Mwenyekiti, inapungua kutokana na hali duni waliyokuwa nayo ndugu zetu wa manispaa. Kila tukipiga kelele Mhe. Mwenyekiti, tunaambiwa sera inakuja, iko mbioni na mambo yao yatakuwa mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, ndugu zetu madiwani wana hali ngumu katika kusimamia kazi zao, katika kusimamia serikali ya mitaa ili ifanye kazi zake katika hali ya ufanisi. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri muda umekuwa mrefu, chonde chonde Mheshimiwa tunaomba jitihada ziongezeke, kwa sababu tunafahamu uimara wako ili sera ije haraka katika kikao kinachokuja, ili tuweze kukamilisha zile taratibu.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili ni zito tutakapolifungia macho pasipo na kupitisha sheria hii ya serikali za mitaa, basi ndugu zetu hawa wataishi katika maisha ya mazingira magumu na watashindwa kufanya kazi zao kwa ufanisi uliokuwa mzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niondoke hapo niende katika Vikosi vya SMZ.

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano za ziada.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, leo utakuwa una kazi ngumu sana. Pamoja na busara zako na hekima zako Mhe. Mwenyekiti, kazi itakuwa ngumu. Tumekuja hapa kuisimamia serikali, kuisaidia serikali na kuwatetea wananchi wa nchi hii na pahala pagumu ni hapa katika kuzungumzia masuala mazima ya Kamati. Mhe. Mwenyekiti, dakika hizi zinatuumiza vichwa, itafikia pahala tuseme bora tupitishe tu ripoti watu waende zao, kuliko tabu unayotupa Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, naomba unistahamilie kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia suala la vikosi vya SMZ. Mhe. Mwenyekiti, vilio vya wengi wanaokuja hapa wanapiga kelele katika hali halisi ya mishahara. Mhe Mwenyekiti, vikosi vinafanya kazi kubwa, vinafanya kazi ngumu, kazi ambayo inafika pahala hata Jeshi la Polisi linashindwa. Sasa bado tuna masikitiko katika hali halisi ya kuangalia maslahi yao. Mhe.
Mwenyekiti, unapozungumzia maslahi ya vikosi, jambo kubwa au jibu rahisi unaambiwa hali ya uchumi mbaya, hali ya fedha ndani sio nzuri. Hili Mhe. Mwenyekiti, tunasema halina ukweli, kwa sababu kuna ushahidi wa hali halisi ni nzuri ya nchi yetu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe mfano mdogo tu na hili asubiri taasisi zinazohusika. Hivi karibuni nchi yetu ilikubwa na kadhia ya ubadhirifu wa fedha za wananchi, fedha za walipa kodi. Sasa tunapoambiwa hali ya uchumi mbaya serikali haina pesa, tunapata tabu. Mhe. Mwenyekiti, kuna ubadhirifu unaofanyika katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, kuna bilioni 1.7 inasemekana na uhakika upo wizara itakapokuja tutakuja kuikamata, zimetafunwa kupitia vibali vya uvuvi, hii ni hatari kwa nchi yetu, pesa za wavuja jasho, pesa za wananchi, wananchi wanateseka na tunaandaa utaratibu mzuri lakini unashindwa kutekelezeka.

Mhe. Mwenyekiti, itakapokuja Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuna 61.3 milioni fedha za malipo ya wanafunzi zimeliwa na mshika fedha na hii ni hatari. Sasa tunapozungumza kwamba uwezo wa kuwalipa wafanyakazi wetu tunao, yaani tunaposema kwamba vikosi vyetu viwezeshwe na pale tunapoambiwa kwamba serikali hali ngumu, kwa kweli tunakuwa tunaingia unyonge na tunasikitika sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie suala la utafiti wa mboga mboga. Mhe. Mwenyekiti katika Kikao cha Bajeti kilichopita taasisi hii tuliinyima fedha kwa kuiondoshea fungu baada ya kutoridhika na kazi ya utafiti. Vile vile tulitakiwa kama Kamati tukae na Wizara, ili tuone tunaisaidia vipi JKU katika suala zima la kuwaingizia fedha za utafiti shilingi milioni 40. Mhe. Mwenyekiti, mwaka unamalizika na kwa bahati vikao hivi havijamalizika kukaliwa, ili kuwaingizia fedha hawa wenzetu.

Kwa bahati mbaya tena ya kusikitisha, kwamba wenzetu sehemu ya pili wafadhili ndugu zetu wa Misri wao fedha zao zimeingizwa na tayari zimeanza kutumika, lakini kutokana na kutoingiza fedha za serikali, sasa kazi ya utafiti katika Shamba la Mboga mboga kule Bambi haiendi katika hali nzuri.

Sasa kuna hatari kwamba mradi ule kufa, na utakapokufa basi ndugu zetu wa Misri hawatatufahamu. Kutokana na hali hiyo, nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kutafuta jitihada za kutosha, ili kuona namna gani ya kuweza kuweka sawa, ili kadhia ile ambayo imepita katika Kikao cha Bajeti kilichopita tuweze kurekebisha na kuiweka sawa, kwa ajili ya kuwaingizia fedha zile watumishi wa JKU, ili utafiti ule uweze kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, yako mengi sana na muda utakapofika utaniambia maana yake sijamaliza.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nataka nizungumzie suala zima la kisheria. Nchi yetu kama tunavyosema inaendeshwa kwa mujibu wa taratibu za kisheria za nchi hii na tunakaa hapa kutunga sheria za nchi, kwa kweli tunajitahidi kujiheshimu na kuzisimamia.

Lakini kuna masikitiko kwa ndugu zetu wafadhili Mhe. Mwenyekiti. Kwa mfano, Kamati yangu ilitembelea Paje na ikaona kadhia ya wananchi katika njia iliyofungwa na mfadhili ambaye anaitwa *Crystal*, Mhe. Mwenyekiti wananchi wameshafikia pahala wanakwenda kutukanana naye, sheria zipo, Halmashauri ya Kusini imeshatoa *notice* si chini ya tatu katika suala hili la njia kwa *Crystal*.

Matokeo yake sheria inashindwa kutekelezeka na wananchi wanadhalilika na wanashindwa kwenda baharini kwa ajili ya kufanya shughuli zao za kujitafutia riziki, inabidi wapite masafa marefu. Sasa niombe kwa Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba suala hili ajitahidi kulifanyia kazi, ili tuweze kupata ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe wengi wanakuwa wanalalamika kwamba tunatunga sheria nyingi lakini sheria zetu tunashindwa kuzisimamia pamoja na kuzitekeleza. Kwa kweli kelele zimekuwa nyingi sana na tunafika pahala watu wanaanza kutoa imani na kusema maneno ambayo hayastahiki.

Nikiondoka hapa kuhusu suala la *Crystal* Pemba. Sasa naomba niende Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais nimalizie hapo. Mhe. Mwenyekiti, napenda nimshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji kwa jitihada ambazo amezionesha katika suala zima la kusimamia kutokomeza mifuko ya *plastic*.

Mhe. Mwenyekiti, jitihada tumeziona na naomba ziendelee, kwa sababu kawaida ya Wazanzibari wanapohisi kwamba suala hili basi limesita kidogo wanatumia mwanya huo, ili kuendeleza kuvunja taratibu za nchi na sheria.

Lakini pongezi zaidi naomba niipongeze taasisi ya *Azam Marine*. Mhe. Mwenyekiti, katika safari zangu ambazo siku mbili hizi najaribu kwenda Dar-es-Salaam ndugu zetu wa *Azam Marine* katika kuhakikisha kwamba wanaunga mkono suala la kutoingiza mifuko Zanzibar. Kwa hivyo, utakapopita bandarini ukionekana umechukua mfuko wa *plastic* umetia bidhaa ya aina yoyote basi unanyang'anywa na kupewa mfuko ambao unakwenda na hali halisi ya kukubalika katika nchi yetu.
Kwa kweli ni suala la kupigiwa mfano na kama kuna haja ya sisi basi kutoa matangazo katika nchi za wenzetu zaidi ya pale Tanzania Bara, kwamba Zanzibar mifuko ya *plastic* hairuhusiwi na wala haitakiwa na atakayeingia nayo, basi ajue amevunja taratibu za kisheria. Sasa naomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, niwaunge mkono ndugu zetu wa *Azam Marine* kwa jitihada ambayo wameanza kuionesha kule Tanzania Bara za kuunga mkono jitihada za Makamu wa Kwanza katika kupiga vita mifuko ya *plastic*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kabisa kwa sababu mimi ni mdau

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zingatia muda.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, namalizia kidogo tu, kwa sababu mimi ni mdau wa Bomani pale niko mpakani, na kwa bahati Kamati yangu ilifanya ziara ya kuangalia makaazi halisi ya ndugu zetu wa Jeshi la Polisi, basi tumefanya ziara Bomani, Mwera. Kwa kweli pamoja na mapungufu yote yaliyojitokeza, lakini Ofisi ya Makamu wa Pili imeonesha mfano wa kujitahidi pamoja na Jeshi la Polisi katika kufanya ukarabati wa baadhi ya majengo.

Lakini pamoja na jitihada hizo nadhani kunahitajika jitihada za haraka au za nguvu zaidi, kwa sababu pamoja na yale majengo ambayo tayari yameshafanyiwa ukarabati, lakini yapo majengo ambayo yamekaa katika hali mbaya. Kwa hivyo, nashauri kwamba uwezo wa fedha ni mdogo, basi angalau majengo yale yakaezekwe, ili kuondosha ile kadhia ya kuvuja na baadaye kuanguka.

Mhe. Mwenyekiti, matatizo katika Jeshi la Polisi ni mengi. Kwa hiyo, naiomba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, ikaangalia jitihada zilizokuwa zikifanywa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano ilikuwa ikifanya jitihada binafsi katika kusaidia masuala mazima ya kulisaidia Jeshi letu la Polisi na jitihada hizi zilionekana kwa kuwa serikali wakati ule wa uongozi wa Dkt. Salmin Amour Juma alikuwa akinunua magari na kulikabidhi Jeshi la Polisi na tumewahi kuona Jeshi la Polisi waliwahi kukabidhiwa magari aina ya *TATA* na *LAYLAND*.

Sasa jitihada zile zinahitaji kuungwa mkono, ili kulisaidia jeshi la Polisi kuondokana na uchache wa magari na kutumia magari machakavu na hususan magari ya *escort* za viongozi, kwa ajili ya kuweka usalama wa viongozi wetu katika hali nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani naunga mkono Ripoti hii ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Kitaifa, ambayo inaongozwa na Jemedari, Kamanda Mhe. Hamza Hassan Juma, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru na mimi kunipa nafasi hii kuweza kuchangia katika masuala mbali mbali yanayohusu Wizara zetu hizi tatu ambazo ni wizara mama, ambazo ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
Awali ya yote Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujaalia kufika hapa tukiwa na afya njema na katika kutekeleza shughuli zetu ambazo zimetuleta hapa.

Vile vile nichukue fursa hii adhimu kumpongeza sana Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Hamza Hassan Juma kama alivyotangulia Mhe. Ali Salum Haji, ambaye kwa kweli anazo sifa na umahiri wa kuwa Kiongozi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka miwili na nusu ambacho tumekuwa katika Kamati hii, yaani kamati yetu haikuwa inakosa kitu cha kufanya. Hali hii si kwa sababu yoyote isipokuwa Mwenyekiti wetu alikuwa mtundu na anatafuta nini cha kufanya. *(Vicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nakuhakikishia tena kwamba hata akirudi Mhe. Hamza Hassan Juma kwenye Kamati yoyote basi atakuwa Mwenyekiti, kwa sababu uwezo anao. *(Makofi)*

Nianze mchango wangu kwa kuzipongeza wizara zetu zote tatu ikiwemo Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Wizara ya Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kazi ngumu ambazo wanazifanya.

Mhe. Mwenyekiti, wakati tulipokuwa tukisimamia wizara hizi tumezikuta zina changamoto nyingi, lakini mambo mengine yalikuwa sio kwa makusudi isipokuwa kutokana na hali yetu. Nikisema hivyo, nina maana kwamba kutokana na hali yetu ya kiuchumi, masuala mengine yamekuwa hayafanyiki kama ipasavyo.

Naomba nianze kwenye Idara ya Uchapaji. Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uchapaji kama tunavyofahamu sote kwamba ni Idara ambayo tumekuwa tukiitumia kwa kipindi kirefu katika kuchapisha majalada yetu mbali mbali ya serikali, lakini idara hii tunaweza kusema imekufa kabisa.

Lakini hata hivyo, idara hii imebeba wafanyakazi wenye juhudi, uzoefu pamoja na kupenda taifa lao. Kwa bahati mbaya Mhe. Mwenyekiti naweza kukwambia kwamba wafanyakazi hawa wengi wamevunjika moyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipata bahati pamoja na wenzangu kwenda kutembea kwenye idara hii na tumekuta malalamiko mengi. Kwa bahati nzuri hivi sasa yale malalamiko yao yanatekelezwa, lakini bado yanakwenda taratibu.

Kwa kweli wafanyakazi hao wamekuwa wakifanya kazi zaidi ya muda ambao wamepangiwa, yaani walikuwa wakifanya kazi mpaka usiku na malipo hayapo. Jambo hili liliwasababisha hata kwenda katika redio kwa ajili ya kulalamika. Kwa mfano, wafanyakazi hao mtu mmoja anafanya kazi za watu wawili au watatu.

Kutokana na hali hiyo, naomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Wizara imeshaanza kushughulikia malalamiko yao, basi hili lisiwe kama vile anavyosema Mhe. Ismail Jussa Ladhu, isipokuwa limalizike kwa haraka iwezekanavyo na sio kwamba lifanyiwe kazi na badala yake limalizike kwa haraka iwezekanavyo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nitalizungumzia kuhusu Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni kuhusu suala zima la sherehe zetu za miaka 50. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninazo tafsiri nyingi za sherehe za miaka

50, maana yake sherehe za miaka 50 sio kwamba tunashereheka, isipokuwa ni sherehe za kujipongeza tumepata uhuru wetu pia ni sherehe za kujitathmini tulipofikia, ndio maana ya sherehe za miaka 50.

Mhe. Mwenyekiti, tunajua kwamba Mhe. Waziri wizara yake imejipanga, lakini sisi kujipanga kwake hatutaki iwe kujipanga kwa maneno, isipokuwa tunataka vitendo, yaani kuona kwamba kwa kweli sherehe zile zitasema kuwa Zanzibar imekuwa huru kwa miaka 50. Kwa maana hiyo, sherehe hizo zizungumze wenyewe. *(Makofi)*

Nafikiri binadamu mara nyingi tunakuwa na tabia ya kujitathmini wenyewe, kama mtu hana tabia ya kujitathmini basi ana kasoro, lakini lazima tujitathmini. Sasa kujitathmini kwenyewe ndiko kutakakotusaidia kuweza kuendeleza taifa hili katika kipindi cha miaka 50 yale malengo yetu tumeyafikia vipi.

Mhe. Mwenyekiti, tulifanye hili kwa kurudi chini kwa wananchi. Kwa hivyo, naomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba serikali ifanye kila mbinu kuwahoji wananchi kutaka kujua kuridhika kwao. Kwa kweli hapo ndipo serikali itajua nini cha kufanya na wala isijipangie tu, wananchi wanao uelewa mzuri sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wakati tunazitengeneza sherehe hizi basi lazima serikali irudi kwa wananchi ifanye vipindi maalum vya kuwahoji wananchi mpaka kwenye vijiji, yaani iwahoji rika zote. Kwa mfano, wazee, vijana kwa sababu wote wanayajua Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, nilisikitishwa sana niliwahoji vijana wawili, watatu ambao wanasoma skuli zetu za serikali nikawauliza kwamba skuli asubuhi kila siku kama wanaimba nyimbo ya taifa. Mhe. Mwenyekiti, nasema aibu! Yaani skuli zetu za serikali hazina na wala hawaimbi nyimbo za taifa na watoto wetu hawajui nyimbo ya taifa ya Zanzibar inasikitisha. Hivi tunaona aibu haya Mapinduzi au uhuru wetu tunauonea aibu. *(Makofi)*

Jambo la kushangaza nimemuhoji mtoto mdogo wa *Nursery School* nilimuuliza nyimbo ya taifa ya Zanzibar na ile ya Tanzania anazijua tena hiyo ni *private school*, yaani walimu wake ni wageni.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana katika sherehe hizi za miaka 50 turudi twende katika skuli zetu na wale ndio *generation* ya kesho na tunatakiwa sisi tuwafundishe maana ya Mapinduzi. Vile vile tunatakiwa sisi tuwape elimu, ujasiri wa kuwa Wazanzibari, lakini leo tukitenga baadhi ya mambo tukayaonea haya. Mhe. Mwenyekiti, hii ni kazi ya wizara ya Mhe. Waziri.

Kwa kweli mambo kama haya kwa wenzetu hayajawahi kutokea na badala yake yanatokea hapa tu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, jambo hili lirekebishwe.

Suala la pili nataka kuzungumzia kuhusu ujenzi wa choo. Mhe. Waziri ningekupongeza sana Wizara yako kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuhusu ujenzi wa choo kilichopo pale *Airport* ambacho kitasaidia katika kukamata wahalifu wanaosafirisha dawa za kulevya.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hili tumelifanya bila ya kufanya utafiti, kwa kweli kile choo mimi nataka Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze baada ya kutiwa kile choo kama tayari kimeshaanza kutumika wangapi wameshakamatwa na changamoto zipi zimejitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, choo kile kimejengwa bila ya utafiti, kwa sababu choo kile kimejengwa chini ya sehemu ambayo unaingilia *Airport*. Vile vile pale sijui kitatumika vipi, lakini ni mtihani mkubwa.

Halafu pale hakuna *facilities* nyengine ambazo zitasaidia katika kumtoa yule mtu kule, kwa sababu lazima kwanza mtu aulizwe maswali apekuliwe mpaka ajulikane kwamba kweli anacho hichi kitu na halafu apelekwe chooni ndio *process* ndefu mno. Sasa haya mambo sijui yatafanyika vipi kwa kweli sisi hali hii inatushangaza sana.

Kwa hiyo, naiomba wizara kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, ikae kitako tena na iangalie uwezekano wa choo kile kuweza kutumika vizuri.

Nikiendelea na mchango wangu naomba niipongeze Wizara kwa juhudi zake kubwa alizozifanya za kutuletea amani pale ambapo tulianza kuwa na machafuko katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, sote tuliona kilichotokea katika kipindi kifupi sana. Lakini Mhe. Mwenyekiti na sote tunajua nini kilichotokea na serikali ilichukua hatua, ambavyo sivyo sisi tulifikiria kwamba hatua ile itachukuliwa pale ambapo yale mambo yanapotokea.

Sasa mimi ningeiomba sana serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba tusicheze na amani ya nchi hii. Jambo la msingi ni kuhakikisha kwamba pale ambapo yanapotokea machafuko na vurugu, basi serikali ichukue hatua kali mara moja au tukiweza kulea hawa watu wa vurugu na machafuko hawalali wenzetu. Kwa kweli naipongeza serikali pia naiomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, iwe nyepesi katika kuchukua hatua.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, unazo dakika tano za ziada.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, leo msimamo wangu naona kama ni mkali sana, lakini nina wasi wasi na saa yako sijui kama iko sahihi. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka kuzungumzia kama walivyozungumza wenzangu kidogo tu kuhusu Nyumba za Jeshi la Polisi. Kwa kweli Nyumba za Jeshi la Polisi za kwetu ni aibu na tulikwenda Bara na tukaoneshwa Nyumba za Jeshi la Polisi za wenzetu, basi mtu yeyote atakayetizama baina ya Nyumba za Jeshi la Polisi za Zanzibar na wenzetu kule utaingia unyonge mkubwa sana. Kwa hiyo, hata hizo ambazo tunaambiwa sisi kwamba zimetengenezwa, basi haziwezi kulingana na za kule hata kidogo. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, naomba suala hili kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais jambo hili lishughulikiwe, kwa sababu linatutia unyonge Wazanzibari, kwa nini tuwe na nyumba mbovu za Jeshi la Polisi na wakati nyengine tumeziona ni nzuri. *(Makofi)*

Jambo jengine ambalo nataka nizungumze ni lile ambalo Wajumbe wenzangu ambao tumo ndani ya Kamati moja wamelizungumza ni kuhusu watu wa Paje. Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri tulipofanya ziara kwenda Tanzania Bara tukaonana na uongozi mzima wa Jeshi la Polisi walizungumzia suala la kuanzisha Mfuko wa *Trust Funds*, wamesema kwamba mfuko utawawezesha kuwa na nyumba bora na kuwawezesha polisi katika maeneo mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, nadhani mfuko huu na Zanzibar utafika na wala usiishie Tanganyika tu na Zanzibar ufike.

Vile vile suala hili naomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba alisimamie na aulizie mfuko huu kuwa vipi Zanzibar tuta-*benefit* kwenye mfuko huu. Jambo hili limekuja kwa sababu tulipokwenda Paje tumekutana na watu waliokasirika na wamekasirika kwa sababu wamekataliwa na mwenye Hoteli ya *Crystal Resort* kutumia njia ya asili ambayo wameizoea, na yule mwenye hoteli amefunga geti kabisa na wala hawana njia ya kupita, masikini wanawake ambao wanabeba magunia ya mwani, wanazunguka mpaka wafike kijiji kwao kwa sababu ya raha ya huyu mfadhili.

Mhe. Mwenyekiti, wanawake hawa niliwauliza mimi kwamba wanataka nini baina ya huyu mwekezaji ambaye anatupatia dola na hii njia ambayo nyinyi munapita kila siku na mkaweza kwenda kufanya shughuli zenu kule mbali mbali, huyu anacho kipato analeta serikali. Kwa kweli waliniambia hatutaki, kama ni hivyo na iwe basi.

Halafu huyo amekwenda kujenga Kituo cha Polisi na baadae akabandika kimejengwa na *Crystal Resort*. Mhe. Mwenyekiti, huyo pia ameweza kuonesha nguvu zake kwa kupitia polisi kwamba polisi yeye hawawezi kufanya chochote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niliambiwa na mlinzi wa ile hoteli kwa sababu alikuwa hajui kwamba mimi ni mmoja ya wale waliokwenda basi aliniambia mnahangaika au hawa wanahangaika bure huyu mwenye hoteli akienda huko kwenye serikali yenu atachakachua na mtashindwa nyinyi. Mhe. Mwenyekiti, aliniambia na wala sisahau maneno hayo aliyoniambia na nilikasirika sana na nilitaka kumpiga kibao! Kwa sababu hawezi kunitusi na amelitusi taifa langu, utasema vipi mambo kama hayo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, anataka kuniambia kwamba serikali yetu haina maana, lakini hili ni kwa sababu sisi wenyewe hatuchukui hatua, na laiti angelichukuliwa hatua yule basi wasingeweza kusema maneno yale. Mhe. Mwenyekiti, naogopa siku moja ile hoteli inaweza kuchomwa moto na wananchi na ikawa kesi kubwa zaidi na tukawachukua wananchi wetu tukaenda kuwafunga kumbe vile hawana hatia masikini, isipokuwa wanadai kilicho chao. Kutokana na hali hiyo, ni vyema naomba tuwe waangalifu sana katika hili na wala tusiwakere wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie suala la *DNA machine*. Kwa bahati nzuri Jeshi la Polisi wamesema wako mbioni kuitafuta mashine ya *DNA*, ili kuhakikisha kwamba hizi kesi zinazohusu unyanyasaji wa kijinsia na watoto zinapungua. Lakini Mhe. Mwenyekiti, suala zima haliko tu katika mashine ya *DNA*, isipokuwa lipo katika uelewa wa hawa Polisi wenyewe. Hawa Polisi wenyewe bado elimu yao kuhusu masuala yote ya kijinsia na uharibifu wa watoto ni mdogo mno. Uwezo wao wa kukusanya vithibitisho ni mdogo mno. Mhe. Mwenyekiti kwa haraka haraka kuna kesi ya mtoto mlemavu ambaye alikuwa na msimamo mmoja kumtaja hawezi kuzungumza vizuri lakini tushakwenda kuonana nae kama mara tatu jina la mtu ambaye amemharibu ni hilo hilo hajabadilika hata siku moja. Lakini mtoto yule imekwenda imekwenda na kazaa yule mtoto kaambiwa asubiri mpaka azae kazaa, baada ya kuzaa wakasema inachukuliwa DNA inapelekwa Bara, tukaomba ihimizwe DNA ile ihimizwe kwenda Bara wakatwambia Bara hapana huko Bara kuna watu kama 1000 wanasubiri *result* na huyu itakuwa wa 1001. Kwa hivyo sasa si rahisi kuipata sasa hivi imechukua miezi sita.

Baada ya kuchukua miezi 6 *result* zimekuja sie yule baba yake sie aliyemharibu inasikitisha. Kwa sababu kuna kila aina ya ushahidi unaonesha kwamba kweli kwa sababu mtoto mgonjwa wa akili lakini anafahamu ana kumbukumbu nzuri, pale majirani kuna wengi lakini kwa nini kamtaja huyo huyo mmoja. Mhe. Mwenyekiti nilisimama nikamuuliza IGP nikamwambia kuhusu kesi hii ya mtoto mlemavu akanambia mimi sioni sababu kwa nini kesi hii haikupewa *priority*. Kwa nini hii kesi kutaka uthibitisho wa DNA isifanyiwe haraka, iwe kama kesi za kawaida huyu ni mtoto mlemavu. Mhe. Mwenyekiti suala la unyanyasaji wa kijinsia, unyanyasaji wa watoto litachukua muda mrefu kama hatukujiweka vizuri. Kila mmoja anatakiwa achukue jukumu lake vizuri. Mhe. Waziri ninakuomba sana kwa kweli hili ulisimamie vizuri. Maaskari wetu, mapolisi wetu bado hawajawa na uwezo mzuri tuombe waelimishwe vizuri, madeski yapo lakini bado kesi nyingi zinakosa ushahidi kwa sababu ya uwezo wao wa kukusanya uthibitisho.

Mhe. Mwenyekiti nilikuwa naomba kulizungumzia suala la Maafisa Mawasiliano katika serikali yetu. Mhe. Mwenyekiti mara nyingi sana viongozi wetu wanapokwenda katika maeneo mbali mbali hasa mashambani au kwenye ufunguzi tunawaona Maafisa Mawasiliano kutoka Wizara mbali mbali wanakuwepo. Lakini kwa bahati mbaya maafisa hawa ambao ndio wanaochukua jukukumu kubwa la kuelimisha wananchi tunawasahau katika ziara za viongozi mbali mbali, lakini tunawasahau katika kuwapa elimu, mimi jana nilikuwa Dar es Salaam nimekutana na waandishi wa habari ambao wamepelekwa China kusoma, yule balozi mdogo ni mtu karibu sana wallahi hebu na sisi kuwasaidia waongeze ujuzi. Tunawaacha katika mawizara tunawasahau. Mhe. Waziri hili ni jukumu la Wizara yako waangalie vizuri maafisa wako wa mawasiliano hao ndio wanaunganisha baina ya serikali na wananchi. Wao ndio watakaokuwa na wanawaeleza wananchi nini serikali inafanya. Likiwa zuri watalisema na likiwa baya kwa sababu ni wenu watalipunguza makali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba sasa hivi kwenda Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kidogo na nizungumzie suala zima la mazingira. Mimi kwanza nimpongeze sana Waziri Mhe. Fatma kwa kweli juhudi zake nzuri ambazo amezifanya. Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa naomba bado tuna matatizo katika sheria yetu ya mazingira. Pamoja na utekelezaji wake, tumekuwa tuna sera, tumekuwa tuna sheria ya *chainsaw* ambayo inakataza watu kukata miti ovyo. Lakini hebu tutizame kwa siku miti mingapi inakatwa wangapi wamekamatwa na wangapi wamehukumiwa. Wengi wao wakikamatwa wanapigishwa faini wanatolewa. Kwa hivyo Mheshimiwa juu ya kuwa unafanya kazi nzuri bado una kazi kubwa kuhakikisha kwamba tunailinda miti yetu, tunailinda misitu yetu.

Mhe. Mwenyekiti mimi siku zote huwa nina dukuduku langu kubwa sana kuhusiana na misitu ambayo niliyonayo na ninajua hili halihusiani tu na kukosa mvua ikiwa tutakata miti yote. Lakini kuna viumbe vinavyoishi ndani ya misitu hiyo, Mhe. Waziri tunavikosa misitu yetu sasa hivi haina ndege tuliozoea kuwaona enzi hizo, serikali inafanya jitihada gani? Tunataka wale ndege tuwaone angalau unaweza kukaa mwezi mara moja ukamuona tuseme ukasema umemuona chozi sasa hivi humuoni. Unakaa mwezi unaona aina nyengine ya ndege, unaona tingi manjano sasa hivi humuoni.

Mheshimiwa mimi naiomba Wizara yako ilisimamie hili tunataka ndege wetu warudi, hivi ni vivutio tulivyonavyo Mungu hajatujaalia mengine makubwa, lakini katujaalia vitu *simple* lakini vizuri. Mheshimiwa mimi naomba sana Wizara yako ishughulikie sana kwa makini suala zima la mazingira.

Na la mwisho kabisa Mheshimiwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ni suala zima la zile nyumba zetu za vijana wetu za *Sober House*. Kama sikosei mara ya mwisho tulikubalina hapa kwamba wataanza kusaidiwa vijana

wale. Mheshimiwa naomba ukija hapa uniambie kwamba ni msaada gani uliotoka serikalini kwenda katika zile nyumba ambazo vijana wetu wanaishi kwa ajili ya kuachana na dawa za kulevya. Vijana wale wanahitaji kusaidiwa sana na nia yao wameionesha kuanza, kwa hivyo serikali lazima iwasaidie, hatuna jinsi wale ni vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti la mwisho kabisa itakwenda kwenye Ofisi ya Rais, Mheshimiwa mwenzangu amelisema suala ambalo nilikuwa nataka kulisema na mimi ni suala la madiwani wetu. Madiwani wetu tumewapa vyeo vikubwa na majukumu makubwa lakini mpaka hii leo Mheshimiwa tumekuwa tunawapiga dane dane tunasubiri sera, miaka mitano itapita sera haipo. Mheshimiwa hawa watu ukija ukisikia wenye maeneo ambao wanaweza kuuza wakauza ardhi tusije tukashangaa. Huwezi kumfanyisha mtu kazi ukampa mtu madaraka halafu usimpe chochote hakuna kitu kama hicho, hakuna pahala popote. Ile ndio motisha pekee itakayomfanya asimamie kazi zake vizuri, lakini sisi tumewasahau Mheshimiwa. Mhe. Waziri nafikiri unanisikia.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kuzungumzia kuhusu suala la posho la mazingira magumu. Wenzangu wamezungumzia lakini mimi nataka kuzungumzia suala la posho la mazingira magumu hususan kwa Idara moja maalum ambayo kila siku Idara hiyo tunaitia mdomoni. Mhe. Mwenyekiti kwa bahati mbaya sana na hili jambo tumekuwa tunalizungumza siku nyingi, lakini kila siku ndio yale wanayosema liko mbioni. Mheshimiwa Idara ya Vitambulisho posho hili hawana, Mheshimiwa inasikitisha hawa wanafanya kazi nyeti leo tumewasahau.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusema hayo machache ninakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi niwatake tu wenzangu tuchangie sana ili Waheshimiwa waliokaa kule mbele watusikie na labda kuna siku yote ambayo tunayahitaji wataweza kuyatekeleza.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti mimi nitachukua muda mchache sana nilijizuia sijasali magharibi.

Mhe. Mwenyekiti mimi nataka nianze na ukurasa 9 wa ripoti hii ya Mhe. Mwenyekiti wa Kushughulikia Ofisi ya Viongozi Wakuu. Katika ukurasa wa 9 tunaelezwa hapa Kamati ilikwenda kutembelea watu wa Mtambwe na ilikwenda kule kwa sababu ya ile ripoti ya ufanisi wa sensa kwamba kule mafanikio hayakuwa mazuri sana yaani watu hawakujitokeza sana. Sasa ukiangalia ukurasa wa 10 kuna sababu kwamba wananchi wale walizitoa kwa nini hawakushiriki ipasavyo katika zoezi la sensa.

Sasa ukiziangalia hizi sababu Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mara nyengine unaweza ukafika pahali ukajiuliza kumbe usipom-*treat* vizuri hata mtoto wako basi nae katika namna ya kudai haki zake kwa lugha nyengine anaweza akasusia hata kula siku moja. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti sensa ni kitu cha msingi sana katika nchi, lakini kwa sababu ya *treatment* ambayo kwa kweli wananchi haikuwa ikiwaridhisha walifika pahali wakasusia zoezi la sensa jambo ambalo lilitusikitisha wengi.

Mhe. Mwenyekiti moja katika sababu walizozitoa zilielezwa hapa kifungu (b) anasema wananchi kutopatiwa vitambulisho vya Mzanzibari ingawa huwasilisha vyeti vya kuzaliwa ili wapate vitambulisho hivyo. Mhe. Mwenyekiti hili sasa ni tatizo kubwa katika nchi yetu na katika juhudi za kujaribu kulitatua hivi karibuni tulizungumza na Mhe. Waziri Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tukafuatana nae hasa kutokana na ahadi yake aliyoitoa katika Baraza hili tukenda nae mpaka Pemba, tukatembea nae Wilaya zote. Lengo ni kujaribu kupata ufumbuzi wa tatizo la vitambulisho na Mhe. Mwenyekiti vitambulisho kama sheria ya vitambulisho inavyosema, kwamba kutokuwa na kitambulisho ni kosa tena ni kosa la jinai na unaweza ukafungwa jela kwa kutokuwa na kitambulisho.

Lakini sheria ile bahati mbaya haikueleza mtu anayemzuia mtu yeye afanywe na nini? Maana yake nilidhani kama kuna mtu wa kufungwa ni huyo anayemzuia mtu kupata kitambulisho. Sasa Mhe. Mwenyekiti zoezi lile la Mhe. Waziri tulikwenda nalo katika Wilaya zote 4 kwa ufanisi mkubwa kwa kiasi fulani tuliowaita walikuja, wakaelezwa, na Mhe. Waziri alitoa maagizo kwa kweli mazuri ya msingi kabisa. Tatizo ambalo watu wengi walikuwa wakinung'unika walikuwa ni masheha wakiwazuia kutoa zile barua za kwenda kupata vitambulisho. Waziri akalizungumza kwa nguvu zote na akaagiza kuanzia sasa Sheha si kazi yake kuweza kumu-*assess* mtu kwamba anafaa kwenda kupewa kitambulisho au laa, kazi yake yeye ni kuandika barua ya kumtambua tu kwamba huyu ni mwananchi wa shehia yangu basi na hilo masheha sasa wanalifanya.

Lakini tatizo limetokea upande mwengine Mhe. Mwenyekiti tatizo lililotokea sasa hivi ni vyeti vya kuzaliwa vyote havifai, hata ukienda na cheti cha namna gani hicho ukifika kule karani wa Idara ya Vitambulisho anakwambia cheti hiki ni feki na hakifai na hupati kitambulisho. Mfano mzuri humu ndani ya Baraza yuko Mhe. Salma bahati nzuri siku ile tulipokuwa na kikao na Mhe. Waziri Chake Chake pale alikuja na vyeti viwili vya watoto wake. Vyeti vile hapo kabla alivipeleka Idara ya Vitambulisho wakamwambia havifai sijui vikosa nini, sijui vimekosa nini. Akavichukua Mhe. Salma akaja navyo Unguja akampelekea Waziri wa Katiba na Sheria akamwambia Waziri hebu angalia vyeti vyangu vina kasoro gani nimeambiwa kule vina kasoro. Waziri kwa kadri ya ufahamu wake na kujua kwake sheria, mwanasheria wa siku nyingi yule akakitizama cheti akamwambia hakina tatizo lakini kipeleke kwa Mrajis wa Vizazi na Vifo na yeye akaangalie vyeti vikapelekwa kule na Mrajis akasema vyeti vile havina kasoro yoyote.

Lakini siku ile Mhe. Salma alipokuwa anavionesha watu wa Idara ya Vitambulisho pale pale wakamwambia vyeti vyako vina tatizo sijui hili na hili. Sasa mimi nauliza hivi mtaalamu wa vyeti vya kuzaliwa ni Ofisi ya Vitambulisho au ni Ofisi ya Vizazi na Vifo Mhe. Mwenyekiti. Maana yake inaonekana sasa imekuwa ni kikwazo cha makusudi hata wewe uende na cheti cha namna gani kina kasoro tu. Sasa mimi sikatai kama vyeti feki vipo vinatolewa na hata vikiwepo wa kulaumiwa nani, mimi nimekwenda ofisi ile kutafuta cheti, sasa kama maofisa wa Idara ile wananipa vyeti feki hili ni kosa langu au la kwao. Hilo moja.

Lakini upande wa pili mimi nilikuwa nadhani cheti cha kuzaliwa katika suala zima la kitambulisho Mhe. Mwenyekiti lilikuwa kile cheti cha kuzaliwa kina umuhimu wa kuweza kujua tu umri wa mtu kwa sababu ndani ya cheti cha kuzaliwa, zaidi ule umri wa mtu hakuna kumbukumbu nyengine inayochukuliwa mle ndani ya cheti kutiwa kwenye kitambulisho. Sasa kimefanywa ni kikwazo kikubwa cha watu kukosa ikiwa ile herufi moja Mhe. Mwenyekiti herufi moja tu imetoka kwenye mstari ikakaa juu kidogo na hiyo kwa sababu ya ile mashine yao wanayopigia ni yale ya kizamani herufi zinaruka. Ikiwa ile herufi moja imearuka tu unaambiwa cheti hiki hakifai. Kwani ile herufu ikikaa juu hivi ndio inabadilisha umri wa mtu.

Mhe. Mwenyekiti suala hili tusilidharau litatuletea matatizo makubwa watu wa Mtambwe na si wa Mtambwe hata nilipita Tomondo mimi nakaa Tomondo kule, nilipita Tomondo kule Sheha Kidevu ana Polisi mkononi anawalazimisha watu kuandika sensa hawataki. Mimi nikasikitikasikitika halafu nikamuuliza Sheha kwani kuna nini? Hawataki bwana hawataki. Lakini pale pale kuna watu wanasema huyu tulimuendea atuandikishe anasema hatutambui. Sasa watu unakaa nao jirani zako huwatambui vipi, Mhe. Mwenyekiti hebu tubadilikeni hii nchi haiwezi kuwa na amani kama haina haki. Unajua kutoa haki ni sehemu moja ya kulinda amani ya nchi. Tukifika pahali tunabinya haki za watu wale ni binaadam, binaadam ukimzuia huku yeye atapita huku. Tujitahidini.

Halafu nilipokuwa nasoma huu waraka wa Mhe. Waziri Ofisi ya Rais wa utekelezaji wa yale maagizo ya Kamati kwenye ukurasa wa pili, Mhe. Waziri ameandika hapa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imo katika hatua za mwisho za maandalizi ya kuwasajili wageni baada ya kufanya marekebisho sheria namba 7 ya mwaka 2005 bila shaka ni sheria ya vitambulisho. Halafu akasema hatua hii itaweza kuondosha tatizo la raia wa kigeni kupata kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Sasa mimi hofu yangu iko hapo kwamba kumbe kwa sababu sheria namba 7 tulikuwa hatujairekebisha, ilitoa mwanya kwa wageni kupata vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Na kama hivi ndivyo basi nadhani sasa kuna haja ya daftari la Mzanzibari Mkaazi sasa kufanyiwa mapitio Mhe. Mwenyekiti kama kuna wageni maana kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi ile ni haki ya Mzanzibari pekee. Sasa kama kuna wageni wamepewa mimi nadhani tukaeni kitako lakini daftari tulifanyie mapitio, tuwabaini waliokuwa wameandikwa mle hawastahiki tuwatoe na wabakishwe Wazanzibari watupu.

Wallahi mimi nilikuwa najiuliza sana katika mtu makini mmoja ni Mkurugenzi wa Idara ya Vitambulisho, hivi anakwenda kwendaje mtu mpaka akafika pahali kumpa kitambulisho wakati si mzanzibari inakuwaje. Maana wazanzibari tunajuana kwa sura, tunajuana kwa ubini wetu, tunajuana hata akisema mtu unajua kama huyu mzanzibari tena anatoka Makunduchi. Maalim Haroun akisema mimi ninajua kuwa anatoka Makunduchi. Lakini kuna lugha mtu akisema unajua kama huyu kwa hapa Zanzibar hakuna watu wanaosema hivi, sasa unakwendaje kumpa kitambulisho kama si kwa makusudi Mhe. Mwenyekiti. Ikiwa anatoka Chonga anajulikana anatoka Chonga.

Sasa mimi nadhani kuna haja sasa ya daftari hili Mhe. Mwenyekiti kulikagua tukawabaini walioandikishwa mule wana vitambulisho vya Mzanzibari, maana kumpa mtu Uzanzibari wakati yeye si mzanzibari ni kitu hatari mno. Mhe. Mwenyekiti hivi karibuni *impact* yake itaonekana hapa na ngojeni kidogo mtakapokuja kupiga kura ya maoni

kuamua mustakbali wa nchi yetu tutaona wimbi la watu watakaotuamulia ambao hawakustahiki kutuamulia nchi yetu tutaona wenyewe.

Mhe. Jambo jengine ambalo watu wa Mtambwe walilitaja kwamba ni miongoni mwa mambo waliyoyafanya wasiende kujiandikisha sensa wameeleza hapa Mhe. Mwenyekiti kwamba wananchi kutopatiwa mikopo ya AK na JK na hii nisingeitaja hapa, lakini juzi nilipigiwa simu na mtu kutoka Chake Chake akaninung'unikia sana kuhusu ombi lake alilolipeleka linafika mwaka huu anasema bado liko juu ya meza mpaka leo halijafikiriwa. Akawahi kunambia hebu mtafute Waziri husika umuulize kulikoni nimekosa nini mimi mpaka leo sijapatiwa mkopo wa AK na JK. Sasa Mwenyekiti haya yapo na nadhani Waziri husika hapa yupo naomba sana baadae tuonane nimwambie ni nani ambaye kwa kweli ananisikitikia hili. Maana mtu kama huyu asipopewa na yeye ni mnyonge. Na alikwisha *target* nikipata huo mkopo mimi naweza nikafanya hivi na hivi nikawa najiendesha kwenye maisha yangu.

Sasa usipompa keshokutwa anaweza akasusia hata kupiga kura asiende, jambo ambalo ni hatari sana. Kwa hivyo mimi nilikuwa naomba tu bwana watu haki zao tujitahidi tuwape ni sehemu ya kulinda amani, ni sehemu ya ufanisi wa shughuli zetu za kila siku.

Mhe. Mwenyekiti nikitoka kwenye Ofisi ya Rais sasa niende kwenye Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na katika hili naomba nigusie jambo moja tu. Mhe. Mwenyekiti ukisoma ukurasa wa 14 katika maoni na ushauri wa Kamati kifungu namba 5 kinasema uharibifu wa mazingira bado unaendelea. Na cha kusikitisha baadhi ya masheha wanachangia uharibifu huo. Sasa Mhe. Mwenyekiti ikiwa hata sheha nae anachangia mimi nadhani huo sasa ni mtihani.

Mhe. Mwenyekiti mazingira yetu yana maadui wengi; kuna makampuni ya ujenzi ambao wao uchafuzi wao wa mazingira ni kuchimba pengine kifusi au kuchimba mawe kwa ajili ya shughuli zao za barabara. Hapa sheha atakuwa hahusiki kwa sababu ni jambo kubwa zaidi. Lakini kuna adui namba mbili ni wawekezaji, wawekezaji hawa hasa katika mahoteli ya kitalii wao wanachafua kwenye fukwe za bahari, wanajenga mpaka mule ambamo ni sehemu za maji. Sasa unapojenga mle maana yake nini unazuia maji, maji ya bahari kuzuiwa hayakubali yatatafuta sehemu nyengine yatapenya.

Mara moja nilikwenda Uroa kwa rafiki yangu, nilipofika pale Uroa nikakuta kwenye ile chochoro kati ya nyumba na nyumba maji ya bahari yanapita pale, mimi nikamwambia yule rafiki yangu mambo haya yanakuwaje sasa kuwa maji ya bahari yanakuja mpaka kwenye majumba yenu. Akanambia bwana hivi ndivyo tulivyo sisi, akanionesha kule kwenye mawimbi ya bahari akanambia huu mji wetu ulikuwa kule. Lakini maji yamekuja sisi tunarudi nyuma kila yakija tunarudi nyuma, mpaka tupo huku sasa hivi. Kule kulikokuwa na mji sasa hivi ni baharini. Sasa haya ni mambo ya kitaalamu lakini kwa kweli maji ya bahari hayakubali kunyang'anywa eneo lake. Sasa hawa wanaojaribu kujenga na sisi tukawavumilia kwa sababu ni watalii wanaleta pesa sawa wanasaidia uchumi wa nchi, lakini mimi nadhani kufuata sheria na hasa kwa usalama wa visiwa vyetu vidogo nadhani jambo la msingi zaidi. Kwa hivyo, wawekezaji wa mahoteli mimi naungana na kamati kwamba lazima serikali iwe macho sana wasituharibie mazingira yetu ya baharini.

Adui wa tatu wa mazingira Mhe. Mwenyekiti, ni sisi wananchi wenyewe na hapa sheha sasa ndiye anaehusika. Mhe. Mwenyekiti, kule kwetu Pujini kulikuwa na ekari nyingi sana za mkoko, *Wallahi* ukienda ulikuwa unapenda kabisa. Nimekaa kiasi miaka mitatu minne sijatembelea kule maeneo ya pwani pwani, hivi karibuni nilikwenda kutembelea kwa kweli niliona machozi yananitoka mkoko wote umekatwa watu wanapiga chokaa. Sasa katika utafiti wangu nikajaribu kuuliza uliza watu tena wanafanya mpaka jiwe haya serikali haimuoni?

Mhe. Mwenyekiti, Diwani wangu akanambia kwa kweli serikali haitaki kumchukulia hatua huyu mtu, haya kwa sababu gani? Kwa sababu tayari ripoti wanazo watu wa misitu, watu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wanajua, lakini bado mtu yule anaendelea kuachiliwa sasa hivi ni tishio maji ya bahari yanaanza kupanda juu. Wataalamu wanasema ile mikoko Mwenyezi Mungu kaijaalia ina hekima kubwa sana, moja katika hekima zake ni kuzuwia ule upepo mkali wa chumvi usipande juu, sasa unapoikata maana yake upepo ule hauna kizuizi unakuja juu unauwa na miti mingine na nimeona athari kuna baadhi ya miembe imeanza kukauka kule kwa sababu ya upepo wa chumvi.

Sasa naomba sana Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Unajua uami siku zote mimi huwa nagombana nao, huu uami uami utatudhuru sana, kwamba unashindwa kumchukulia mtu hatua kwa sababu yuko hivi na hivi, hapana

jamani tusipochukuliana hatua nchi yetu hii itapoteza haiba yake. Nadhani kama kuna mtu kafanya kosa ni vyema achukuliwe hatua, nilikwenda mpaka Idara ya Misitu nikawaambia vipi, wakasema aah, bwana yule akija anasema hivi na hivi, sasa anasema hivi mmuachie kwa sababu anasema hivi? Msifanye bwana, mimi jamaa yangu lakini kwa anavyochafua mazingira sikubaliani naye.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka niligusie kidogo ni kuhusu Mahkama. Mahkama zetu ni chombo muhimu sana cha kutoa haki na mimi mara nyingi huwa nasema ikiwa Mahkama zitatumiwa vizuri basi zinaweza kulinda amani na utulivu wan chi na kama Mahkama hazitatumika vizuri basi zinaweza zikachafua amani na usalama wa wananchi na mali zao.

Mhe. Mwenyekiti, imekuwa ni mtindo sasa hivi Mahkama zetu sijui naogopa mimi kusema kwa sababu ni muhimili mwengine, lakini kama kwamba hawako *serious* katika kulinda haki za watu, wamefanya tamaa nyingi. Mara moja niliwahi kusema hapa na hata hili Waziri wa Katiba na Sheria atakuwa shahidi wangu na hata Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Kusini Pemba atakuwa shahidi wangu, kuna uhalifu unafanyika katika jimbo langu. Kuna watu wanauza bangi na bahati mbaya wanakamatwa, wanapelekwa polisi, wanapelekwa Mahakamani lakini hawajawahi kuwekwa hata ndani kwa wiki mbili, hata ile kuzuwiwa rumande hawajawahi. Sasa matokeo yake ile biashara inakiwa inaendelea tu kule tukafika pahala wale wanaonunua ile bidhaa wakishavuta bangi akili zao zinachafuka, zikishachafuka wanafanya uhalifu mwengine zaidi, wanaiba ng'ombe wa watu, wanauwa.
Mhe. Mwenyekiti, kuna mmoja siku hiyo kenda kawakamata ng'ombe masikini ya Mungu watano kawakata miguu wote, akachukua punda akampiga mashoka akamuuwa ah, sasa punga kakukosa nini wewe yote ni sababu ya bangi na polisi inajua.

Siku moja wananchi walitoka wakamwendea RCO mwenyewe wakamwambia bwana ni wewe unayesababisha tatizo hili, wakamueleza kwa ukali akasema sasa situmi askari mdogo nitakuja mwenyewe. RCO akaja akamkamata muuza bangi ana ndoo nzima ya bangi akenda akampeleka Mahkamani kasimama mwenyewe RCO kutoa ushahidi, siku zote mimi huwa nasema uongo wa askari si kweli ya raia, pamoja na *principle* hiyo kule Mahkamani lakini muuza bangi yule hakufungwa na karudi na *speed* kubwa na yakatokea yaliyotokea. Mimi nikamwambia Mhe. Waziri wananchi sasa wamepoteza imani na Jeshi la Polisi, wamepoteza imani na Mahkama. Mwananchi akifika hapo anaweza kufanya jambo baya zaidi.

Mhe. Waziri akachukua hatua akenda akazungumza na Mahkama lakini hakuna kilichofanyika. Sasa kilichotokea nini, kilichotokea wananchi siku moja walihukumia mikono yao yule yule mhalifu kwa sababu si siri anajulikana, yeye mwenyewe kama keshaweka vitu vyake mle hajali chochote. Kwa hivyo, wakamuotea wakampiga vibaya sana, inasemekana wakampotezea mpaka Jicho Lake. Sasa hapo amani imevunjika kwa sababu gani, Mahkama haikutoa haki.

Nilikuwa naomba sana Mahkama zetu ziwe *serious* kosa likitendeka lichukuliwe hatua. Kuna makosa mengine hayavumiliki huwezi kumvumilia mvuta bangi kwa sababu kumvumilia yeye ni kuzalisha vichaa katika mitaa, kukishakuwa na vichaa wengi hakukaliki tena mitaani, naomba sana Mahkama ziwe *serious*.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwisho ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na hapa nazungumzia Tume ya Uchaguzi. Katika Tume ya Uchaguzi Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia jimboni kwangu, unajua mazingira yetu sasa yamebadilika zile siasa chafu, zogo na ghasia mhe. Mwenyekiti, toka tuanze GNU nadhani ni wakati wa kuzizika sasa. Kule jimboni kwangu kulitokea tatizo kubwa la kupandikiza wapigakura na hii ilifanywa kwa sababu ya vikosi kuna vikosi vitatu kule sasa hivi; kuna JKU, kuna KVZ na kuna kikosi cha KMKM Tundauwa.

Mhe. Mwenyekiti, vikosi hivi vilitumika kuongeza wapiga kura katika jimbo langu hawapungui elfu moja na zaidi hivi, na nilikuwa mkali sana lakini hatimaye dola ni dola wakanizidi nguvu mpaka leo wako. Nilikuwa naiomba sana Tume ya Uchaguzi wale watu sasa wawaondoe siasa chafu zimekwisha, wabakie wale wale wapiga kura halali wa Jimbo la Chonga.

Mhe. Mwenyekiti, kuna JKU mmoja alipelekwa kule aliandikishwa lakini alikuwa si kambi yake ile kambi yake ilikuwa Wawi sijui huko, akapelekwa kule sasa keshastaafu lakini bado anakuja akipiga kura Pujini na mimi huwa namtania sana nikifika humwambia hee, haomba kura yako, ananambia wewe sikupi kura yangu hata siku moja, siku hizi nikimkuta pale Chake Chake ni mlemavu humwambia mara hii nikikuona Pujini nakutia kwenye gunia nakwenda kukutia pwani, mfupi hivi maana yake ni mlemavu Mhe. Mohamed Aboud anamjua ni rafiki yake sana.

Naomba sana Mhe. Mwenyekiti, hebu tumalizeni haya matatizo sasa, wale waliokuwa si wapiga kura kule watoeni na watu nao wapate kupumua.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, mimi ripoti hii ya Ofisi za Viongozi Wakuu naiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia machache kwenye Ripoti hii ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Mhe. Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuumba waja wake na kutufikisha katika ukumbi huu leo tukiwa na afya njema. Pia niwashukuru mawaziri wote watatu kwa jinsi walivyotoa taarifa zao za utekelezaji wa kazi katika ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi.

Pia naomba nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Wenyeviti kwa umahiri wake mkubwa wa kufanya kazi hii kwa muda wote wa miaka miwili na nusu katiaka kusimamia viongozi wakuu wa kitaifa katika wizara hizi tatu muhimu na wizara mama. Sasa nianze moja kwa moja na kuingia katika ripoti yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze na Ripoti katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nakuomba Mhe. Mwenyekiti, univumilie usifikirie kama ninarudia hapa sio kurudia, ukiona pahala panarudiwa ni pahala ambapo panakera panatakiwa parekebishwe haraka.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwenye umuhimu wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Mhe. Mwenyekiti, vitambulisho vya Mzanzibari ni sehemu ya maisha ya mwanadamu Mzanzibari kwa sababu kila kitu kinatakiwa uwe na kitambulisho na waziri katika ripoti yake amesema kwamba amefanya juhudi kubwa za kutoa elimu zaidi juu ya umuhimu wa vitambulivyo hivi katika vyombo vya habari kama redio, TV na sehemu nyenginezo. Lakini nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba bado suala la vitambulisho ni tatizo, mbali na wale watu ambao wanatakiwa waende wakale kiapo kwa sababu ya umri wao, mimi wale naachana nao, lakini nataka hawa vijana wetu wadogo wadogo.

Kwa sababu kitambulisho cha Mzanzibari ukikikosa unaweza ukashtakiwa kwa mujibu wa sheria na kukipata ni tatizo, basi nataka nimuombe Mhe. Waziri kwa hekima zake na uwezo wake mkubwa alionao atumie busara zake. Kwa sababu vijana wetu wengi tunawaona katika skuli wanaomaliza *Form* IV, kwa sababu awamu ya mwanzo baada ya kupatikana huumfumo wa kutafuta vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi basi watu walipita skulini wakachukua jitihada za kuwaandikisha watu na wakapewa pale skuli. Kaw hivyo, naona haiwezekani mtu amalize skuli mpaka *Form* IV iwe bado tu hajafikia umri wa kupewa kitambulisho. Wengine vyeti vya kuzaliwa wanavyo lakini ni usumbufu mkubwa hali zetu za maisha tunazijua Mhe. Mwenyekiti, mtu kutoka kila siku kwenda mjini ukijitizama wewe umtizame na mwenzako aliyeko chini yako.

Sasa namuomba Mhe. Waziri achukua jitihada angalau na busara zake apitie maskuli achukue wale vijana wetu waliiokuwa tayari wana vyeti na waliokuwa hawana watapewa elimu zaidi ya kutafutiwa, lakini angalau kuwapunguzia usumbufu hawa watu kupata haki zao za msingi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nataka niingie kwenye mageuzi ya Serikali za Mitaa, kwenye mageuzi haya naomba nimpongeze Mhe. Waziri keshalizungumza sana na sasa hivi kilichobakia ni sera. Lakini nataka niseme hii sera imeshakaa muda mrefu sana, sasa katika hotuba yake hii Mhe. Waziri kuna eneo kasema anasubiri uajiri kwa watumishi wapya katika Mabaraza na Halmashauri za Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi yoyote yenye kuingiiza na kukusanya mapato inatakiwa ienziwe na iheshimiwe. Taasisi hii inakusanya mapato mengi, sasa tukikaa katika kusubiri uajiri wa watumishi wapya katika Mabaraza na Halmashauri, lazima tuwe makini katika kuajiri watu waaminifu, wanaoweza kukusanya ikawa makusanyo yale yanaingia katika Mfuko ule isiwe makusanyo yale yanaingia katika mifuko yao ya suruali na matumbo yao.

Mhe. Mwenyekiti, nalisema hili kwa sababu ya ushahidi, tumeshapita, tumeshazungumza katika Halmashauru na Mabaraza ya mimi yopt ya Unguja na Pemba, tulililoliona watu wanakusanya sana lakini baadhi yao sisemi wote, baadhi yao wanakusanya lakini makusanyo yote hayaonekani, baada ya watu kuhoji na kudai tumeingiza nini kilichoingizwa hakionekani kinaingizwa ndani ya matumbo ya watu. Kwa hivyo, uwe makini sana katika hili na katika kutafuta uajiri basi uajiri watu waaminifu atakaotuletea maslahi katika serikali zetu za mikaa, kwani serikali

za wenzetu za Mitaa za Bara zinajenda mpaka maskuli, zinajenga vituo vya afya kwa sababu ya ukusanyaji na umakini wao na kulinda kile kinachokusanywa. Kaw hivyo, na sisi naomba Mhe. Waziri uwe katika hali kama hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nataka niingie katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika uchakavu wa mitambo ya Kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Mhe. Mwenyekiti, mbali na uchakavu wa mitambo katika kiwanda kile lile jingo lenyewe pia pale lilipo ni aibu na ni hatari, kipindi cha mvua mfanyakazi akiweko ndani hatoki nje na aliyeko nje pia haingii ndani. Kwa sababu pale panakuwa kama bahari panahitaji boti ya kuvushia watu kuingia ndani na kutoka nje.

Halafu pia kuna tatizo jengine, kuna taasisi za serikali zinazodaiwa na kiwanda kihi hazilipi sasa kiwanda hiki kitakuwa hakiendi mbele. Sasa wao wanatakiwa walipe zile taasisi za serikali zinazodaiwa na kiwanda ili kile kiwanda kipate kujiendesha, kile kiwanda ni chetu wenyewe, kinafanya kazi vizuri, kinaingiza lakini bahati mbaya sana kinachoingizwa hakionekani kwa sababu kuna baadhi ya taasisi za serikali hazilipi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakuja ukurasa mwengine wanne katika Ofisi hiyo hiyo ya Makamu wa Pili wa Rais kwenye umuhimu wa kujenga Vituo vya Polisi katika maeneo muhimu kama vile *Airport* na Bandarini. Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme katika kujenga vituo vya polisi kuna maeneo mengine yanatakiwa yapewe kipaumbele kama *Airport* panatakiwa pawe na kituo cha polisi pamoja na Bandarini.

Mhe. Mwenyekiti, jambo zuri huigwa Zanzibar ni nchi na ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nafikiri nyote mnaona tukipita pale bandarini Dar es Salaam kuja zetu Unguja pale kuna mashine la kuchunguzia wale wanaoingia kama wanaingia na vitu vilivyokuwa havitakiwi kuingia, lakini kwa bahati mbaya sana Unguja mashine hiyo hapana. Cha kusikitisha zaidi nalisema hili kwa ushahidi kwa jambo liliopo na akilitaka Mhe. Waziri basi mimi nitamwita huyo kijana aje. Alitoka kijana wa kike Dar es Salaam keshaangaliwa kule kaja zake Unguja kashuka kwenye boti anataka kubadilisha boti jengine kuelekea Pemba kwenye msiba, kilichomkuta pale Mhe. Mwenyekiti, hata kukisema ni aibu.

Mtoto yule wa kike aliambiwa pale kwamba watu wana wasi wasi na yeye, akauliza mna wasi wasi na nini? Akaambiwa ingia ndani, akaingizwa ndani mna mwanamke na mwanamme akaambiwa avue nguo mbele yao, akasema siwezi kuvua nguo penye mwanamme lazima mwanamme atoke, baada ya mzozano mkubwa yule mwanamme akatoka akabakia mwanamke askari alivuliwa nguo kama alivyozaliwa, baada ya kuvuliwa wakamsachi hawakumuona na kitu wakamwambia ainame kama anayerukuu kutaka kusali, akaingama wakati hana nguo kama alivyozaliwa na hawakumuona na kitu chochote. Lakini cha kusikitisha zaidi kama walikuwa na kitu wanataka kutafuta ndani ya *handbag* za wanawake kuna vipochi na mambo mengine, ndani ya *handbag* walitizama juu juu tu kwenye kipochi hawakutizama. Sasa walikuwa na tatizo gani na hawakumuona na kitu chochyote wakamuachilia pale aibu mpaka jamaa zake walikuwa wanataka kuchelewa kwenda kwenye msiba wanalizana pale nje mama yake akapiga kelele kama aliyechanganyikiwa ndio wakamtoa wakamuachia.

Sasa hii si haki kama kuna mtu anatakiwa asachiwe Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria na wao waweke ile mashine pale iwatizame watu. Mbali na hilo kama ni kusachiwa wasachiwe watu wote wanaopita kwa nini asachiwe peke yake katika hali kama ile. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kuwa na vituo katika taasisi muhimu kama zile ni muhimu na lipewe kipaumbele.

Mhe. Mwenyekiti, katika ofisi hiyo hiyo na kuhusiana na suala hilo hilo la kuwa na vituo kwenye maeneo muhimu kuna changamoto hapa katika utekelezaji wa miradi hiyo ya kujenga hivyo vituo *airport*. Kuna changamoto ya tano Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu niisome.

“Idara ya Polisi ina kitengo kinachoshughulikia na ukamataji wa madawa ya kulevya. Hata hivyo, kitengo hiki hakina usafiri na kwa kipindi cha miaka mitatu Jeshi la Polisi halikuwa na lengo la kununua gari kwa vitengo vyake na vituo, ijapokuwa jeshi hilo lilinunua gari katika vipindi vya uchaguzi kwa kila wilaya. Kwa upande mwengine Jeshi la Polisi la Zanzibar lina vitendea kazi vilivyochakaa ambavyo hutumika kwa Jeshi la Polisi Zanzibar kwa ajili ya ulinzi na usalama. Jeshi hilo tayari limeshafikisha suala hilo katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais lakini bado halijapatiwa majibu”.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo, hiki ni kitengo maalum kinachojihusisha na ukamataji wa madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya ni adui wa nchi yetu, sasa kitengo kama hiki kinaomba usafiri au kinaomba vitendea kazi kwa

ajili ya kukamata hayo madawa ya kulevya hakina, lakini yamepatikana magari kununuliwa kwa ajili ya uchaguzi. Mhe. Mwenyekiti hawa vijana wetu wote wakishaathirika na madawa haya huo uchaguzi nani atayechagua kuchagua hao viongozi wetu wakuu wa nchi hii ili nchi hii ikenda vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo pahali ambapo pana umuhimu wa kufanywa kitu kifanywe, kipewe kipaumbele japokuwa nchi yetu inaambiwa bado ni masikini, bado uchumi haujakua, lakini katika mambo mengine kama hayo ya kuzuia madawa ya kulevya basi ni mtihani Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwenye Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Katika ofisi hii kwanza nataka nimpe pongezi za dhati Mhe. Waziri kwa kutokomeza mifuko ya plastiki, hongera sana. Lakini juu ya pongezi hizo nataka nimwambie Mhe. Waziri ana kazi kubwa, nzito na ngumu ya kuingizwa bidhaa chakavu zisizo kiwango ndani ya nchi yetu. Hilo bado ni tatizo na ni tatizo sugu linatakiwa kufanyiwa mipango ya dhati kabisa, kwa sababu Zanzibar imeonekana ni jaa la kutupwa vitu vichakavu, bado vyakula vibovu vinaletwa na hali vinapigwa karantini visiingizwe lakini bado vinaingizwa, bado mambo mabaya mabaya kama magodoro mabovu yanaingizwa na mafriji. Hili Mhe. Mwenyekiti, bado waziri litakuwa ni gumu kwake inabidi ajipange kisawasawa katika kulitekeleza hili.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, kuna changamoto nyengine hapa katika ofisi hii aliyoisoma mwenyewe katika kitabu hiki cha ripoti kuwa bado tatizo la uingizwaji na utumiaji wa madawa ya kulevya Zanzibar linazidi kwa kasi baada ya kupungua. Sasa hapa ndio pale patapoonekana ule umuhimu wa kujengwa vile vituo vya polisi katika yale maeneo muhimu.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, dawa za kulevya hazishuki kutoka mbinguni dawa za kulevya zinapitishwa *airport* na bandarini, halafu wale wanaoleta hasa kutoka huko kuzileta hapa Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha hawaathiriki wanaoathirika ni vijana wetu wadogo wadogo, watoto wote ukiwaona wanasinzia na hawana usingizi ni kwa sababu ya madawa ya kulevya, tutapoteza nguvu kazi za taifa Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, ninaiomba sana serikali kuwachukulia hatua wale vigogo wanaoleta dawa zile hapa tusioneane haya, tukioneana haya hii nchi itapoteza, ishapoteza na itazidi kupoteza.

Mhe. Mwenyekiti katika hili la madawa ya kulevya naona hata sijui niseme nini kwa sababu serikali inalijua hili na inaliona na hizo dawa zinaletwa tena na watu wakubwa. Juzi nilisikia taarifa kwenye ZBC kuna mtu kakamatwa na kete ngapi sijui za bangi kutoka Tanga kuja Pemba, hivi kwa nini wengine wasikamatwe na zinaletwa hapa hapa kwa makontena. Mhe. Mwenyekiti, hilo ni tatizo tena ni tatizo kubwa ambalo linatakiwa lifanyiwe dawa kubwa lakini kama si hivyo vijana wetu wote tutakuwa tumewatoa kafara na Mwenyezi Mungu hatotusamehe katika hilo. Naiomba ofisi inayohusika na madawa ya kulevya na hili si la ofisi moja, ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Ofisi nyengine zote zinazohusika kama ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa sababu zinaletwa katika vyombo bandari bubu zipo lazima tushirikiane katika hili jamani kuiokoa nchi yetu, wananchi wetu pamoja na vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia mana naona ushaanza kuniwashia taa niendelee kumpa pongezi tena Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa awe na msimamo madhubuti wa kufanya kazi katika nchi yake kusimamia yale mazuri yote. Ahsante mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia machache katika Ripoti hii ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Kwanza nimshukuru Mwenyekiti wa kamati hii kwa kuwasilisha ripoti hii kwa uzuri ambayo alichukua kama masaa mawili kuisoma na tukaielewa na kuanza kuichangia.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza na ripoti hii niende ukurasa nambari mbili kwa kuanza na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambayo kwa kuitizama kuwa ofisi hii ina majukumu mazito na idara zake ni nyeti kabisa na zina changamoto nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ina idara ambayo ni muhimu na ni idara ya faragha ya Makamu wa Pili wa Rais. Vile vile kuna Idara ya Maafa ambayo nayo ina majukumu mazito. Vile vile kuna Tume ya Uchaguzi nayo ina majukumu mazito pia na Baraza la Wawakilishi ambapo ni sisi Wawakilishi wa wananchi pia

tumo katika ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa kweli changamoto kama ilivyoelezwa na kamati kwamba kuna changamoto ambazo zimejitokeza.

Kamati ilieleza changamoto zifuatazo ambazo ofisi kwa ujumla imezikabili katika utekelezaji wa kazi zake. Kwanza ni uhaba wa wataalamu wa fani muhimu katika Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, Idara ya Sera, Mipango na Utafiti, Idara ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na idara nyenginezo. Kwa kweli idara hizi zote ni muhimu na bila ya kuwa na wataalamu wa kutosha basi itakuwa ni changamoto kama ilivyoeleza kamati.

Uhaba wa usafiri, uchakavu wa magari kwa upande wa Unguja, Pemba na Dar es Salaam. Ni kweli kwamba uchakavu wa magari unaleta changamoto

Uhaba wa usafiri, uchakavu wa magari kwa upande wa Unguja, Pemba na Dar es Salaam. Ni kweli kwamba uchakavu wa magari unaleta changamoto vile vile na kwa mtazamo kwamba magari ni moja ya *assets* ambayo ni changamoto kubwa. Magari na hasa ya serikali yanakuwa muda mrefu magari ya serikali yanajitokeza kwamba yanakuwa hayana uangalifu.

Mimi niseme Mhe. Mwenyekiti, kwa hili kwa kweli na mimi linanisikitisha kuona kwamba idara hizi zinachangamoto kama hizi hapa. Vile vile kuna uchakavu wa mitambo ya Mpigaji Chapa. Tunajua kwamba kiwanda chetu cha serikali hii inategemea kiwanda hiki. Lakini kwa kweli mpaka sasa hivi bado hakijaenda na wakati hasa huu wakati ambao tunakwenda na mitambo ya digital. Kwa kweli sisi Zanzibar tutokane ni sehemu ya ulimwengu ni lazima twende na wakati. Kama ofisi hii bado ipo nyuma na haijaweza kutumia mitambo ya kisasa, kwa kweli tutashindwa kufanya kazi zetu kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna umuhimu wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupatiwa usafiri wa kutosha katika ofisi zake kama nilivyosema na hasa huko Dar es Salaam ilivyoelezewa na kamati. Lakini vile vile kutokana na utekelezaji usioridhisha kwa taarifa za kamati za kudumu na kamati teule za Baraza, kamati inaitakia serikali ifanyie kazi ili kupunguza kero katika jamii ili. Hili ni suala la msingi kabisa kwa sababu kamati hizi zinafanya kazi kubwa na vile vile tunatumia fedha nyingi ambazo kwa kamati kuzifanyia kazi kuchunguza mambo mbali mbali. Kwa kuwa vile vile Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na tunakabiliwa na sherehe za miaka 50 na mimi niungane na wenzangu kuona kwamba kuna haja ya kufanya sherehe za aina yake kwenye miaka hiyo. Ni lazima tuthmini bila ya kutathmini miaka hii 50 mafanikio gani ambayo tumeyapata na serikali yetu yale ambayo mengi tumeyafanya basi ni lazima, hapa tuthmini yale yote ambayo tumeyafanya.

Mhe. Mwenyekiti, nikenda katika ukurasa wa 7 na niende kwenye Jeshi la Kujenga Taifa kwamba kamati ilikwenda ikaona na kutembelea ofisi ya JKT ambayo imefanya mafanikio mbali mbali. Sisi hapa tuna vikosi vyetu vya KVZ, JKU. Kwa hivyo ningeomba vikosi hivi vya Zanzibar navyo vikaenda Tanzania Bara au kwa wenzetu JKT ili kuona yale mafanikio ambayo wanayapata, si vibaya kuiga ili kuleta mafanikio ya vikosi vyetu navyo vikapata mafanikio.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimeona kwamba kuna matatizo ya nyumba za Polisi. Kwa kweli nimeona vile vile kuna matatizo ya utunzaji wa nyumba na kwa kweli hili ni tatizo, kwa sababu watu wanasema, “Kitunze kidumu”. Ni kwa nini Mhe. Mwenyekiti, huwa ninajiuliza kwamba kunakuwa na vitu vichakavu ambavyo na kwa sababu pesa kwenye bajeti kama sisi Wawakilishi hapa tunapitisha vifungu mbali mbali katika bajeti za mafungu mbali mbali, lakini kwa nini kwamba kunakuwa hakuna utunzaji wa vifaa vile. Kwa sababu sasa hivi tuna ukaguzi mpya kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu anakuwa anakagua mpaka ile hali ya utunzaji wa vitu mbali mbali, kama ni majengo, magari. Kwa hivyo mimi ningependa sana ili twende na uhifadhi wa hivi vifaa basi ni vizuri tukavifanyia ukarabati wa mara kwa mara, kwani watu wanasema kwamba usipoziba ufa utajenga ukuta. Hivyo Mhe. Mwenyekiti, ni lazima vitu hivi tuvitunze kwa uzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikenda kwenye Ofisi ya hii hii ya Makamu wa Pili wa Rais. Nimeona agizo lililotoka la ujenzi wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi Pemba. Ningekuwa na swali jengine ambalo na mimi nina hamu nalo niliulize, kwa sababu tuna ofisi mbali ya hili ambalo nimeliona hapa lakini kuna swali jengine ambalo ningependa labda kwenye Ofisi yetu ya Baraza la Wawakilishi Pemba angalau siku moja kikao hiki tukafanya kule. Lakini kwa kweli mpaka sasa hivi hakujakuwa na ubora huo wa kutengenezwa na tukafanya vikao hivi katika ukumbi wetu wa Baraza la Wawakilishi liliopo pale Wete Pemba. Kwa hivyo ningependa suala hili nilitoe hapa ili tuweze kuuboresha ule ukumbi wetu wa Baraza la Wawakilishi Pemba na tuweze kwenda kufanya vikao vyetu pale.

Mhe. Mwenyekiti, nikenda na hapa Baraza la Wawakilishi. Hapa ofisini kwetu kwa kweli vyoo haviridhishi. Kwa kweli na hasa kule juu ndio kabisa. Kwa hivyo jengo letu ni zuri lakini bado vyoo vyake haviridhishi, kuna tatizo hilo. Hivyo ningependa vile vile Mhe. Mwenyekiti, kupitia Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, hili suala ikaliona na ikalishughulikia.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, kwanza nimshukuru Waziri mwenye jina kama langu Mhe. Fatma Fereji na niseme kwamba yupo *committed* kweli kweli ni mtu ambaye anapenda na nimpongeze sana kwa kupewa yeye ni mwanamke jasiri.

Ni mtu anayejiamini na vile vile nimshukuru kwa kusimamia mpaka sasa hivi mifuko ya plastiki imepotea kabisa kabisa. Kwa hivyo nimshukuru sana kwa kulishughulikia hili lakini niende katika uchafuzi wa mazingira. Kuna agizo ambalo katika ripoti yake niliona kuna sehemu hii karatasi imenipotea sasa hivi hapa lakini kuna sehemu kwamba alitakiwa shimo la Bumbwini kwamba lifukiwe lakini akasema kwamba yeye Wizara ya Mawasiliano ndio wanashughulikia hilo suala, lakini kama yeye anayeshughulikia na mazingira basi ningependa kwamba akajitahidi kwamba shimbo hilo likafukiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo niende Ofisi wa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa kweli na yeye nimpongeze kwa yote ambayo ameyaleta lakini vile vile wizara hii inaendelea na utekelezaji wa mageuzi wa serikali za mitaa. Miongoni mwa mambo ambayo yanayopewa kipa umbele katika serikali za mitaa ni kuwa na watumishi wa kutosha wenye ujuzi kwa mwaka 2012/2013 na amesema kwamba watumishi 26 wataajiriwa kwenye fani ya sheria, mipango na utumishi, ununuzi, wahandishi majengo na wakusanyaji mapato.

Mimi hili nimpongeze sana kwa kulizungumza hapa na akatoa kwamba akianzisha hii serikali za mitaa ni lazima kuwepo na watu waliokuwa na ujuzi na kuendesha hizo serikali za mitaa. Vile vile Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri nimpongeze amesema hapa katika kutekeleza sheria Na. 9 ya 2005 ofisi yake imeanzisha Bodi ya Zabuni na vitengo vya *procurement* karibu katika idara zote kwenye ukaguzi wa ndani, zinafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria na vile vile sambamba na hilo daktari la kuhifadhia mali ambalo ni kitu muhimu bila ya kuhifadhi kuzijua mali zako ni zipi...

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tumsikilize mheshimiwa ambaye anachangia.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Kwa kweli nimpongeze kwa sababu bila ya kuwa na daftari la kuhifadhia mali inakuwa ni tatizo.

Vile vile amesema kwamba tayari mali zimeshaorodheshwa, nimshukuru kwa hilo na hakuna haliwezi kufanyika. Mimi niseme niwapongeze mawaziri kwa haya yote waliyoyafanya kwani wanatekeleza kwa kiasi fulani isipokuwa kuna mambo ambayo yatakuwa yana kasoro ni wajibu wa kila mtu kutizama kasoro zipo wapi, na vile vile kukaa na kuyafanyia kazi ili tuwe pamoja sisi Wawakishi humu na mawaziri wetu basi pale panapokuwa na kasoro yoyote basi ni wajibu wetu kufahamishana kwani asiyekubali kukosolewa atakuwa hata ile maadili ya uongozi atakuwa hana. Kwa hivyo tukubaliane kwamba linapotokea tatizo basi tukae pamoja na kufanya solution kwa pamoja.

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nilikuwa nataka kusema sana lakini, kwa sababu hizi ripoti zimetugusa sana na zinatukuna sana, kwa hivyo ninakupongeza kwa kuniachia muda wote huo.

Mhe. Mwenyekiti, nakupongeza kwa kutuachia muda kuchangia ripoti hizi na niseme naunga ripoti hii kama wenzangu walivyokwisha kutangulia, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia fursa ya kueleza machache kuhusiana na ripoti hii ya Kamati ya Viongozi Wakuu wa Serikali. Kabla ya kutoa maoni yangu naomba niungane na wenzangu kusudi kumpongeza mwenyekiti wa hii kamati. Kwa kweli mwenyekiti wa kamati hii kaiwasilisha ripoti hii kitaalamu mno kiasi ambacho nilikuwa ninasinzia lakini ikabidi niamke na kuisikiliza. Nakupongeza sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nianze na suala zima la Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Ofisi hii kama utaangalia taarifa ya kamati hii katika ukurasa wa 13 amesema kwamba kipengele nambari 5 changamoto kwenye utekelezaji wa kazi

katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa 2012/2013, hapa nambari 5, mabadiliko ya tabia na nchi wanaendelea kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii. Kamati imefanya kazi kubwa kuona hili.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna jambo linalomomonyoa uchumi wa nchi hii na kusababisha umaskini kwa kiasi kikubwa sana ni haya mabadiliko ya tabia ya nchi. Sasa mimi nilifikiria hapa kwenye taarifa kwenye utekelezaji wa hii Ofisi ya Rais Makamu wa Kwanza, nilifikiria wangeweza kufanya kazi ya ziada katika kupambana na adui huyu wa mabadiliko ya tabia ya nchi.

Hivi sasa Mhe. Mwenyekiti, kuna hatari ya baadhi ya visiwa kuvikosa katika nchi yetu. Hivi sasa tunalima kwa kubahatisha, kwa sababu mazingira yameathirika na mvua hatuzipati kwa wakati. Nilidhani ofisi hii ingeleta jibu la kutosha juu kwa kiasi gani serikali katika bajeti yake itaangalia udhibiti wa haya mabadiliko ya nchi ikiwa ni pamoja na kutayarisha mikakati madhubuti katika kuleta kilimo cha umwagiliaji na kadhalika, lakini hili sikuliona.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ukimwi. Suala la ukimwi bado linaendelea kupoteza nguvu kazi za nchi hii. Lazima tukumbuke Mhe. Mwenyekiti, kwamba nguvu kazi ya nchi ni pamoja na raslimali watu ambayo ndio nguvu yetu kubwa. Lakini hivi sasa kundi la vijana linaendelea kututoka kuathirika kutokana na maradhi haya ya ukimwi.

Nashukuru jamii imeshafanya iniative kubwa kuona kwamba suala hili la ukimwi kwa kiasi fulani linapungua maambukizi mapya kwa sababu wengi wao ni jamaa wanaojishughulisha na madawa ya kulevya, kwa hivyo *possibility* ya kupata ukimwi watu wa madawa ya kulevya ni kubwa, wananchi kwa *initiative* wakaanzisha suala zima la sober house (nyumba za kubadilisha tabia).

La kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, serikali katika hili hatujaona nguvu zake. Nilidhani katika baadhi ya mambo kwenye wizara tungeona kwamba serikali kwa kiasi fulani imesaidia kiasi fulani kuimarisha hizi *sober house* kusudi hili kundi la vijana kuweza kulisaidia.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo jengine katika hili ni suala la ulemavu kwenye Ofisi ya Rais Makamu wa Kwanza wa Rais. Mimi nilidhani kwamba hili kundi, pamoja na kuambiwa ni lazima lijikite kwenye jamii, lisitengwe na jamii wakati tunajibiwa maswasli asubuhi hapa kwamba serikali haina iniative ya kuwaweka pahala kama walivyoweka watoto wenye mazingira magumu pamoja na wazee. Lakini walemavu hivi wanahitaji Mhe. Mwenyekiti, na wao waangaliwe kwa jicho la kuruma na serikali yetu, angalau kwa kuweza kuboresha miundo mbinu katika maeneo kadhaa ya huduma ikiwa pamoja na hospitali na skuli. Inasikitisha sana Mhe. Mwenyekiti, kwenye hospitali zetu nyingi ziliopo walemavu wanakwenda pale wanashindwa kupima ujauzito kwa sababu hawawezi kupanda ngazi.

Sasa naomba sana serikali Mhe. Mwenyekiti, katika hili ione sasa kuna haja sasa pia walemavu wao kuwekewa miundo mbinu skulini, hospitali, mabenki, kusudi na wao wajisikie kwamba wapo katika nchi yao na wapo huru kabisa.
Baadae nije katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Hapa Mhe. Mwenyekiti, ndio penye matatizo. Mhe. Mwenyekiti, ofisi hii kwanza hii taarifa yao ya karatasi mbili, mimi nasema ni kulidhihaki Baraza. Kwa sababu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ina mambo mengi na kero nyingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika ofisi hii inatupa shida sasa kwamba Mhe. Mohamed Aboud na wenzako; ni watu wazima ambao munaoweza kuzishughulikia hizi kero za muungano, hizi ninadhani hamuziwezi tena tuleteeni wenyewe sasa. Uwezo wa kushughulikia kero za muungano Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hamna uwezo. Haya mambo sasa tuleteeni wenyewe. Ikiwa nyinyi kutaka tu habari ya mafuta munatetemeka, kutaja neno mafuta munatetemeka, kutaja Zanzibar kuingia katika FIFA munatetemeka, munaweza nini jamani. (*Makofi*).

Mimi hapa Mhe. Mwenyekiti, ndio ninapopata machozi, muungano ndio huu bwana, bega kwa bega baina ya Karume mkubwa na bwana Nyerere wapo bega kwa bega katika kukagua paredi (*picha*). Huu ndio muungano.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa wakati ambao tumejipangia kuendelea na shughuli zetu hapa tumefikia mwisho. Katika orodha yangu nina orodha ya wachangiaji 24. Wachangiaji waliobahatika kupata ni kwenye 10 tu. Sasa kuna njia mbili za kufanya.

Moja tuongeze muda ili wachangiaji wafanye kazi hiyo tumalize hii kazi leo au pili tukatishe hapa wachangiaji kesho tuje tuwape nafasi mawaziri pamoja na mwenyekiti kwa majumuisho. (*Kicheko*).

Sasa kama ni hivyo tumuombe Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais atuongezee muda ili kupata nafasi.

Wajumbe: mmm! aah!

Mhe. Mwenyekiti: Basi kama yote munayakataa, naomba kuchukua fursa hii kukushukuruni sana Waheshimiwa Wajumbe kwa namna tulivyoshiriana mpaka tukaweza kufikia hapa. Sasa basi naahirisha Baraza hili hadi kesho asubuhi saa 3.00 barabara.(*Makofi*).

(Saa 1.45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 12/042013 saa 3.00 asubuhi)